Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

### MKUTANO WA KUMI NA TANO

**Kikao cha Pili – Tarehe 22 Aprili, 2009**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kwanza kabisa napenda niwasalimu na kwamba tumetoka kwenye mkutano wa *steering committee* ya *SADC parliamentary forum* tulikuwa tunajaribu kumpata katibu mtendaji wa *SADC* lakini wale wote walioomba hawakuwa na sifa zinazostahili kwa hiyo sasa hivi bado tunatangaza wale wenye sifa za kustahili waweze kuomba tena katika muda wiki tatu.

Kwa hiyo, na Watanzania wote wenye sifa zinazostahili wawe na *master degree*, wawe wame-serve katika institution miaka isiyopungua kumi na kama alishakuwa na sifa za kuwa Mbunge au amefanya kazi na Bunge anakuwa na sifa zilizoongezeka. Kwa hiyo naomba tuendelee na kikao.

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Taarifa ya Mwaka wa Hesabu za Shirika la Viwango Tanzania *(TBS)* kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2007 *[The Annual Report and Accounts of the Tanzania Bureau of Standards (TBS) for the year ended 30th June*, 2007].

### MASWALI NA MAJIBU

Na. 14

**Sheria KUhusu Haki ya Kuchagua au Kuchaguliwa**

**MHE. HEMED MOHAMMED HEMED** aliuliza:-

Kwa kuwa, Ibara ya 5(1) na (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977 inatoa haki ya kila raia aliyetimiza umri wa miaka 18 kupiga kura wakati wa uchaguzi na kwa kuwa Katiba iko kimya kuhusu watanzania wanaoishi nje ya nchi kutekeleza haki yao hiyo na kwamba Rais wa Tanzania alipotembelea nchi ya Namibia mwezi Aprili, 2006 aliahidi kuwa Watanzania waishio nje ya nchi wataweza kupiga kura katika uchaguzi wa mwaka 210:-

(a) Je, Serikali imechukua hatua gani kupitia sheria ya uchaguzi katika kuboresha hali hii ili kuweza kutoa haki kwa Watanzania waishio nje?

(b)Je, Serikali inasema nini juu ya haki ya kuchagua na kuchaguliwa kwa raia walio ndani ya nchi ambao wako mahabusu, kifungoni, wagonjwa na walemavu ambao mazingira yao yanawazuia kufika katika maeneo ya kujiandikisha na kupiga kura?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA NA URATIBU WA BUNGE** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hemed Mohammed Hemed, Mbunge wa Chonga lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kwa mujibu wa Ibara ya 5(1) na (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano waTanzania kila ria wa Tanzania aliyefikisha umri wa miaka 18 anayo haki ya kupiga kura katika uchaguzi unaofanywa Tanzania na wananchi isipokuwa kama; mtu huyo ana uraia wa nchi nyingine, mtu ana ugonjwa wa akili, ametiwa hatiani kwa makosa fulani ya jinai, ameshindwa kuthibitisha au kutoa kitambulisho cha umri, uraia au uandikishaji kama mpiga kura. *(Makofi)*

(b)

Kwa mujibu wa Ibara ya (1) na (2) raia wote waishio nje ya nchi walio mahabusu, wanaotumikia vifungo chini ya miezi sita, wagonjwa na walemavu wana haki sawa na raia wengine ya kupiga kura kumchagua Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Raia hao hawawezi kupiga kura za Wabunge wala madiwani kwa kuwa wanaishi nje ya majimbo na kata zinazofanya chaguzi huo.

Sheria za uchaguzi kwa sasa hazijaanisha utaratibu unaowawezesha raia waishio nje ya nchi kupiga kura. Hata hivyo Serikali imekuwa ikilitafakari suala hili katika utekelezaji wake hususan kuwapata watendaji wa kusimamia zoezi hilo kote ulimwenguni waishipo raia wa Tanzania na namna ya kusafirisha vifaa vya uchaguzi katika maeneo yote na kukusanya matokeo kwa wakati ili kutochelewesha utangazaji wa matokeo.

Kwa kuwa chaguzi zetu zinatakiwa ziwe za wazi ni budi kuangalia pia uwezekano wa vyama vha siasa kuweka mwakala wao katika vituo vya kupigia kura katika nchi hizo wanazoishi Watanzania hao.

Kwa ujumla Serikali inatafakari jambo hili la maamuzi yakifikishwa ili kuweka utaratibu wa kuwa wezesha Watanzania waishio nje ya nchi kumpigia kura Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema hapo awali, raia walioko mahabusu na wale wanaotumikia vifungo vya chini ya miezi sita wana haki pia ya kupiga kura. Kifungu cha 13(6) cha sheria ya uchaguzi Na. 1 ya mwaka 1985 kinaruhusu raia hawa kupiga kura kama wataruhusiwa na sheria inayosimamia mahabusu na vifungo vyao.

Katika Uchaguzi Mkuu uliopita mwaka 2005, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilifanya mashauriano na Idara ya Magereza ili kuona uwezekano wa kundi hili kupiga kura.

Hata hivyo mashauriano hayo hayakuweza kufikia mwisho ili kuliwezesha kundi hili kupiga kura. Kwa sasa Tume ya Taifa ya Uchaguzi inaendelea kufanya mashauriano na idara ya magereza ili kukamilisha utaratibu utakaowezesha kundi hili la mahabusukupiga kura kwa uchaguzi mkuu wa 2010.

Kwa upande wa walemavu na wagonjwa, sheria ya uchaguzi inaruhusu raia hawa kwenda katika vituo vya kupiga kura na jamaa zao ili wawasaidie katika kupiga kura. Aidha, Tume inautaratibu wa kuwapa kipaumbele cha kupiga kura mara wafikapo katika vituo vya kupigia kura.

Katika Uchaguzi wa uliopita wamwaka 2005, Tume ilitayarisha kifaa maalum kiitwacho "*tactile ballot folder*" kwa ajili ya kuwawezesha walemavu wasioona na waliotaka kupiga kura kuwa wao wenyewe kufanya hivyo bila kutegemea msaada wa mtu mwingine.

Kwa uchaguzi unaokuja Tume itaendelea kufanya mashauriano na makundi mbalimbali ya walemavu ili kuweza kuboresha na kuinua zaidi ushiriki wao katika upigaji kura.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa suala la raia wanaoishi nje ya nchi kuweza kupiga kura sio suala geni nchi ambazo hata tumesaidia kukomboa kama Msumbiji tayari wameweza kufanya hivyo, inakuwa Serikali katika kipindi chote hichi cha mfumo wa vyama vingi ikashindwa hata kuiga nchi ambayo sisi tumeisaidia kuikomboa na kuendelea kuvunja Katiba ya nchi ya kumnyima raia kupiga kura.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA NA URATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli suala la Watanzania wanaoishi nje kupiga kura wakati wa uchaguzi mkuu sio suala geni limeongelewa kwa muda mrefu lakini tujue kwamba kila nchi ina mazingira yake.

Watanzania wanaoishi nje wako wengi sana usishangae kuna Watanzania hata Papua Newgine, wako Mangolia, wako Feniland, na kuna kikundi kikubwa sana cha Watanzania kule London, hata Euston, Califonia na kadhalika. Sasa kwa ajili ya uendeshaji wa uchaguzi wa wazi na haki kutendeka na vyama siasa kuwapeleka wakala wao huko kwa kweli inahitaji maandalizi makubwa sana. (*Makofi*)

Hata nchi kubwa kama Afrika Kusini haikuwa na vituo kote duniani ni kwenye miji mikubwa mbalimbali tu ya dunia ambayo imepelekewa ….paper na ndiko wanakopigia. Kama nilivyosema katika jibu la msingi suala hili bado tunalitafakari pamoja na vyama vya siasa pale maafikiano yakifikiwa basi hatutasita kuliweka eneo hili la uchaguzi katika sheria yetu ya uchaguzi.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, ninaomba kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa nchi zetu za *SADC* zinatabia za kufanya kazi kwa pamoja hasa katika mambo ya chaguzi hizi na kwa kuwa *South Africa* tayari wamefanya kazi hii hata kama ni kwa miji mikubwa baadhi ya miji mikubwa. Ni kwanini Watanzania tusianze basi katika ile miji mikubwa ili tutende haki kwa hawa Watanzania walio nchi ya nje.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA NA URATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni suala moja kutowatendea haki Watanzania walio nje ili wapige kura lakini ni jambo tofauti kabisa kuhakikisha kwamba uchaguzi kama huo utakuwa wa wazi na wa haki kwa vyama vyote vya siasa. Lengo letu ni kwamba angalau kuwe na uchaguzi ambao utafanikisha matokeo haraka iwezekanavyo. Uchaguzi ambao utakubaliwa na kuafikiwa na vyama vyote vya siasa.

Na. 15

**Uuzwaji wa Maeneo ya Wazi**

**MHE. ANNA MAULIDAH KOMU (K.n.y. MHE. HALIMA J. MDEE)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ipo kwenye mchakato wa kupima vijiji na kwamba wakati wa zoezi hilo kuna baadhi ya maeneo huachwa wazi kwa madhumuni ya kutumika kwa shughuli za maendeleo ya kijiji.

Je, Serikali ina taarifa zozote kuhusiana na uuzwaji wa maeneo yaliyo wazi katika kijiji cha Mpiji, kati ya Mbweni, Jimbo la Kawe?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na mchakato wa kupima mipaka ya vijiji na kutoa cheti cha Ardhi kwa kuzingatia (Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya mwaka 1999 kwa lengo la kutatua migogoro ya mipaka na kuwezesha vijiji kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi. Ili kufanikisha azma hiyo, maeneo ya shughuli za kiuchumi na ya huduma za jamii kama vile shule, zahanati, pamoja na maeneo ya wazi, maeneo ya makaburi, michezo hupimwa na kutengwa kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kijiji cha Mbweni ni mojawapo ya vijiji 14 katika Manispaa ya Kinondoni ambavyo viliandikishwa chini ya kifungu cha 22 cha sheria Na. 7 ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) ya mwaka 1982. Vijiji hivyo vilifutwa na kuondolewa kwenye daftari la kuandikisha vijiji kwa sabbu vimekuwa ni sehemu ya maeneo yanayohitaji kuendelezwa kwa shughuli za kimji na vimekosa sifa ya kuendelea kuwa vijiji. Vilevile kuwezesha utekelezaji wa *GN Na. 231* ya tarehe 13 Agosti 1993 ambayo ilitoa tamko la kuendelezwa kwa vijiji hivyo ikiwa ni pamoja na kijiji cha Mbweni kwa kuzingatia sheria ya Mipangomji Sura Na. 378 ya mwaka 1956 na sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la Mpiji Kata ya Mbweni ni moja kati ya maeneo yaliyotwaliwa na Wizara ya Ardhi na kupimwa viwanja katika mradi wa upimaji viwanja elfu ishirini (20,000) mwaka 2002/2003 kwa ajili ya kukabiliana na upungufu wa viwanja na tatizo makazi Jijini Dar es Salaam. Katika mradi huo wa viwanja vya matumizi mbalimbali ardhi vilipimwa na kuuzwa.

Aidha, viwanja vya makaburi, maeneo ya wazi maegesho (*parking*) na maeneo ya soko vilipimwa na havikuuzwa bali vilikabidhiwa kwa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni ili vitumike kwa manufaa ya Umma na kwa matumizi yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba hadi sasa ofisi yangu haijapokea taarifa zozote zinazohusu kuuzwa kwa maeneo 43 yaliyotengwa kwa matumizi ya wazi (*open space)* katika eneo la la Mbweni Mpiji. Endapo ofisi yangu itabaini na kuthibitisha maeneo yameuzwa kinyume cha Sheria hatua zinazostahili zitachuliwa.

**MHE. RITA L. MLAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini ningependa kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwa kama Mbunge wa eneo la hilo napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba kuna maeneo ambayo yalipimwa kwa ajili ya shule, makaburi, zahanati na huduma za jamii mbalimbali ambayo mpaka sasa hivi hayajaweza kutumikiwa na ilikisiwa au inaeleweka kwamba yameuzwa kama viwanja. Ningemwomba Mheshimiwa Naibu Waziri tuwasiliane ili tuweze kubainisha maeneo

hayo na tunaomba ikiwezekana Serikali kupitia Manispaa ya Kinondoni wakubali kuyalipia hayo maeneo ili Wizara ya Ardhi iweze kuwamilikisha na kuweza kuyatumia kwa manufaa yanayohusika.

**NAIBU SPIKA:** Anasema je, Waziri anakubali kufanya hiyo. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, itakuwa ni faraja kubwa sana kufanya hivyo na nitakuwa tayari kufanya hivyo isipokuwa nilitaka niseme jambo moja ambalo amelisemea hapa kilichokuwa kinazungumzwa kwenye swali hili kilikuwa kinahusu open space yaani maeneo ya wazi lakini sasa Mheshimiwa anasema kwamba yako maeneo mengine ambayo yalikuwa yametengwa kwa ajili ya shule, kwa ajili ya zahanati na kwa ajili ya taasisi mbalimbali. Nataka niseme tu hapa kwamba katika maeneo haya ambayo yametengwa kwa ajili ya shule na kwa ajili ya zahanati na kwa ajili ya taasisi nyingine mbalimbali, yako maeneo yaliyotengwa kwa ajili public institution lakini kuna maeneo mengine ambayo yametengwa kwa ajili ya shughuli binafsi pia ambazo zimelenga katika kujenga zahanati shule za watu binafsi kama ilivyoelezwa hapa. Vyovyote vile itakavyokuwa mimi nitakuwa tayari kufuatana naye ili tuweze tukaliangalie jambo hilo wote kwa pamoja. (*Makofi*)

Na. 16

**Kujenga Barabara kwa Kiwango cha Lami na Kujenga Daraja la Buyogo Tarafa ya Mwanashimba**

**MHE. BUJIKU P. SAKILA** alijibu:-

Kwa kuwa, wananchi wa Kwimba hususan tarafa ya Mwanashimba wanaitegemea sana kiuchumi barabara Mwamhaya hadi Itongwitale na daraja la Buyogo katika mto Mwame na kwamba miaka mingi miundombinu hii imekuwa ikiharibika mara kwa mara kutokana na ongezeko la magari na mvua zinyeshazo katika eneo hilo:-

(a)Je, mbali na upatikanaji wa fedha za kutosha Serikali inasubiri vigezo vipi ili ishawishike kuamua kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami na kujenga daraja la Buyogo?

(b)Je, kuanzia miaka ya 1995 hadi sasa Serikali imetumia fedha kiasi gani kukarabati barabara hiyo na daraja hilo?

(c)Je, Serikali haioni kuwa kutokujenga barabara hiyo mapema ni kudumaza kasi ya maendeleo ya tarafa ya Mwamashimba?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bujiku Philip Sakila, Mbunge wa Kwimba, swali lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara kutoka Ng'hwamhaya hadi Itongoitale yenye urefu wa kilometa 51 ni barabara ya Mkoa ambayo kutokana na kupitisha magari makubwa, huharibika mara kwa mara. Lakini pia mvua za mara kwa mara huchangia kuharibika kwa barabara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inakubaliana na Mheshimiwa Mbunge ya kuwa suluhisho la kudumu la kuharibika mara kwa mara kwa barabara hiii ingelikuwa ni kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami.

Lakini kutokana na ufinyu wa Bajeti ya Serikali, kwa sasa barabara hii itaendelea kuimarishwa kwa kuifanyia matangenezo ya mara kwa mara kutegemeana na uwezo wa Bajeti ya Serikali. Kwa sasa Serikali inaelekeza nguvu katika kukamilisha miradi ambayo imeshaanza.

Aidha, daraja la Buyogo limekuwa likifanyiwa matengenezo ya mara kwa mara ili kuliwezesha liendelee kupitika kwa kipindi chote cha mwaka. Ikumbukwe ya kuwa daraja hili lipo kwenye kona ambapo kitaalam si salama sana kwa watumiaji wa barabara hiyo. Serikali kupitia wakala wa barabara Mkoani Mwanza iko katika mchakato wa kutafuta fedha za kuijenga upya daraja hili na kulihamishia sehemu salama zaidi. Katika mwaka 2009/2010 Serikali inatarajia kutenga fedha kwa ajili ya kufanya usanifu wa daraja hilo na hatimaye ujenzi kufanyika eneo linalofaa.

(b)Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya shilingi 477,345,600/= zimetumika kukarabati barabara hii sehemu yenye urefu wa kilometa 15 katika kipindi cha miaka sita iliyopita. Aidha, katika mwaka huu wa fedha 2008/2009 Wizara yangu imetenga jumla ya shilingi 92,990,600 kwa ajili ya kuifanyia matengenezo maalum barabara hii ya Ng'hwamhaya – Itongoitale ambayo jumla ya kilometa 13 zinatarajiwa kufanyiwa matengenezo hayo.

(c)Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inafanya na inaendelea kufanya juhudi mbalimbali kuinusuru barabara hii ikiwa ni pamoja na kuitengea fedha kila mwaka ili ipate matengenezo ya kawaida na maalum, kuiwezesha ipitike kwa kipindi chote cha mwaka.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana. Napenda niishukuru Serikali kwa kuanza kufikiria ujenzi wa daraja la Buyoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi wa swali langu ulikuwa unatokana na kuzionea huruma fedha zinazotolewa kila mwaka kutengeneza barabara hiyo halafu baada ya muda mfupi inaharibika. Je, Serikali haioni kwamba ni vyema sasa angalau kujengwa kwa awamu hasa yale maeneo ambayo ni korofi sana wajenge kwa kiwango cha lami? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nipokee pongezi zake kwa niaba ya Serikali kwa kutambua jitihada zinazofanyika ili

kunusuru barabara ambayo alikuwa ameiulizia. Lakini pili kuhusu swali lake aliyoeleza ni kweli kwamba tunapotengeneza barabara hizi mara kwa mara na kuendelea kuharibika fedha hizi zinakuwa kama hazifanyi kazi ambayo inaonyesha *impact.*

Lakini kama nilivyoeleza katika jibu la msingi kwamba tungekuwa na fedha za kutosha za kuweza kujenga barabara hizi kwa kiwango cha lami tungeweza kufanya. Lakini hata hivyo wazo lake la kwamba tuanze kufikiria kujenga kidogo kidogo barabara hizi kwa kiwango cha lami ndiyo kazi ambayo imeshaanza kufanyika sasa hivi kuna miradi mingi ya barabara za lami sasa hivi inafanywa lengo ni kuhakikisha kwamba hatimaye barabara zote ziweze kuwa za lami tutakapokuwa tumekamilisha azma ya Serikali katika kuimarisha barabara zetu.

Na. 17

**Uhakika wa Mbegu za Kitanzania**

**MHE. JANETH B. KAHAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa, kuna mbegu nyingi za asili za nafaka, mboga na kadhalika, ambazo tangu zamani zimekuwa zikutumika kama chakula kwa mfano mbegu za mpunga aina ya Gamti, Mbao, Mbili, Kahogo, Faya, Sindano ambazo kwa hivi sasa zimepotea kabisa Tanzania:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha mbegu hizi nzuri za Kitanzania zinazovumilia ukame na zenye ladha nzuri ya kuhamasisha hamu ya kula ili zilimwe hapa nchini kuliko kuzingatia upandaji wa mbegu ya "*Super*" peke yake.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Napenda kujibu swali la Mheshimiwa Janeth Bina Kahama, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

- Mbegu ya Gamti Mbawa Mbili, Kahogo, Faya na Sindano zipo na zinalimwa katika maeneo hapa nchini kama ifuatavyo:-

- Mbegu ya Gamti inalimwa Mkoa wa Ruvuma maeneo ya Tunduru;

- Mbegu ya Mbawa Mbili, inalimwa maeneo ya Ukanda wa Ziwa Victoria;

- Mbegu ya Kahogo inalimwa maeneo ya Morogoro na Mbeya;

- Mbegu ya Faya inalimwa katika maeneo ya Ukanda wa Ziwa Victora.

Mbegu alizozitaja Mheshimiwa Mbunge, bado zinatunzwa katika Taasisi za utafiti za kimataifa kama vile *International Rice Research Institute (IRRI)* iliyopo

Philippines na *National Plant Genetic Resource Centre (NPGRC)* iliyopo *TPRI,* Arusha na vituo vya utafiti wa mpunga vya *KATRIN – Ifakara* na Chollima – Dakawa Mkoani Morogoro. Napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba aina za mbegu za mpunga alizozitaja pamoja na "*super*" zote zinatoa mavuno kidogo kwa wastani wa tani 3.5 – 4.5 kwa hekta ukilinganisha na mbegu za kisasa kama vila *TXD 306 (SARO 5), TXD 85* na TXD 88 ambazo zina ladha nzuri na zinatoa mavuno kati ya tani 5 hadi 7 kwa hekta. Aidha mbegu hizo alizozitaja Mheshimiwa Mbunge, zinashambuliwa na magonjwa na kwamba siyo zote zinazovumilia ukame. Ni mpunga aina ya Gamti tu ambao unavumilia ukame. Jukumu la Serikali ni kuhakikisha kwamba utafiti wa mazao likiwemo zao la mpunga, unalenga kupata mbegu bora zenye kutoa mavuno mengi, zinazokomaa haraka zenye kuvumilia magonjwa na ukame na zenye kuvumilia magonjwa na ukame na zenye kukidhi mahitaji ya soko.

**MHE. JANETH B. KAHAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa katika kipindi cha miaka michache iliyopita nchi yetu ilikuwa imeagiza minazi mifupi kutoka nchi nyingine minazi ambayo kwa kweli haikuweza kuboresha maisha ya ukulima katika ukanda wa Pwani. Sasa nilitaka kushangaa kwa nini bado Serikali baada ya kuona tatizo hilo bado tunaingiza mbegu nyingine kama vile mbegu za migomba, mbegu za mihogo, mbegu za miembe na pia kuzipandikiza tukichukua mbegu za kutoka nje na nyingine. Sasa je, sisi pia mbegu zetu za kutoka hapa za asilia zinapelekwa nje?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niseme kwamba siyo kila zao la *research* ambalo linatoa mbegu ambazo si nzuri. Tulishatoa hapa majibu tukasema wakulima wa nazi walime *East African Tall* kwa sababu ina sifa za kuzaa zaidi ya kustahimili ukame na magonjwa. Sasa katika suala la *hybrid* katika mpunga ni kwamba *hybrid* ni *cross breeding* ya *breed* mbili yaani aina mbili za mpunga ambazo kwa kuchanganya zinaleta sifa ambazo zinatakiwa kwenye mazao. Kwa mfano mbegu zetu za mpunga kwa sasa zile ndani zenyewe hazizalishi sana. Sasa tunachanganya na zile za nje ambazo zinazalisha sana na zenye kuvumilia magonjwa mbalimbali. Sasa niseme kwa kuwa na mbegu zina sifa ambazo zinatakiwa inawezekana kwamba kuna nchi za jirani ambazo zinatumia mbegu zetu kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inafanya utafiti kwa kila ambalo ni zuri kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunapata mbegu bora wakati wote na utafiti huu unachukua muda mrefu.

**MHE. BASIL P. MRAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kuna ushahidi kwamba mpunga aina ya basmati ambao ni wa asili ya Kihindi watu fulani huko *America* wameiba na kusema ni wa kwao na kuchukua hati miliki ya mpunga huo.

Na kwa kuwa, mpunga aina hii iliyotajwa hapa kama alivyoeleza Naibu Waziri ni ya asili ya uasili wa Tanzania na kwa kuwa tumeshaanza kazi ya kuboresha mpunga huo. Je Wizara haioni ni busara kuchukua hati miliki ya uasilia wa mpunga huo ili watu wengine wasije wakauiba na kufaidika kimataifa na kimapato kutokana na mpunga wetu wa Tanzania?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, Mbunge wa Rombo, kama ifuatavyo.

Ushauri wake ni mzuri sana na Serikali itauzingatia.

Na. 18

**Mafanikio ya Uanzishwaji wa Kodi ya VAT**

**MHE. ANNE K. MALECELA** aliuliza:-

Kwa kuwa, serikali ilianzisha *VAT* mwaka 1998 kwa nia ya kupunguza ukwepaji wa kodi na kuwa na mfumo endelevu na mwepesi wa kukusanya mapato nchini.

Je, serikali inaweza ikawaambia Watanzania imefanikiwa kwa kiasi gani katika lengo hilo ?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela kwa niaba ya uongozi wa Wizara ya Fedha na Uchumi, napenda kumpongeza Mheshimiwa Anne Kilango Malecela kwa tuzo aliyoipa, namtakia kila la kheri katika majukumu yako. Kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Same Mashariki kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)*, ilianzishwa na Serikali mwaka 1998 na kuchukua nafasi ya Kodi ya Mauzo ya mwaka 1976. Sehemu ya Kodi ya Ushuru wa Stempu uliokuwa unatozwa chini ya Sheria ya Ushuru wa Stempu ya mwaka 1972; Sheria ya Starehe ya mwaka 1972 ; na Sheria ya Ushuru wa Hoteli ya mwaka 1972.

Mheshimiwa Naibu Spika, *VAT* ni kodi inayolipwa na mlaji wa bidhaa au mtumiaji wa huduma inayotozwa VAT wakati bidhaa au huduma hiyo inapokuwa imeuzwa na mfanyabiashra aliyesajiliwa kwa ajili ya kukusanya kodi ya *VAT*. Kodi hii ina manufaa zaidi ukilinganisha na kodi za mauzo. Kwanza kwa kuwa na wigo mpana wa kutoza kodi. Aidha, kodi hii ni kichocheo cha uwekezaji kwani bidhaa zote za uwekezaji (*Capital Goods for Investment*) zimesamehewa kodi ya *VAT*, uuzaji wa bidhaa nchi za nje hutozwa VAT katika kiwango cha 0% na hivyo kufanya *VAT* kuwa kichocheo cha uwekezaji na ukusaji uchumi kwa kueka mazingira mazuri ya ushindani wa soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kodi ya *VAT*, Serikali imefanikiwa kwa kiwango kikubwa katika kupunguza kiwango cha ukwepaji kodi na kurahisisha mfumo wa kukusanya mapato ya Serikali. Katika mfumo huu, mapato ya serikali yaliongezeka toka shilingi milioni 138 bilioni kutokana na kodi ya mauzo mwaka 1997/98 hadi shilingi 219 bilioni katika mfumo mpya wa kodi ya *VAT* mwaka 1998/99, sawa na ongezeko la

58.7% na 1% ya pato la Taifa. Mapato ya kodi ya VAT yamekuwa yanaongezeka mwaka hadi mwaka hadi kufikia shilingi 1.0 trillion billion mwaka 2007/08, sawa na 5% ya pato la Taifa. Utaratibu wa wafanyabiashara wa kujikadiria wenyewe (*Self Assessment*) kodi ya kulipwa umerahisisha sana utawala chini ya kodi ya *VAT,* ukilinganisha na kodi ya mauzo. Aidha, ukusanyaji wa *VAT* unafanyika katika hatua mbalimbali kuanzia mzalishaji, msambazaji wa kati na muuzaji wa rejareja na hivyo kufanya ukwepaji wa kodi yote kuwa mgumu kidogo ukilinganisha na kodi ya mauzo. *(Makofi)*

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri, lakini naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Nakubali upande mwingine kama alivyoongea Mheshimiwa Waziri kama ni kweli lakini bado naiomba Serikali iwe makini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wafanyabiashara wakubwa ambao wananunua bidhaa kutoka kwenye viwanda wana tabia moja ambayo ni mbaya sana na inafanyika karibu nchi nzima. Wao wanapokwenda kununua bidhaa viwandani wanalipia *input VAT*, wanapokuja kuuza bidhaa zile kwa watumiaji wa mwisho wanawalaghai wananchi na kuwaonyesha kwamba ukichukua risiti ambayo ina 20% ya *VAT* bei ni kubwa lakini usipochukua risiti bei ni ndogo na kwa hivyo wanawafanya wananchi wakwepe kulipa *output VAT* ambayo inakuwa ni kulinyima taifa mapato yake.

Je, Serikali katika hili hamuoni kwamba wafanya biashara wakubwa wanaiibia Serikali na kuwafanya wananchi wakose haki yao ya kupata mapato ya nchi yao?

Mheshimiwa Naibu Spika, sifa ya kodi nzuri ni ile kodi ambayo Serikali inawatoza wananchi wake ikiangalia na nguvu ya uchumi wa nchi yake. Nimekwenda kufanya *research* vizuri nikaona kwamba nikichukua mfano tu wa nchi mbili, yaani *South Africa* na Tanzania, *South Africa* ina uchumi wa juu sana na Tanzania uchumi wake ni mdogo *South Africa GDP* yake ni 10,000/= *U.S. Dollar,* Tanzania ni 1300 *U.S. Dollar* lakini *South Africa* ina *charge VAT 14%* na Tanzania 20%.

Je, Serikali hamwoni kwamba *VAT 20%* imekuwa juu sana kulinganisha na uchumi wa Watanzania na hivyo ukwepaji kodi utaendelea kuwepo pale. Je, Serikali hamuwezi kurekebisha mara moja ili wananchi waweze kulipa *willingly* kuliko ambavyo wanaendelea kukwepa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, kama ifuatavyo.

Kwanza ni kosa kwa mfanyabiashara yeyote yule ambaye amesajiliwa chini ya *VAT* kutokutoa risiti kwa visingizio kwamba ukitaka na risiti bei hii bila risiti bei itakuwa chini. Hilo ni kosa na ninawaomba ndugu zangu wafanyabiashara wasawazishe tutakapokuka kukamatana katika kosa hili nadhani kutakuwa hakuna msamaha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili nataka nikubaliane na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela kwamba kiwango cha *VAT* cha 20% kweli ni kikubwa kweli tumelisikia hili na tunaliangalia kwa undani kabisa kwa sababu mbili kubwa. La kwanza, *VAT* siyo kodi ya Muungano lakini wakati tunaweka viwango hivi Serikali mbili yaani Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Muungano tulikaa pamoja kuweka kiwango kimoja. Tukipunguza *VAT* kwa upande wetu tunajaribu kuangalia athari zake katika mapato yetu na watu na wapi tuweze kuongeza kodi ili zile athari tuweze kujifidia. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Mbunge vuta subira tunaliangalia kwa undani kabisa tukishirikiana na wenzetu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar pamoja na Jumuiya ya Afrika Mashariki. (*Makofi*)

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Swali langu litakuwa linafuatilia kwamba *VAT* imeondolewa kwenye *capital goods* lakini *VAT* iko kwenye malighafi na kwa sababu iko kwenye malighafi na *rate* ya Tanzania ukilinganisha na wabia wenzetu wa Afrika Mashariki sisi tuko juu, maana yake hata zile *efforts* za kusukuma mauzo yetu nje zinakuwa zinagonga mwamba.

Kwa hiyo, ninaiomba Wizara iangalie suala zima la kuanisha *VAT* katika Afrika Mashariki ili kuweza kusukuma *export* zetu katika soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**NAIBU SPIKA:** Mnakubali? (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kaboyonga kama ifuatavyo.

Kwanza nakubaliana naye katika kukuza uchumi lazima tukuze export zetu na hili alilolizungumza kwamba *VAT* katika malighafi tuweze kuiangalia ili tuweze kukuza uchumi nakubaliana na wewe tutaliangalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Na. 19

**Ardhi Kuwa Sehemu ya Makubaliano ya Jumuiya ya Afrika Mashariki**

**MHE. LAZARO S. NYALANDU** aliuliza;

Kwa kuwa, Ardhi ni urithi wa pekee kwa wananchi wa Tanzania na kwa kuwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wanahimiza ardhi iwe sehemu ya makubaliano ya Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC).*

Je, Serikali itawathibitishia wananchi wa Tanzania kuwa kamwe ardhi ya Tanzania itabaki kuwa mali yao na kwamba haitakuwa sehemu ya makubaliano?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Lazaro Samuel Nyalandu, Mbunge wa Singida Kaskazini, napenda kutoa maelezo yafuatayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jumuiya ya Afrika Mashariki iko katika maandalizi ya kuanza kutekeleza hatua ya Pili ya Mtangamano wa Afrika Mashariki yaani Soko la Pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Majadiliano ya Soko la Pamoja yalianzia Jijini Arusha mwezi Aprili, 2008. Timu ya Wataalamu ya majadiliano kutoka Nchi Wanachama ilikubaliana jinsi ya kuendesha majadiliano. Majadiliano hayo yanafanyika katika ngazi tatu ambazo ni ngazi ya Wataalamu, Makatibu Wakuu na Baraza la Mawaziri. Wakuu wa Nchi wanatarajiwa mwishoni mwa mwezi huu kupokea taarifa ya majadiliano ya Soko la Pamoja na kutoa maamuzi na maelekezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu kuanza kwa majadiliano hayo makubaliano yamefikiwa katika maeneo ya msingi. Maeneo yaliyokamilika ni Utangulizi, Misingi ya Malengo, Uhuru wa bidhaa kutoka sehemu moja hadi nyingine, taratibu za kufuata ili kupata ajira ndani ya Afrika Mashariki, taratibu za kuruhusu Mitaji kutoka sehemu moja hadi nyingine ndani ya Jumuiya, taratibu za utoaji Huduma, utaratibu wa kutoa haki ya kuwezesha kuanzisha shughuli za kiuchumi na taratibu za kutoa haki ya kuishi sehemu yoyote ndani ya Afrika Mashariki kwa lengo la kushiriki shughuli halali kiuchumi au kufanya kazi inayokuwa imepatikana kulingana na taratibu za ajaira zitakavyokuwa zimebainishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ambayo hayajafikiwa muafaka katika majadiliano ya Soko la Pamoja, ni suala la Ardhi, matumizi ya vitambulisho vya kitaifa kama hati ya kusafiria, na Ukazi wa kudumu. Maeneo hayo yatawasilishwa katika Kikao cha Wakuu wa Nchi (*Summit*) kitakachofanyika mwishoni mwa mwezi Aprili, 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli ardhi ni urithi muhimu kwa wananchi wa Tanzania hivyo Serikali inachukuliwa kila juhudi kuhakikisha kuwa suala la ardhi halijumuishwi katika makubaliano ya itifaki ya Soko la Pamoja na tutaendelea kusisitiza kwamba suala la ardhi liongozwe na sera na Sheria za ndani za nchi wanachama kutokana na unyeti waka.

**MHE. LAZARO S. NYALANDU :** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana na ya kuridhisha kuhusiana na swali nililouliza, nakushukuru sana na ninaipongeza sana Serikali kwa huu msimamo thabiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhana ya zamani sana ya mtu kuitwa Land lords au Bwana ardhi ilitokana na ukweli kwamba wale watu walimiliki ardhi, na ardhi ya Tanzania inamtosha kila Mtanzania kuweza kuwa Land lord, kila mwanakijiji kuweza kuwa Mama ardhi au Bwana ardhi lakini ni mpaka ile ardhi itakapomilikishwa kisheria.

Naomba nipate ufafanuzi wa Serikali ni lini hili litafanyika la kuwamilikisha wananchi wetu ardhi kisheria kuanzia vijiji na taasisi zake.

La pili, wananchi wa Tanzania watakapokuwa Mabwana ardhi na hizo ardhi zikaweza kuwekwa kama dhamana katika mabenki, hii dhana ya watanzania ni maskini sana itapotea, ninaomba statement ya Serikali kwamba wanalifuatilia hili na wanatambua kwamba ardhi itapunguza sana kwa kiasi kikubwa hii hali ya umaskini inayojulikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Swali limekwepa toka *East Africa* mpaka Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, majibu tafadhali !

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI :** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa ….

**NAIBU SPIKA :** Kwa niaba yako mwenyewe, hakuna cha niaba ya *East Africa* hapa !

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI :** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu, Mbunge wa Singida Kaskazini, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba ardhi ndiyo raslimali ambayo kila Mtanzania anayo au anaweza kuwa nayo kwa sababu ya Sera yetu nzuri kwamba ardhi ni mali ya umma.

Serikali sasa hivi ina mpango wa kuanza kuwamilikisha ardhi mpaka wanavijiji liko swali baadaye tutalijibu katika Bunge hilihili kikao cha leo kuonyesha kwamba mchakato wa kuanza kuwamilikisha wanavijiji ardhi yao imekwishaanza, kasi si kubwa sana kwa sababu inategemea na fedha yaani waliopima ardhi kuna gharama zake lakini kazi imeanza na nitaifafanua kwenye swali ambayo nitajibu hivi punde.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa na mimi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na

majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri na ya sasa hivi ya Mheshimiwa Waziri ambayo nina hakika Watanzania watayafurahia sana.

Kwa kuwa, kimsingi katika makubaliano haya ya Afrika Mashariki, suala la ushirikiano kwa mbali kabisa ukilitazama linahusisha na namna gani watu katika soko la pamoja watakavyoweza kutembea katika maeneo haya na kufanya shughulimbalimbali ikiwa ni pamoja na matumizi ya ardhi.

Je, inachukuliwa hatua gani hasa kuhakikisha maana yake unaweza ukasema kuwa ardhi inatawaliwa na Sheria za nchi, lakini kiujanjaujanja kama ambavyo sasa hivi inafanyika watu wengi kutoka nje wananunua ardhi nyingi katika nchi yetu. Hili mnalifuatiliaje katika Wizara Afrika Mashariki na kuona kuwa balaa hili haliendelei kuwasumbua Watanzania?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa kama ifuatavyo.

Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iko makini kuhakikisha kwamba hakuna ujanja wa aina yoyote kwa sasa kwa watu kujipenyeza kununua ardhi kinyume cha Sheria na wale watakaobainika hatua kali zitachukuliwa na hata kunyang'anywa ardhi hiyo waliyoipata kinyume na taratibu za kisheria. Kwa hiyo, ndiyo maana hata suala la vitambulisho kuwa ni hati rasmi ya kusafiria hatukubaliani nayo kwa sababu inaweza kusababisha watu kuingia kiholela na kukaa bila utaratibu mzuri. Hata suala la ukazi wa kudumu tumetilia mkazo sana kwenye mazungumzo ili kuhakikisha kwamba taratibu zote hizi zinalinda vizuri ardhi yetu na watu wasipate kujipenyeza. Kwa hiyo, hatua mbalimbali zinachukuliwa kuhakikisha kwamba usalama wa ardhi ya Watanzania upo na unamilikiwa na Watanzania wenyewe na moja kubwa ni hili la kuhakikisha kwamba tunafanya land use plan ardhi yote iweze kumilikishwa na wananchi wa Tanzania na yatengwe maeneo mbalimbali kwa shughuli mbalimbali.

Kwa hiyo, uhakika ni huo kwa kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba ardhi itaendelea kulindwa.

**NAIBU SPIKA:** Tuko nyuma ya maswali, sasa tunaendelea na swali linalofuata. Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe, karibu!

Na. 20

**Utekelezaji wa Itifaki ya Umoja wa Forodha wa Afrika Mashariki**

**MHE. HARRISON G. MWAKYEMBE** aliuliza:-

Kwa kuwa utekelezaji mzuri wa Itifaki ya Umoja wa Forodha wa Afrika Mashiriki ndio msingi wa ufanisi wa soko la pamoja la Jumuiya hiyo:-

Je, ni kiasi gani Itifaki hiyo imetekelezwa kwa ufanisi hivyo kuwa na msingi imara wa uundwaji wa soko la pamoja?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, Mbunge wa Kyela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa utekelezaji mzuri wa Itifaki ya Umoja wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ndiyo msingi wa ufanisi wa Soko la Pamoja na ndio maana Wizara imeendelea kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Itifaki ya Umoja wa Forodha na mafanikio yamepatikana katika maeneo yafuatayo:-

(i) Kuondoa ushuru wa Forodha miongoni mwa nchi wanachama (*Internal Tariff Elimination*); Chini ya mpango huu bidhaa zinazoingia katika soko la Kenya kutoka Tanzania na Uganda hazitozwi ushuru wowote tangu mwaka 2005.

Bidhaa za kundi B kutoka Kenya zinapoingia Tanzania na Uganda zinatozwa ushuru ambao umekuwa ukipingua mwaka hadi mwaka na ifikapo mwaka 2010 utakuwa umefika kiwango cha sifuri. Hii ina maana kwamba nchi hizi tatu anzilishi zinatarajia kuwa ifikapo mwaka 2010 ushuru wa bidhaa kati yao utakuwa umeondolewa kabisa.

(ii) Nchi wanachama zimefanikiwa kuwa na Sheria moja ya ushuru wa forodha. Pia zimefanikiwa kuhuisha taratibu na nyaraka za kiforodha zinazotumika mipakani.

(iii) Kuweka wigo wa pamoja wa ushuru wa forodha kwa bidhaa zitokazo nje ya Jumuiya *(Common External Tariff).* Bidhaa zinazoagizwa kutoka nje ya Jumuiya naq kuingia katika soko la Afrika Mashariki zinatozwa viwango vya kodi vinavyofanana.

Bidhaa hizo zimewekewa viwango vitatu ambavyo ni asilimia sifuri kwa malighafi na bidhaa za uzalishaji *(capital goods);* asilimia kumi kwa bidhaa za kati *intermediate goods* na asilimia 25 kwa bidhaa zilizokamilika kabisa *(finished goods).*

(iv) Kuundwa kwa Kamati za kitaifa za kudhibiti, kusimamia na kuondoa vikwazo visivyo vya kiforodha. *Eliminationa for Non Tariff Barriers* zilizoundwa mwaka 2007 na nchi wananchama. Kamati zinazosimamia na kuratibu uondoaji wa vikwazo vya kibiashara.

(v) Nchi wanachama zimekubaliana kuondoa vikwazo visivyo vya kiforodha. Vikwazo hivyo ni pamoja na urasimu katika usimamizi wa masuala ya forodha, taratibu ngumu za ukaguzi wa ubora na viwango vya bidhaa, vizuizi visivyo vya lazima barabarani, mlolongo wa vyombo vinavyosimamia masuala ya forodha yanayofanana na taratibu ngumu za usajili na kupata leseni.

(vi) Mheshimiwa Naibu Naibu, aidha, fomu maalum zimeandaliwa zinazowezesha kubaini vikwazo katika shughuli za kibiashara. Fomu hizo zinapatikana Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Chama cha Shirikisho la Wenye Viwanda *(CTI),* Mamlaka ya Mapato *(TRA),* Vituo vya forodha vya mipakani na katika tovuti ya Wizara ya Afrika Mashariki. *www.meac.go.tz.*

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya mafanikio niliyoyataja mkataba wa kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki unatutaka tuendelee na mazungumzo ya soko la pamoja ikiwa ni hatua ya pili ya mtangamano wa Afrika Mashariki.

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja tu la nyongeza.

Kwa kuwa, Mheshimiwa Waziri ameorodhesha faida za ujumla kwa Afrika Mashariki nzima. Je, Serikali haioni umuhimu kufanya tathmini ya kina kujua Tanzania kama nchi imelegalega wapi, imefaidika vipi na kwa kiasi gani na utaratibu huu wa Umoja wa Forodha kulinganisha na wenzetu wa Kenya na Uganda kabla ya kujitosa kuingia hatua ya pili ya soko la pamoja?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwakyembe kama ifuatavyo:-

Kwanza nakubaliana naye sana Mheshimiwa Mwakyembe kwamba upo umuhimu wa kufanya tathmini ya kina ili tujue wapi tumefaidika na wapi tumeathirika. Mimi nilitaka nimhakikishie kwamba *study* hiyo imeanza na mwishoni mwa mwezi huu wa Aprili, 2009 itakuwa imekamilika na tutajua kwa kina wapi tumeathirika na wapi tumefaidika.

Hata hivyo, pia ipo *study* inayofanywa ndani ya Jumuiya nzima ya Afrika Mashariki kuona hilohilo kwa sababu wote watakaoathirika watakuwa na haki kwa mujibu wa Mkataba kuonyesha kuathirika kwao ili maathiriko hayo yatatuliwe kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa.

Na. 21

**Uharibufu Unaotokana na Kukatika kwa Umeme bila Taarifa**

**MHE. DR. OMAR MZERU NIBUKA** aliuliza:-

Kwa kuwa, mara nyingi umeme umekuwa ukikatika mara kwa mara tena bila taarifa kutoka *TANESCO* ili wananchi wazime vyombo vyao vya umeme na kupelekea kuungua kwa vyombo hivyo.

(a) Je, Serikali haioni kuwa, huu ni uzembe wa watendaji wa *TANESCO* ambao husababisha hasara kubwa?

(b) Je, Serikali inawachukulia hatua gani Watendaji hawa?

(c) Je, Serikali ipo tayari kutoa fidia kwa wananchi wanaopata hasara kutokana na hali hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Omar Mzeru Nibuka, Mbunge wa Morogoro Mjini, napenda kutoa maelezo yafuatayo:

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la kukatika umeme mara kwa mara linatambuliwa na Serikali. Miongoni mwa maelekezo yaliyotolewa na Serikali kwa *TANESCO* ni kuhakikisha kuwa matukio ya kukatika umeme yanapungua kama si kuisha kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukatika kwa umeme kunatokana na sababu zinazoweza kugawanywa kwenye makundi makuu mawili. Moja ni umeme unazimwa ili kufanya matengenzo, kuingiza kifaa kipya kwenye mfumo wa umeme au kuondoa kifaa kisichohitajika na kuunganisha njia mpya ya umeme.

Kundi la pili ni la hitilafu. Ni katika kundi hilindipo malalamiko ya kutokutoa taarifa yanajitokeza. Hitilafu katika mfumo wa umeme zipo za aina nyingine, kwa uchache nitazitaja zile kubwa. Moja ni kuzidiwa mzigo wa mfumo wa umeme kutokana na upungufu uliojitokeza kwenye uzaalishaji, ya pili ni hitilafu inayotokea kutoka na uchakavu wa kifaa au vifaa vinavyopitisha umeme, tatu ni matukio ya binadamu kama madereva, wakata miti, weziwa vifaa vya umeme na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kundi la kwanza ambapo umeme unazimwa makusudi ili kutekeleza wajibu fulani *TANESCO* inatoa taarifa kwenye vyombo vya haari mapema ikiwafahamisha matarajio ya muda na maeneo yatakayoathirika. Inawezekana kuwa njia hii si rahisi kuwafikia watumiaji wote wa umeme, lakini hii ndiyo njia muafaka kuliko njia zote ambazo zingeweza kutumika.

Katika kundi la pili ambapo umeme unakatika kutokana na hitilafu, si rahisi kutoa taarifa kwa mtuamiaji kabla ili aweze kuzima vyombo vyake vya umeme. Hitilafu ni jambo lisilotegemewa. Hakuna anayeweza kutambua kuwa baada ya muda fulani gari litagonga nguzo, waya utaibiwa, mafuta ya transfoma yataibwa au kifaa kitaharibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama taasisi yoyote ile *TANESCO* ina taratibu za kushguhulikia uzembe wa watedaji. *TANESCO* inatumia kanuni na mwenendo wa maadili (*Code of Ethics and Conduct*) kuwawajibisha Watendaji wazembe.

Katika kanuni hizi kuna kanuni ya uwajibikaji, majukumu, uwazi na ukweli. Mfanyakazi asiyezingatia au anayetenda kinyjma na kanuni hizi uongozi huchukua jukumu la kumwajibisha kulingana na kosa alilolifanya. Aidha, ikibainika kwua kuna uzembe wa utekelezaji na kusababisha hasara, kwa taratibu za Shirika wajibu wa kulipia fidia ni wa Shirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TANESCO* haina sheria ya fidia ila ina kitengo kinachoshughulikia malalamiko. Kitengo hiki hupitia malalamiko mbalimbali yanayoletowa na jamii wakiaminikuwa utendaji wa *TANESCO* umewaathiri. Mapendekezo ya kitengo hiki hupelekwa kwenye Kamati ya Uongozi kwa ajili ya kuyatolea maamuzi. Aidha, jamii inaweza kutumia *EWURA* kama mdhibiti kutoa malalamiko yake na kufuata Sheria ya *EWURA* maamuzi yake yana nguvu ya Kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo hapo juu napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Omar Mzeru Nibuka, Mbunge wa Morogoro Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Kwa mujibu wa ushahidi ulivyokuwepo, kukatika kwa umeme hakutokani na uzembe bali hutokana na hitilafu zisizotarajiwa au kuzimwa kwa njia za umeme kwa ajili ya matengenezo ambapo taarifa hutolewa mapema.

(b) Kwa kuwa, kukatika kwa umeme hakutokani na uzembe, hakuna hatua yoyote inayochukuliwa dhidi ya watendaji, kwa kosa la kusababisha kukatika kwa umeme.

(c) Kama nilivyosema kwenye maelezo aliyotangulia, fidia hutolewa iwapo itathibika kuwa hasara iliyopatikana inatokana na hitilafu katika mfumo wa usambazi umeme, iliyosababishwa na aidha makusudi au uzembe wa wafanyakazi wa *TANESCO* kwa mujibu wa kanuni na taratibu zilizowekwa na Shirika.

**MHE. DR. OMARI MZERU NIBUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri, lakini hata hivyo nina maswali mawili ya nyongeza.

La kwanza kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba mara nyingine kumekuwa kunatokea dharura lakini utakuta mara nyingi umeme huu ulikuwa ukiwashwa na kuzimwa, kuwashwa na kuzimwa katika muda mfupi sana kitu ambacho inaonekana ni suala la makusudi kwa Watendaji wa *TANESCO*.

Je, hawaoni kwamba huo ni uzembe?

La pili, ni kwamba yeye anasema kwamba *TANESCO* mara nyingi huwa wanawawajibisha wafanyakazi ambao wanaonekana kwamba ni wazembe.

Je, anaweza kuniambia mpaka sasa hivi ni wafanyakazi wangapi wa *TANESCO* ambao wameshawajibishwa kwa ajili ya uzembe katika kazi zao?

**NAIBU SPIKA:** Naomba swali hilo la pili Mheshimiwa Naibu Waziri asijibu yaani awajue ni wangapi?

Mheshimiwa waziri jibu kwa kifupi lakini maana jibu lilikuwa refu. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Omari Mzeru Nibuka, swali la nyongeza kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ile washa zima, washa zima anayosema Mheshimiwa Dr. Mzeru ndiyo sehemu hiyo tunayosema kwamba inatokana kusema kweli na matatizo yaliyopo kwenye mitambo wakati mwingine kunakuwa na matatizo ya *short* na kadhalika.

Kwa muda huo ambao unawashwa unazimwa, unawashwa na kuzimwa katika utafiti uliofanywa imeonekana siyo kwamba unawashwa na kuzimwa kwa makusudi ya wafanyakazi, hapana! Isipokuwa ni ule utaratibu wenyewe tu wa miundombinu ambao unatupelekea kwenye hali hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Serikali imetoa miongozo thabiti kabisa na kwamba tunawaomba *TANESCO* wajitahidi kwa kadri inavyowezekana kushughulikia matatizo haya hasa pale yanapohusiana na miundombinu na ikizingatiwa kwamba bajeti yake japo ni ndogo ya 15% ya kila mwaka inakwenda kwa makusudi kabisa kushughulikia matatizo yanayohusiana na matatizo ya miundombinu. (*Makofi*)

Na. 22

**Kupeleka Umeme Kilimatinde**

**MHE. DIANA M. CHILOLO** aliuliza:-

Kwa kuwa, Makao Makuu ya Tarafa ya Kilimatinde yana wakazi wengi pamoja na hospitali, shule za Sekondari mbili na Chuo cha Ufundi, na kwa kuwa, Mji huo hauna umeme na kwamba Serikali kupitia Bajeti ya mwaka 2008/2009 iliahidi kupeleka umeme kupitia Mfuko wa Umeme Vijijini; na ofisi ya *TANESCO* Mkoa ilionyesha kuwa inawezekana kuvuta umeme kutoka Manyoni Mjini:-

(a) Je, Serikali inasema nini juu ya kupeleka umeme Kilimatinde kutoka Manyoni Mjini?

(b) Je, ni lini kazi ya kupeleka umeme Kilimatinde itaaanza maana hadi sasa ni kimya wakati kelele za wananchi zinazidi sana?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Diana Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, baada ya kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa Makao Makuu ya Tarafa ya Kilimatinde yana wakazi wengi. Mji una hospitali, shule za sekondari mbili na chuo cha ufundi. Serikali pia inatambua wananchi wa eneo hili ni wakulima wazuri wa zao la alizeti na wafugaji wa ng'ombe na mifugo mingine.

Aidha, kwa kuwa umeme ni chachu kubwa ya maendeleo katiak shughuli zote hizi, ni imani ya Serikali kuwa wawekezaji watapatikana kwa ajili ya viwanda na biashara kwa ujumla. Pia umeme huo unatarajiwa kutumika kuendesha pampu za kusukuma maji ukizingatia kuwa Kilimatinde na maeneo yaliyo jirani yana msimu mmoja wa mvua.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kama alivyoomba kufahamu kwenye swali lake, mpango uliopo baada ya kufanyiwa tathmini yakinifu ni kutoa umeme kutoka Mji wa Manyoni wenye umeme wa *Grid* uliopo umbali wa Kilomita 85 kwenda Solya, Kilimatinde, Chibumagwa, Chikuyu na kuishia Kintiku.

Kwa kuzingatia haya na pia kwa kuzingatia ukweli wa ukubwa wa miradi hii, mipango ya mradi huu umetulazimu tutafakari kwa kina utekelezaji wenye ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ukweli huu, Wakala wa Nishati Vijijini (REA) umeidhinisha jumla ya shilingi milioni 700 ili mradi uweze kuanza. Gharama za kupeleka umeme kutoka Manyoni kupitia Kilimatinde mpaka Kintiku, unakadiriwa kuwa shilingi bilioni 4,253,590,000.00. Mradi utahusisha ujenzi wa laini ya KV 33 yenye urefu wa kilomita 85, vituo vya kusambaza umeme 7, na ujenzi wa laini ndogo zenye kilomita 12.

Mradi huu unatarajiwa hufanywe kwenye awamu ya tatu. Awamu ya kwanza itakuwa ni uandaaji wa mradi mpaka upimaji wa njia ya umeme, na mradi huo unatarajiwa pia kuweza kukidhi mahitaji ya kilomita 7 za KV33 na kwa maana hiyo umeme utafika mpaka kijiji cha Mhelela. Pindi fedha zikipatikana mradi utaendelea kutekelezwa kulingana na kiasi cha fedha kilichopatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo basi, baada ya maelezo hayo, napenda kutoa maelezo kama ifuatavyo:-

(a) Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)* katika bajeti yake ya mwaka 2008/2009 imetenga kiasi cha shilingi milioni 700 kwa ajili ya utekelezaji wa awali wa mradi huu;

(b) Kazi ya kupeleka umeme Kilimatinde imepangwa kuanza mwezi Oktoba, 2009. Mpaka sasa *TANESCO* imekwikamilisha zabuni za kuwapata wakandarasi wa ujenzi wa mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ninamuomba Mheshimiwa Mbunge, viongozi na wananchi wa Kilimatinde na Manyoni kwa ujumla tufanye subira wakati Serikali inafanya kila juhudi ili mradi huu upate kutekelezwa mapema. Aidha, pamoja na hayo Serikali inafanya kazi na mwekezaji (*Wind East Africa*) ili kubaini uwezekano wa kuongeza upatikanaji wa nishati ya umeme katika maeneo hayo kwa kutumia nishati mbadala itokanayo na upepo, ambao umebainika inawezekana kuwa ni rasilimali kubwa ya chanzo cha umeme.

**MHE. DIANA M. CHILOLO**: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Majibu haya mimi yamenichanganya. Nina uhakika hata Mbunge wa Jimbo anayongonyea hapo alipo na hata wananchi wanaonisikiliza wamechanganyikiwa.

La kwanza, kwa kuwa, Mheshimiwa Naibu Waziri, amesema fedha alizonazo ni za kupeleka umeme kwa umbali wa kilomita 7 tu kwa maana mpaka kwenye Kijiji cha Mhelela; na kwa kuwa kupitia swali langu kwenye Kikao cha Bajeti cha mwaka jana Mheshimiwa Waziri mwenyewe aliniahidi na wananchi wakasikia kwamba atapeleka umeme Kilimatinde ambapo kuna umbali wa kilomita 24 tu kwa mwaka wa fedha 2008/2009, leo hii Mheshimiwa Naibu Waziri anatoa mlolongo mrefu wa awamu tatu, awamu ambazo hata muda maalumu hazina. Je, atawambia nini wananchi wa Kilimatinde wanaotegemea kuupata umeme kwa Bajeti hii inayoishia tarehe 30 Juni, 2009?

La pili, kwa kuwa, hata maeneo yenye umeme wananchi wengi wameshindwa kuingiza umeme majumbani mwao kutokana na gharama kubwa za uingizaji umeme. Je, Serikali haioni kwamba kuna kila sababu kupunguza za uvutaji umeme kwenye nyumba za wananchi ili sehemu nyingine atoe mwenye nyumba na gharama nyingine ilipie Serikali ili wananchi wengi waweze kuvuta umeme tuondoke kwenye asilimia 10 ambayo ndiyo hao tu wanaotumia umeme Tanzania? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri naomba ujibu kwa kifupi sana jibu lilikuwa refu, swali limekuwa refu basi kila kitu ni kirefu. Naomba ujibu kwa kirefu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namwomba radhi kama majibu yangu yamemchanganya. Lakini nilichosema ni kwamba mradi wote kupeleka umeme Kilimatinde umejumuishwa kwenye mradi mkuu

unaotoa umeme kutoka Manyoni kwenda mpaka Kintiku kwa umbali wa kilomita 85. Hapo katikati umeme huo utatoka Manyoni utaifikia Kilimatinde ambapo ni kilomita 28.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zilizotengwa mwaka huu mradi huo wote jumla ni bilioni 4.2, lakini fedha zilizotengwa mwaka huu kwa sababu ya sababu maalum za upatikanaji wa fedha kama anavyofahamu Mheshimiwa Mbunge ni milioni 700. Milioni 700 hizo zitaanza uandaaji wa mradi, upimaji na kadhalika na baada ya mambo hayo pia wataanza kuunganisha kwa kilomita 7.

Sasa kwa kadri ya upatikanaji wa fedha utaendelee mradi huo hadi kufikia Kilimatinde na kuendelea hadi mpaka kwenye maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ndiyo hali halisi ya kifedha iliyopo. Kwa hiyo, utekelezaji huo tumetoa ahadi kwamba tutaufanya kwenye awamu ili upate kuanza kupata mwelekeo wa utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la gharama kubwa za kuunganisha umeme tumewahi kulizungumzia humu Bungeni. Ni kweli kwamba vifaa vya kuunganishia umeme hapo katika mwaka mmoja uliopita vimepanda bei sana. Lakini tumeiomba *TANESCO* iangalie uwezekano waweze watu kuunganisha umeme kwa kulipa kidogo kidogo au kwa kukopa. Hata hivyo, tunaamini kwamba wanalifanyia kazi kwa kuangalia pia hali halisi ya kifedha ya Shirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ni jambo ambalo tumelielekeza *TANESCO* lifanyiwe kazi kuangalia kama wananchi wanaweza kufanyia utaratibu wa kuunganisha umeme kwa kulipa kidogo kidogo.

**NAIBU SPIKA:** Swali lilikuwa la Kilimatinde, wote mliosimama mnatoka Kilimatinde. Tunaendelea na Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Mheshimiwa Ruth Msafiri atauliza swali.

Na. 23

**Tatizo la Maji – Muleba Kaskazini**

**MHE. RUTH B. MSAFIRI** aliuliza:-

Kwa kuwa, tatizo la maji limezidi kuwa kubwa baada ya kukosekana kwa vyanzo vya uhakika katika Kata za Muhutwe, Izigo na Kagoma katika Jimbo la Muleba Kaskazini licha ya Kata hizo kupakana na Ziwa Victoria na Mto Ngono:-

Je, Serikali haiwezi kutumia chanzo kimajawapo kutengeneza mpango mkubwa wa maji kwa wananchi hao?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ruth Blasio Msafiri, Mbunge wa Muleba Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba katika Kata za Muhutwe, Izigo na Kagoma vyanzo vya maji vya uhakika ni Ziwa Victoria na Mto Ngono. Kama tunavyojua, Serikali inaendelea kutekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji katika Halmashauri zote nchini.

Katika utekelezaji wa Programu hii, Halmashauri ya Wilaya ya Muleba inaendelea na mchakato wa kumwajiri Mtaalam Mshauri, atakayeshirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Muleba na wananchi kuhakiki vyanzo vya maji na kusanifu miradi ya maji katika vijiji kumi ambavyo ni Katoke, Iroba, Kiragi na Muyenje katika Jimbo la Muleba Kaskazini, vijiji vingine ni Katembe, Kishoju, Kangaza, Kyota, Kabale na Karutanga.

Tayari Halmashauri ya Wilaya ya Muleaba imewasilisha Wizarani rasimu ya mkataba wa Mtaalam Mhsauri. Wizara yangu inafanya mapitio ya rasimu hiyo na hatua itakayofuata ni kuwasilisha mapendekezo Benki ya Dunia ili itoe ridhaa kwa Halmashauri kusaini mkataba na Mtaalam Mshauri aliyependekezwa.

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa mwaka 2009/2010, Halmashauri ya Wilaya tayari kwa kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji imetenga shilingi milioni 87 kwa ajili ya kujenga mradi wa maji utakaohudumia Kijiji cha Izigo.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake aliyotupatia. Pamoja na kuishukuru Serikali kwamba imekwishatenga milioni 87 kwa ajili ya mradi wa maji katika kijiji cha Izigo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, naomba niseme kwamba kutenga fedha kidogo kidogo kwa Serikali katika miradi hii ya vijiji na Halmashauri za Wilaya kunasababisha miradi ile isikamilike na mwisho inaisha ama inatelekezwa kwa sababu inakuja kuwa na gharama kubwa.

Napenda kuiomba Serikali kwamba iongeze kiasi cha shilingi milioni 87 ilizokwishakutenga ili fedha hizo ziweze kushirikiana na *Community Solution for African Development* ambao ni *NGO* iliyokwishagundua vyanzo mbili vya maji katika Kata ya Izigo ambayo ni sehemu ya Jimbo la Muleba Kaskazini ili fedha hizo ziweze sasa kusambaza maji katika maeneo yote ambayo nimeyataja.

La pili, nilipouliza swali hili nilikusudia nipate majibu ni kwa nini Serikali imeshindwa kutumia chanzo cha maji ya uhakika cha Ziwa Victoria ambacho ndicho tulichopakanacho. Mimi Jimbo langu sehemu kubwa inapakana na Ziwa Victoria.

Lakini kuna mto mkubwa unaozunguka Mkoa mzima wa Kagera ikiwa ni pamoja na Jimbo langu na unaitwa Mto Ngono. Ni kwa nini maeneo haya yenye maji ya

kudumu na hayakauki tunashindwa kumaliza tatizo la maji katika Jimbo la Muleba Kaskazini? Ndiyo hasa lilikuwa swali langu. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba ujibu kwa kifupi sana muda umetupita.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru kwa taarifa hiyo kwamba kuna *NGO* ambayo inajitahidi kusaidiana na Serikali kutatua matatizo ya maji. Kazi yetu sisi ni kuangalia pale ambapo juhudi za watu wengine napo zipo na Serikali nayo ina-*compliment initiative* kama hizo. Kwa hiyo, ninakubaliana naye kwamba Serikali ipo tayari kabisa kushirikiana na *NGO* hiyo kuangalia namna ya kutatua matatizo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niongeze tu kwamba tulipoamua kutenga fedha kidogo kidogo hasa kupitia utaratibu wa *Quick Wins* ilikuwa kwamba wakati tunasubiri programu hii ndefu ambayo tunaitekeleza chini ya *Water Sector* na hususan *World Bank* basi tuwe na kitu kinaendelea ndilo lilikuwa lengo la Serikali na mahali pengi imezaa matunda mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu chanzo cha Lake Victoria na Mto Ngono kuwa chanzo kizuri, mimi ninakubaliana na Mheshimiwa Ruth Msafiri.

Lakini napenda nimhakikishie na nimweleze kiutaalam kwamba Ziwa Victoria na Mto Ngono vyote vyanzo hivi vipo chini vinahitaji kupampu maji kwenda juu ambako ndiko wananchi waliopo na mahali pengi vinahitaji *double pumping* yaani kuwa na *pump* mbili na zaidi kwa ajili ya kupeleka maji. Halafu na maji na hasa ya Ziwa yanahitaji kutibu kwa sababu ni maji machafu kwa kiasi fulani. Kwa hiyo, tunataka angalau vyanzo hivi tuviingize katika programu kubwa hii ili haya matatizo makubwa tuweze kuyashughulikia kikamilifu.

Na. 24

**Juhudi za Kufanikisha Kilimo cha Umwagiliaji Maji**

**MHE. JUMA SAID OMAR** aliuliza:-

Kwa kuwa kilimo ni uti wa mgongo wa Taifa na kwa kuwa, maji ni uhai:-

Je, ni ushirikiano gani uliopo baina ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na Wizara ya Maji na Umwagiliaji katika kufanikisha kilimo cha umwagiliaji maji na hivyo kuleta tija zaidi kwa wananchi na Taifa?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma Said Omar, Mbunge wa Mtambwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 12 Februari, 2008, Mheshimiwa Rais alifanya mabadilio katika Baraza la Mawaziri. Katika mabadiliko hayo Mheshimiwa Rais alihamisha majukumu ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji kutoka katika Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na kuyaweka katika Wizara mpya ya maji na umwagiliaji.

Lengo kubwa la mabadiliko hayo ni kutoa mgawanyo mzuri wa kazi ambapo Wizara ya Maji na Umwagiliaji inashughulikia kazi za ufundi zinazohusu ugawaji wa maji na uendeshaji wa miundombinu ya umwagiliaji maji mashambani kama mabanio makubwa ya mito, mifereji mikuu, visima virefu, mabwawa na miundombinu nyingine.

Jukumu kubwa la Wizara ya Kilimo ni kusimamia uzalishaji wa mazao na huduma za ugani ikiwa ni pamoja na maandalizi ya pembejeo kama mbolea, mbegu bora, viuatilifu na zana za kilimo. Utaratibu wa kutenganisha majukumu ya uendeshaji wa miundombinu na uzalishaji mazao unatumika kwa mfanikio katika nchi kadhaa duniani kama vile India, Bangladesh, Kenya, Malawi, Ethiopia, Sudani na Misri.

Katika mazingira ya sasa yanayoashiria kuendelea kupungua kwa rasilimali maji na upungufu wa chakula duniani iko haja kubwa kuongeza tija siyo tu katika kuzalisha chakula bali pia katika matumizi bora ya maji (*water productivity*). Lengo hili litafikiwa kwa ushirikiano wa sekta zote mbili kwa kuwa zote zinamhudumia mkulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, upo ushirikiano baina ya Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika na Wizara ya Maji na Umwagiliaji katika kufanikisha umwagiliaji maji mashambani na uzalishaji wa mazao. Kwa mfano, katika kupanga mipango ya kuendeleza umwagiliaji, wataalam wa umwagiliaji wanashirikiana na wataalam wa kilimo ili kuweka miundombinu ya umwagiliaji inayokidhi mahitaji ya mimea na kuacha kiasi kingine cha maji kutumika kwa matumizi mengine kwa ajili ya binadamu, mifugo na kulinda mazingira.

Utaratibu huu umedhihirika katika skimu za umwagiliaji kama vile skimu ya Mkula katika Wilaya ya Kilombero ambapo miundombinu iliboreshwa na hatimaye mpango wa stakabadhi za pembejeo ukaanzishwa katika skimu hiyo. Matokeo yake ni kwamba katika msimu wa 2007/2008 uzalishaji wa zao la mpunga uliongezeka kutoka tani 3 hekta hadi wastani wa tani 7.5 hekta.

Changamoto iliyopo katika matokeo haya ni kwamba mbegu bora na mbolea zikielekezwa katika skimu za umwagiliaji kuna uwezekano mkubwa wa kuongeza uzalishaji wa mazao. Wizara yangu itashirikiana na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kulisimamia jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hizi mbili katika kutekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (*ASDP*) zimekuwa zikipanga kwa pamoja maeneo ya kuendeleza umwagiliaji. Katika kufikia uamuzi wa skimu zinazostahili kupewa fedha za nyongeza kupitia Mfuko wa Kuendeleza Umwagiliaji, ngazi ya Wilaya, *(DIDF),* Wizara hizi zimekuwa zikifanya tathmini kwa pamoja.

Tathmini hizi zimekuwa zikifanywa kwa kushirikiana na Wizara nyingine za Sekta za Kilimo *(Agricultural Sector Land Ministries)* ambazo ni TAMISEMI, Wizara ya Maendeleo ya Uvuvi na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mwingine wa ushirikiano ni kwamba katika mwaka 2008/2009 Wizara hizi mbili ziliandaa na kupeleka kwa pamoja maombi ya fedha za nyongeza zilizoombwa na Serikali kutoka Benki ya Dunia ili kukabiliana na tatizo la upungufu wa chakula. Fedha hizi zitawekwa kwenye Mfuko wa Pamoja wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo *(ASDP Basket Fund)* ambapo zitatumika kama Bajeti ya nyongeza kugharamia uboreshaji wa miundombinu ya umwagiliaji kupitia Mfuko wa Kuendeleza Umwagiliaji Ngazi ya Wilaya (*DIDF*) kwa kipindi cha kuanzia 2009/2010 hadi 2011/2012.

**MHE. JUMA SAID OMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kilimo cha umwagiliaji ndiyo mkombozi wa Mtanzania na kwa kuwa inaonyesha kuna ushirikiano wa Wizara mbili hizi ikihusisha watalaam. Je, ni lini sasa Tanzania tutaweza kujitosheleza kwa chakula ili kupata ziada ya kuuza nje ya nchi na hivyo kumkomboa mkulima pamoja na kuongeza pato la taifa? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Swali dogo lakini kubwa lakini ujibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, labda kifupi niseme kwamba tunayo malengo ya kujitosheleza kwa chakula. Hivi sasa ukitazama chakula ambacho tunazalisha na hususan mchele unaweza ukafikiri kwamba tumekwishajitosheleza kwa sababu tunazalisha takribani tani laki saba na kitu zaidi ya yale mahitaji.

Lakini ile ziada ni ndogo mno ukilinganisha na upungufu uliopo kwenye nafaka zingine hasa mahindi. Kwa hiyo, bado iko kazi kubwa ya kuhakikisha kwamba kupitia kilimo cha umwagiliaji basi zao kama la mpunga nalo tunalipa nafasi kubwa.

Labda nikitaka kujibu swali kwa urahisi ni kwamba tunatarajia tutakapofikisha hekta laki nne, zote zikilimwa kwa kumwagiliwa mara mbili, mara tatu kwa mwaka basi Tanzania itakuwa imejitosheleza hususan kwa zao kama hilo la mpunga. Hivi sasa tunalima tu hekta 289 ndiyo maana tunafanya juhudi kwa Wizara hizi mbili angalau tufikie hekta hizo laki nne zinazolimwa kwa ufasaha.

Na. 25

**Mahakama Kutengewa Fedha za Kutosha**

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA** aliuliza:-

Kwa kuwa, ili Mahakama ziweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu zinahitaji kutengewa fedha za kutosha za kujiendesha kulingana na mahitaji yake:-

(a) Je, Serikali inatekeleza kwa kiasi gani suala hili?

(b) Je, kwa mwaka 2008 kesi ngapi hazikusikilizwa kutokana na ukosefu wa fedha nchini na kupelekea kuongezeka kwa msongamano wa Mahabusu?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mbunge wa Micheweni, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kwamba ili Mahakama ziweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu zinahitaji fedha za kutosha za kujiendesha kulingana na mahitaji na kwa kuzingatia ukweli huu Serikali imekuwa ikiitengea Mahakama fedha za kuendesha shughuli zake ingawaje sio kwa kiwango cha kutosha sana, hii inatokana na ufinyu wa mapato ya Serikali kugharamia shughuli zote za Serikali kwa wakati mmoja. Hata hivyo Serikali iko tayari siku zote kuongeza Bajeti ya matumizi kwa Mahakama kadri uchumi wake utakavyokuwa unaimarika.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, msongamano wa mahabusu magerezani husababishwa na mambo mengi na sababu mojawapo ikiwa ni ukosefu wa watumishi wa kutosha katika kukamilisha upelelezi wa kesi kwa haraka, upungufu wa fedha kuhakikisha mashahidi wanaitwa Mahakamani kwa wakati.

Upungufu wa fedha kutekeleza majukumu haya husababisha Mahakama kupunguza vikao vyake kwa ajili ya kuamua kesi mbalimbali. Na kutokana na upungufu huu wa fedha Mahakama ilishindwa kusikiliza kesi za Jinai 907 na kesi za madai 531 hadi kufikia tarehe 31 Disemba, 2008. Takwimu hizi ni kwa Mahakama za Rufaa pekee.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kuwa mahakama zetu hazitengewi fedha za kutosha ili kutekeleza majukumu yake na kwa kuwa jukumu kubwa la mahakama ni kutoa haki na kwa wakati.

(a) Sasa je, Serikali haioni kwamba kutokuitengea fedha za kutosha Mahakama kunaisababishia kutokulitekeleza jukumu lake hili muhimu?

(b)Kwa kuwa kesi 907 za jinai na kesi 531 za madai mpaka kufikia tarehe 31 Desemba, 2008 zilikuwa hazijaendeshwa kutokana na ukosefu wa fedha na hizi ni kwa mahakama ya rufaa. Je, kesi hizi kutoendeshwa hatuoni kwamba hatuwatendei haki wananchi wetu na kuwa suala la kutokuwa na fedha wao haliwahusu? (*Makofi*)

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana kwa kuijali mahakama na kuiheshimu kama anavyoiheshimu kwamba ni chombo ambacho kinapaswa kuwatendea haki wananchi kwa ujumla. Kwa kweli hiyo ndio kazi yake na tunataka tutoe haki kwa wananchi kwa wakati sasa ukosefu wa fedha unaikumba Serikali yote kunalikumba Bunge hili ndiyo maana hata wakati mwingine vikao vinapunguzwa. Umuhimu wa mahakama tunaujua lakini pia tunavyo vyombo vingine ambavyo vina umuhimu vile vile kweli tunaifanya mahakama isitekeleze jukumu lake. Lakini kama nilivyosema tunajitahidi sana kadri inavyowezekana kuipatia mahakama Bajeti ambayo inaweza kuiendesha kwa kiasi fulani. Ni kweli pia wananchi kwa kesi zao kutokusikilizwa kwa kiasi fulani wanakosa haki.

Lakini sasa ili mahakama zijiendeshe lazima ziwe na fedha na ili fedha zipatikane inabidi uchumi wetu ukue ili tuweze kukidhi kiasi hicho. Kwa hiyo, wananchi itabidi nao wavumilie katika hili maana hakuna ujanja mwingine wowote wa kufanya hatuwezi kuendesha mahakama bila fedha. Kuendesha mahakama kwa kweli tunahitaji pia mahakama zikae peke yake zinahitaji mawakili wa Serikali nao waweze kwenda pale na hawa nao watumishi wa Serikali na wanahitaji fedha.

Kwa hiyo, Bajeti tu ndiyo tatizo letu. Lakini kama nilivyosema kadri uchumi wetu utakavyozidi kukua tutahakikisha kwamba mahakama inapata fedha za kuweza kutoa haki kwa wananchi. (*Makofi*)

Na. 26

**Utaratibu wa Kuendeleza Vizazi kwa Viumbe wa Majini**

**MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN** aliuliza:-

Kwa kuwa, wanyamapori hupewa fursa ya kuzaliana kati ya mwezi Januari na Juni, ambapo huwa ni marufuku kufanya shughuli za uwindaji katika kipindi hicho ili kusaidia kuendeleza kuwepo kwa wanyama hao kwa faida ya vizazi vijavyo:-

(a)Je, kuna utaratibu wowote unaosaidia kuendeleza kuwepo kwa viumbe vyote vilishivyo majini ikiwa ni pamoja na samaki?

(b)Je, Serikali inaelewa kuwa, kiasi kikubwa cha samaki aina ya Jodari wanavuliwa kwa wingi kwenye Bahari ya Hindi kwa kutumia uvuvi haramu?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Parmukh Sing Hoogan, Mbunge wa Kikwajuni, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali inao utaratibu unaosaidia kuendeleza kuwepo kwa viumbe vyote viishivyo kwenye maji wakiwemo samaki. Utaratibu huo ni pamoja na kufunga maeneo ya uvuvi *(Closed Area)* na vipindi vya uvuvi *(Closed Seasons).* Lengo la utaratibu huu ni kutoa nafasi kwa viumbe waishio kwenye maji kuzaliana na kukua kabla uvuvi

haujaanza tena ili uvuvi huo uweze kuwa endelevu na usioharibu kizazi cha viumbe hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya Mwaka 2003 na Kanuni zake za mwaka 2005, maeneo ya uvuvi wa samaki aina ya kamba hufungwa kwa kipindi cha miezi mitatu kuanzia tarehe 30 Novemba, hadi 29 Februari, kila mwaka. Vile vile, maeneo ya mazalio ya samaki yanalindwa na Sheria Na. 29 ya mwaka 1994 iliyoanzisha Hifadhi ya Bahari ya Maeneo Tengefu *(Marine Parks* na *Reserves Act).* Aidha, uvuvi kwenye maeneo ya maingilio ya mito kwenye maziwa yamepigwa marufuku kutumika kwa ajili ya uvuvi. Lengo la utaratibu huu ni kuhakikisha kuwa maeneo muhimu na tete *(Critical Habitats)* ya uvuvi yanalindwa na kutunzwa ili viumbe hao waendelee kuwepo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua tatizo la uvuvi haramu katika maeneo ya uvuvi nchini ikiwemo Bahari ya Hindi ambapo samaki aina ya Jodari huvuliwa. Serikali inaendelea kupambana na uvuvi huo ambao sio endelevu kwa kuchukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na doria za anga na majini za kukabiliana na uhalifu huo.

Aidha, Serikali ilikwishafanyia marekebisho sheria ya Mamlaka ya Uvuvi katika Bahari Kuu *(Deep Sea Fishing Authority)* Na. 17 ya mwaka 2007 na kukamilisha kanuni zake za mwaka 2009 ili ziweze kutumika kikamilifu katika kupambana na auvuvi haramu.

**MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza kuchukua fursa hii kuipongeza Wizara hii kwa kazi nzuri waliyofanya hivi karibuni kukamata meli ya kigeni na hivyo kesi hiyo ndiyo inashughulikiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Samaki wale walikuwa tani ngapi na watauzwa lini? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba tarehe 8 Machi, 2009 doria iliyokuwa inafanywa na meli ambayo tulikuwa tunashirikiana na Kenya, Afrika Kusini na *Mozambique* tuliweza kukamata meli aina ya *Tawarik* ambayo ilikuwa na mabaharia kutoka Philippine, Vietnam, China na Kenya, mle tuliweza kupata tani 293 za samaki ambazo thamani yake tunakisia kwamba ni shilingi bilioni 2.7.

Samaki hawa waliondolewa kwenye meli hiyo na wamehifadhiwa katika *cold storage* ya bahari *food company*. Kwa sasa hivi samaki hao tumekwenda mahakamani na mahakama ninayo furaha kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba mahakama imeamuru samaki hao wapigwe mnada.

Sasa kufuatana na hali ya utaratibu namna ya kuhakikisha kwamba samaki hawa Wizara imetangaza *tender* tunatafuta kampuni itakayopiga mnada huo na fedha itakayopatikana yote tutapeleka *Hazina* kwa upande wa Serikali. Sasa atakayeshinda

watapata hizo hela. Wale wakishindwa sisi tutachukua hizo hela sasa hivi tunatarajia kupata bilioni 2.7 kesi inaendelea mahakamani siwezi kueleza zaidi. (*Makofi*)

Na. 27

**Mpango wa Kuwanufaisha Wafugaji**

**MHE. MARTHA J. UMBULLA** aliuliza:-

Kwa kuwa bei ya bidhaa mbalimbali hupanda kulingana na gharama za uzalishaji kuwa juu; na kwa kuwa wafugaji wanafuga kwa gharama kubwa hasa wakati wa ukame wakihamahama kutafuta maji na malisho lakini mifugo yao hukonda na kuuzwa kwa bei ya chini:-

Je, Serikali ina mpango gani wa makusudi wa kuwanufaisha wafugaji kuhusiana na changamoto hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya mikakati inayotekelezwa na Wizara ni pamoja na kutenga maeneo kwa ajili ya ufugaji. Hadi sasa Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Halmashauri mbalimbali, zimetenga maeneo yenye jumla ya hekta 1,391,109.4 kwa ajili ya wafugaji katika mikoa 13, wilaya 31 na vijiji 240.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inaendelea kuyaimarisha mashamba ya kuzalisha mbegu za malisho ya mifugo. Awali mashamba mawili ya Langwira (Mbeya) na Vikuge (Pwani), ndiyo yaliyotumika kuzalisha mbegu za malisho. Hivi sasa uzalishaji wa malisho unafanyika pia katika mashamba ya Mabuki (Mwanza), Sao Hill (Iringa), Kituo cha Utafiti wa Mifugo Tanga, Kituo cha Biashara Mifugo Kizota (Dodoma) na Kituo cha Utafiti wa Malisho Kongwa (Dodoma). Katika mwaka 2007/08 jumla ya tani 42 zimezalishwa na kusambazwa kwa wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inashirikiana na wadau kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya *(DADPs)*, kujenga miundombinu ya maji, ambapo tangu 2001/02 jumla ya malambo 852 yamejengwa, 32 yamekarabatiwa pamoja na visima virefu 13 katika Wilaya 65. Majosho mapya 182 yamejengwa na 605 yamekarabatiwa. Pia jumla ya lita 193,433 za dawa za kuogesha mifugo za ruzuku zenye thamani ya shilingi bilioni 4.1 zimesambazwa kwa wafugaji. Mwaka huu wa fedha 2008/09, Serikali itatumia shilingi bilioni 11.4 kwa ajili ya ruzuku ya kununulia dawa ya kuogesha mifugo.

Serikali pia imetoa chanjo kwa ajili ya kudhibiti ugonjwa wa homa ya mapafu, ambapo katika mwaka 2007/08 dozi milioni 3.2 za chanjo zilinunuliwa kwa ajili ya kukinga ugonjwa huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inahimiza usambazaji wa huduma za uhimilishaji ili ziwafikie wafugaji na kuhimiza matumizi ya mbegu bora. Ili kuongeza uzalishaji wa mbegu bora zinazosambazwa kwa wafugaji, Kituo cha NAIC – Arusha kimeendelea kuimarishwa kwa kununua madume kumi kutoka Afrika ya Kusini na kufikisha idadi ya madume 34 kwa sasa ili kiweze kuzalisha dozi 100,000 kwa mwaka badala ya dozi 65,000 zilizozalishwa mwaka 2007/08. Lengo ni kufikisha madume bora 68.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Wizara imeanzisha vituo vya uhimilishaji vya Kanda vikiwemo vya Mbeya (Nyanda za Juu Kusini), Mwanza (Kanda ya Ziwa), ambavyo vimekwishaanzishwa; vituo vya Kibaha (Kanda ya Mashariki) na Dodoma (Kanda ya Kati) vitaanzishwa mwaka 2008/09. Lengo ni kuwa na vituo vitano hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, wafugaji wanahamasishwa kunenepesha mifugo yao. Hivi sasa unenepeshaji unafanywa na wafugaji katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa (Shinyanga, Mwanza na Mara) na katika ranchi za Ruvu, Mzeri, Kongwa, Manyara, ambapo takriban ng'ombe 56,000 hunenepeshwa kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwapatia wafugaji soko la uhakika, Wizara inaendelea kuhamasisha ujenzi wa viwanda vidogo, vya kati na vikubwa vya kusindika nyama na maziwa. Hadi sasa machinjio za *Tanzania Meat Company* (Dodoma), *Arusha Meat Company* (Arusha), *Tanzania Pride Meat* (Morogoro) na *Sumbawanga Agriculture and Animal Feeds Industries* – SAAFI (Rukwa), zenye uwezo wa kuchinja kila moja kati ya ng'ombe 150 – 200 kwa siku zimejengwa na zinafanya kazi.

Aidha, vipo Viwanda vya Maziwa vikubwa vitano na vya ngozi sita. Hali hii itaongeza ubora wa bidhaa na kuwapatia wafugaji bei nzuri kwa mifugo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu imetolewa kwa wafugaji 21,106 juu ya ufugaji bora na mafunzo ya stashahada kwa wanachuo 1,185, ambayo yamegharimiwa katika mwaka 2008/09. Aidha, vipindi vya redio 52 na televisheni 12 kuhusu ufugaji bora vimetayarishwa na kurushwa hewani. Lengo ni kutoa mafunzo ili kuwa na wagani 16,000 wanaotoa huduma za mifugo.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa semina, sasa namwita Mheshimiwa Umbulla. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza, nashukuru sana kwa majibu marefu na ya kina ya Mheshimiwa Naibu Waziri; pamoja na majibu hayo nina swali dogo tu la nyongeza.

Kwa kuwa nchi yetu ina mifugo mingi sana ikiwemo ng'ombe zaidi ya milioni 18, mbuzi, kondoo na kadhalika, kudhihirisha kwamba mifugo ni utajiri mkubwa sana wa nchi yetu. Je, Serikali itakubaliana nami kwamba sasa ni wakati muafaka kujenga viwanda vingi zaidi hasa maeneo ya wafugaji ili kuwapa wafugaji soko la uhakika zaidi ya viwanda alivyovitaja vya Dodoma, Arusha na Morogoro ili kukabiliana pia na changamoto niliyouliza ya ukame?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa sasa hivi ipo katika harakati za kuhakikisha kwamba, viwanda vinajengwa ili wananchi waweze kuuza mifugo yao na kujipatia faida.

Mfano, wiki chache zilizopita tulikuwa Botswana ambapo tulikwenda kuangalia namna wanavyoendeleza viwanda vya nyama na sasa hivi tunao mpango wa kujenga kiwanda, tumeshatangaza kujenga Kiwanda cha Nyama kule Ruvu. Tunazo shilingi bilioni tatu na kiwanda hicho kinatarajiwa kuanza kujengwa hivi karibuni. Tunataka kufufua Kiwanda cha Mbeya ambacho kilijengwa lakini kilikuwa hakijamalizika na tunatafuta mwekezaji. Vilevile Shinyanga tuna mwekezaji amejitokeza na tunatarajia kuhakikisha kwamba, kiwanda hicho kinajengwa. Vilevile Arusha nilikuwa natembelea huko, kile kiwanda tumekuwa tukikiangalia kama kinaweza kukidhi mahitaji ya viwanda vya kusindika nyama kwa upande wa Mkoa wa Kaskazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yetu ina nia thabiti kabisa, kuhakikisha kwamba wafugaji wananufaika kwa mifugo yao.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Naomba nitumie muda wa dakika tano ili swali la Mheshimiwa Charles Mlingwa, linalohusiana na suala la ardhi ambalo Waziri aliahidi kwamba litajibiwa sasa lijibiwe.

Na. 28

**Serikali Kutoa Hatimiliki za Maeneo ya Makazi**

**MHE. DKT. CHARLES O. MLINGWA** aliuliza:-

Kwa kuwa mwaka 1974/75 Serikali iliwahamisha wananchi nchini kutoka kwenye makazi ya asili na kuwapeleka kwenye vijiji vya maendeleo, ambapo kila kaya ilipimiwa eneo la makazi la ekari moja:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha mpango wa kuwapatia hati miliki za maeneo ya makazi yao?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa DKT. Charles Ogesa Mlingwa, Mbunge wa Shinyanga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya ardhi waliyopewa wananchi wakati wa uanzishaji wa vijiji vya ujamaa 1974/75, yalitolewa kwa mujibu wa Sheria ya wakati huo,

iliyokuwa inaitwa *Land Tenure (Village Settlements*) Na. 27 ya mwaka 1995, ambayo kwa sasa imefutwa wakati wa kupitishwa kwa Sheria ya Ardhi Na. 4 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 za mwaka 1999. Chini ya Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5, suala la wanavijiji kumilikishwa ardhi wanayoitumia limezingatiwa. Kwa mujibu wa Sheria hiyo, ardhi ya kijiji sharti mipaka yake ipimwe na kutoa vyeti vya Ardhi ya Vijiji (*Village Land Certificates).* Pia sheria inahitaji kijiji kifanyiwe mpango wa matumizi bora ya ardhi, kuwekewa mipaka ya maeneo ya makazi na mashamba ya wanavijiji na hatimaye zitolewe Hatimiliki za Kimila (*Customary Right of Occupancy*) kwa wanavijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu kazi za upimaji wa vijiji ianze kutekelezwa chini ya Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995, jumla ya vijiji 9,300 vimepimwa na kuwekewa mipaka, kati ya vijiji vipatavyo 11,000 vilivyosajiliwa hapa nchini hii ni asilimia 85. Lengo ni kupima na kuweka mipaka ya vijiji vyote ifikapo mwaka 2010. Kazi ya kutoa vyeti vya ardhi ya vijiji, kupanga matumizi bora ya ardhi, kupima maeneo ya makazi na mashamba ya wananchi, kujenga masjala za ardhi na utayarishaji na utoaji wa hatimiliki za kimila, imeanza kutekelezwa na Serikali kulingana na upatikanaji wa fedha.

Kazi hii inafanywa na Halmashauri za Wilaya, kwa kushirikiana na Wizara yangu na ilianza mwaka 2004/2005. Tangu mwaka 2004 hadi Desemba, 2008 jumla ya Hatimiliki za Kimila 16,967 zimetolewa kwa wananchi katika Wilaya 15 Tanzania Bara. Wilaya hizo ni Newala, Mbinga, Ileje, Rungwe, Kilombero, Njombe, Mbozi, Handeni, Iringa, Monduli, Ukerewe, Kisarawe, Mbulu, Hanang, Babati na Arumeru.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia utaalamu uliopatikana kutoka kwenye Wilaya zilizotekeleza miradi ya mfano, tunategemea Halmashauri za Wilaya nyingine zitaiga na kuongeza kasi ya utoaji wa vyeti vya ardhi ya vijiji, upimaji wa makazi na mashamba, upangaji wa matumizi ya ardhi, ujenzi wa masjala za ardhi katika ngazi ya Wilaya na Vijiji na vilevile utoaji wa hatimiliki za kimila.

**MHE. DKT. CHARLES O. MLINGWA**: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza, namshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa majibu sahihi na mazuri kwa swali langu; nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa Jimbo la Shinyanga Mjini ndio Manispaa ya Shinyanga na hivyo matumizi ya ardhi hiyo kustahili kusimamiwa kwa mujibu wa Sheria Na. 4; ni lini basi Wananchi wa Shinyanga watapimiwa maeneo yao wanayoishi leo ili waweze kuyamiliki kwa mujibu wa sheria hiyo Na. 4?

Pili, kwa kuwa Manispaa nyingi na Majiji mengi nchini kwetu yana maeneo holela katika makazi ya watu; ni lini basi Serikali itaondoa tatizo la makazi holela kwenye Manispaa na Majiji yetu ili Watanzania waishi kwa utaratibu ulio bora zaidi kuliko hivi sasa? (*Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la kwanza, kazi ya Manispaa zote nchini na

Halmashauri za Miji ya kupima viwanja na kugawia wananchi viwanja ni ya kudumu, maana anasema itaanza lini; inaendelea na itaendelea. Tatizo ambalo Wizara yangu naliona na tunashirikiana na wenzetu wa Wizara ya TAMISEMI ni kwamba, Manispaa na Halmashauri za Miji hawatengi fedha kila mwaka za kutosha kupima viwanja na kuwagawia wananchi.

Pili, baadhi yao wana upungufu wa hao wapima wataalamu wa ardhi, lakini hawaoni umuhimu wa kuajiri wataalamu ili waongeze kasi ya kupima. Halmashauri nyingi zikiwa na upungufu wa Madaktari au Walimu zinapiga kelele kweli kweli. Wanapokuwa na upungufu wa wapima ardhi, wataalamu wa Mipango Miji hawapigi kelele, hawaajiri wanaomba. Haya mawili yakifanyika, wakitenga fedha za kutosha kupima viwanja, wakiajiri wataalamu wa kupima kasi itaongezeka na Wizara yangu ipo tayari kushirikiana nao. *(Makofi)*

La pili, kuhusu ujenzi holela mijini ni kwamba, sasa hivi tunao mpango kwanza wa kutambua wale ambao wamejenga nyumba zao holela. Mpango wa MKURABITA huzirasimisha ili nyumba zile walau zitambuliwe na sheria walau hata wasihudumiwe kupata mikopo. Tumeanzisha utaratibu wa kuzitambua na kuwapa leseni za makazi, ilikuwa ya miaka miwili, Bunge lililopita limeongeza mpaka miaka mitano, ile leseni ya makazi anaweza akaitumia kupata mikopo. Hiyo ni hatua ya kwanza kuwasaidia wale waliojenga holela.

Vilevile kuna mpango wa kuboresha hayo maeneo sasa kwa kuyawekea miundombinu, barabara, mifereji ya maji machafu na kadhalika. Mpango huu umeshaanza katika Jiji la Dar es Salaam; mwaka huu vilevile utakwenda Mwanza na baadaye tungependa usambae katika miji mikubwa yote nchini.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Swali la Mheshimiwa Martha Mlata ni la 16; hata ukijitahidi kwa nguvu zote, huwezi kumaliza maswali chini ya 15 na hili lilikuwa la 16. Wapangaji wameweka la 16, msiwape matumaini Waheshimiwa Wabunge kwamba watafikiwa, kumbe swali limezidi yale yanayostahili kujibiwa kwa siku; kwa hiyo kesho litakuwa la kwanza.

Waheshimiwa Wabunge, kwanza kabisa, naomba niwatambulishe wageni. Tunao wageni wa Mheshimiwa Lucy Nkya, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ambao ni Uongozi wa Shirika Linalohudumia Watu Wenye Ulemavu wa Ngozi *(Albino).* Naomba wote wasimame walipo ili tuwaone. Ahsante, karibuni sana tunawatakia kazi njema. *(Makofi)*

Tuna wageni wa Mheshimiwa Luckson Mwanjale, ambao ni Mheshimiwa Margareth Mwanjale, mke wake; yuko wapi? Naona kama wapo. Mchungaji Patrick Nyanga na mke wake Jane Wangui. Ahsante sana. Yupo Mchungaji Iteru Grayson, yupo Ndugu Gilbert wa Murango Transport Limited na yupo Ndugu Kigundu Isaya. Hawa ni wageni wa Mheshimiwa Mwanjale, Mbunge wa Mbeya Vijijini.

Vilevile wapo Viongozi wa Chama cha Wanafunzi wanaosomea Sayansi ya Siasa katika Chuo Kikuu cha Dodoma. Naomba wote wasimame kama wapo. Karibuni sana tunawatakia kheri na mtunze majengo yetu yale, kwa sababu ndio *symbol* ya kazi nzuri, tunawatakia kheri. Tunao wanafunzi 20 kutoka Saint John's University Dodoma, wapo hapa hapo, naona hawapo labda kesho. Ahsanteni sana.

Waheshimiwa Wabunge, matangazo ya vikao; Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba, leo tarehe 22 kutakuwa na Kikao cha Kamati hiyo saa tano asubuhi na ajenda ya kikao hicho ni kujadili Muswada wa Bima na kitafanyika katika Ukumbi wa Pius Msekwa, maana yake na wengine wanakaribishwa pia.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Wilson Masilingi, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo saa 5.00 asubuhi kutakuwa na kikao chumba Na. 231, ghorofa ya pili, Jengo la Utawala. Anaomba Wajumbe wa Kamati hiyo wahudhurie.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma, Mheshimiwa Zitto Kabwe, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo hii saa 5.00 asubuhi kutakuwa na Kikao cha Kamati hiyo katika Ukumbi Na. 219, ghorofa ya pili, Jengo la Utawala. Hawa ni 219 na wale wengine 231.

Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati ya Sheria, anaomba niwaarifu Wajumbe kuwa, kutakuwa na Kikao cha Kamati ya Kanuni za Bunge, tarehe 22 Aprili, 2009. Anasema, Katibu wa Bunge anaomba Kamati ya Kanuni za Bunge ikutane leo tarehe 22 kushughulikia rufaa ya Mheshimiwa Dkt. Willibrod Slaa, Mbunge, dhidi ya uamuzi wa Spika wa tarehe 11 Februari, 2009 baada ya Mheshimiwa Spika kuelekeza kuwa suala hilo lishughulikiwe na Kamati hiyo.

Kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 5(6), Toleo la 2007; Spika au Naibu Spika, hatakuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kanuni za Bunge inapokaa kujadili uamuzi unaolalamikiwa. Kwa sababu hiyo, tunaomba uwatangazie Wajumbe wa Kamati wakutane kushughulikia rufaa hiyo. Tunapendekeza kikao kifanyike Ukumbi Na. 219, ghorofa ya pili, Jengo la Utawala, saa saba. Wale wengine ni saa 5.00 asubuhi, Kamati ile ya Mashirika ya Umma; sasa sijui mtapishana huko huko kama saa zitakuwa zimeingiliana? Naomba kuwasilisha.

Kwa kuwa ile rufaa inakatwa dhidi ya Spika, bila shaka hicho kikao itabidi Mwenyekiti niwe mimi kwa mujibu wa kanuni na ndiyo maana kitafanyika saa 7.00 mchana.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

**Muswada wa Sheria ya Bima wa Mwaka 2009**

***(The Insurance Bill, 2009*)**

*(Muswada uliotajwa hapo juu Ulisomwa Bungeni*
*Mara ya Kwanza)*

**(Muswada wa Sheria ya Vinasaba vya Binadamu wa Mwaka 2009**
***(The Human DNA Bill, 2009)***

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. MERYCE M. EMMANUEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami pia naomba nitumie wasaa huu mfupi, kutoa pongezi kwa Wizara ya Afya, Katibu wa Wizara na Watendaji kwa ujumla, kwa kuuleta Muswada huu kwa muda muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wapo watu wanaozaliwa na jinsia mbili; na kwa kuwa kipimo hiki husaidia sana kuelewa mtu huyu ni jinsia ipi zaidi ni vyema ila nashauri kuwa baada ya kuelewa kuwa mtu huyu ni jinsia ke au me, apewe elimu ya kupokea kile kilichopatikana katika majibu yale na kutiwa moyo, kwani wakati mwingine anaweza kudhani yeye ni mwanaume kumbe ni mwanamke na inabidi ajichanganye zaidi na jinsia yake. Vilevile wakati mwingine kubadili hata mavazi si jambo rahisi, linahitaji kujengwa na kupewa faraja ya kile kilichopatikana katika kipimo hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipimo hiki cha *DNA* kimekuwa kikitumika hata katika mambo ya mahakama zaidi katika mambo ya mada kesi. Ni ukweli kuwa kipimo hiki hubaini ukweli wa mtu aliyehusika kwa hakika na kumrahisishia hakimu au jaji kuhukumu kwa haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo linalojitokeza katika eneo hili ni kule kucheleweshwa majibu; ni kweli kwamba, Ofisi ya Mkemia Mkuu, huchukua zaidi ya miaka hata sita na zaidi, hii pia inaweza kutoa mwanya wa rushwa, badala ya ukweli wa kipimo hicho ukawa siyo ukweli. Naishauri Wizara ifuatilie kwa karibu zaidi, nini zaidi hupelekea kucheleweshwa majibu kwa muda mrefu huo. Vilevile wakati mwingine mshtakiwa hunyimwa haki yake ya msingi ya kupata hukumu yake kwa wakati unaotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hii ni nzuri sana, ila kwa kukaa na kipimo hicho muda mrefu ni dhahiri kuwa kipimo hicho hakiwezi kuaminika sana kwa yule anayesubiri majibu yale. Vivyo hivyo hata kipimo cha kutambua mtoto huyu baba yake nani, pia ukweli unapungua zaidi baada ya kuchukua muda mrefu.

Naomba Wizara iangalie upya muda wa kutoa majibu angalau isichukue muda mrefu sana ili kipimo hicho kiaminike. Lakini pia nigeshauri Wizara iongeze vituo vya kuchukua kipimo hiki, jambo ambalo linasababisha msongamano mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kutamka kuwa, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii kuhusu Muswada huu.

Muswada huu umeletwa mbele ya Bunge lako Tukufu ukiwa umechelewa sana kuletwa; hivyo, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalam wa Wizara yake, kwa kazi nzuri ya kuandaa Muswada huu ili nchi yetu iweze kwenda sambamba na mabadiliko yanayotokea katika Sekta ya Afya katika matumizi ya teknolojia mbalimbali; hii ni pamoja na teknolojia ya *DNA* ya Binadamu katika maeneo ya kinga na tiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa ushauri/mapendekezo kwa ajili ya kuuboresha Muswada kama ifuatavyo:-

Sehemu ya tatu ya Muswada kuhusu kuanzishwa kwa maabara kwa ajili ya *DNA* ya Binadamu ndani ya maabdra ya Mkemia Mkuu wa Serikali. Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali itahitaji fedha za kutosha, wataalamu, vifaa vya maabara na majengo ya kutosha kwa ajili ya kuanzisha maabara ya *DNA*; hivyo, nashauri maandalizi ya kina yafanyike kwa lengo la kuhakikisha kuwa fedha za kutosha, vifaa, wataalamu na nafasi ya kutosha yote yanazingatiwa.

Kuhusu mafunzo; Serikali ihakikishe kuwa, mafunzo ya wataalamu yanafanyika ndani na nje ya nchi ili kupata wataalamu wa kutosha kwa ajili ya kuanzisha maabara.

Sehemu ya nne ya Muswada inahusu kukusanya na kuchunguza sampuli za *DNA* za Binadamu. Ninashauri kazi hii ifanywe kwa uangalifu, tukizingatia kuwa nchi yetu ni kubwa; ili kufanikisha zoezi la ukusanyaji, uchunguzi, usafirishaji na utunzaji wa sampuli ni vyema Wizara iangalie uwezekano wa kuwa na maabara ya *DNA* ya Binadamu kikanda kama ilivyo MSD. Lengo ni kupeleka huduma karibu na wananchi na kupunguza kero ya ucheleweshaji wa matokeo ya maabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia tena kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalamu wa Wizara yake kwa kukamilisha Muswada. Naomba kurudia tena kuunga mkono hoja.

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wote walioshiriki katika kuandaa Muswada wa Sheria hii.

Kwanza kabisa, naipongeza serikali kwa kuleta Muswada wa kutunga Sheria ya Kusimamia na Kudhibiti Matumizi ya Teknolojia ya *DNA* ya Binadamu. Sheria hii ni muhimu sana kwa nchi yetu, nasema ilichelewa kuletwa. Kutungwa kwa sheria hii kutainua wigo wa watu kupata haki zao.

Nchi yetu ina matatizo ya baadhi ya watu hasa polisi kuwabambikizia kesi watu wasio na hatia. Vitendo hivi husababisha wasio na hatia kufungwa au hata kuamuliwa kunyongwa bila kosa, kwani ushahidi unaotolewa ni hafifu. Hivyo, teknolojia hii itasaidia kuwakamata wahalifu wenyewe na kuwaepusha wasio na kosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kupanga uzazi, watu wengi wangependa wazae watoto wachache watakaoweza kuwamudu. Watu wengi wangependa kuzaa watoto wa jinsia zote; hivyo, teknolojia hii itawasaidia wazazi kupanga wazae watoto wangapi na wa jinsia ipi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kihistoria, jamii nyingi za Kitanzania wanathamini sana watoto. Wengi wanatamani kuzaa watoto lakini wapo wanaowapa wasichana mimba na kuwakataa. Matokeo yake, hawa wasichana wanadhalilika na kuchukua jukumu la kulea peke yao. Teknolojia hii itawatambua hawa wanaowapa wasichana mimba za utotoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri alisema sheria hii ikipita itabidi sheria nyingine zirekebishwe. Ningependa kujua ni kwa namna gani sheria hii itagusa Sheria ya Ndoa?

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kujua kama hospitali za kupima vinasaba hivi zitakuwa kote nchini, ili kurahisisha kazi hii ifanywe kwa usahihi au kituo kitaendelea kuwa Muhimbili tu?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga mkono hoja.

**MHE. CHARLES N. MWERA:** Ninamshukuru Mheshimiwa Profesa Mwakyusa, kwa Muswada huu. Kwanza kabisa, Muswada huu umechelewa sana. Umuhimu wa Muswada wa *Human DNA* utasaidia sana kutatua matatizo mengi ambayo si ya lazima; kwa mfano, kwenye kesi mbalimbali ambazo zinahitaji ushahidi wa vinasaba vya binadamu kama kupata uhalali wa mtoto kama kuna utata kwa wanandoa.

Nashauri pawepo na maabara za kutosha kwa nchi nzima hasa Wilayani ili wananchi waweze kupata huduma muhimu. Maabara hizo ziwe za kutoa majibu sahihi, ambazo hazitaingiwa na rushwa. Ni vyema hizo maabara za serikali na binafsi zikaguliwe mara kwa mara.

Wananchi washirikishwe na wapate taarifa juu ya umuhimu wa maabara ya vinasaba vya binadamu ili waweze kupata huduma hii muhimu.

## KAMATI YA BUNGE ZIMA

**(Muswada wa Sheria ya Vinasaba vya Binadamu wa Mwaka 2009**
***(The Human DNA Bill, 2009)***

Ibara ya 1

Ibara ya 2

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 3

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge pamoja na mabadiliko yake)*

**MHE. DKT. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 2.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo tunarudi nyuma?

**MHE. DKT. TARAB ALI:** Ina maana hukuniona Mheshimiwa Mwenyekiti?

**MWENYEKITI:** Sikukuona, hukusimama bwana?

**MHE. DKT. ALI TARAB ALI:** Nilisimama lakini hukuniona.

**MWENYEKITI:** Haya nakupa nafasi.

**MHE. DKT. ALI TARAB ALI:** Ahsante. Tumesema kwamba, sheria hii ihusishe sio Tanzania Bara peke yake, lakini ihusishe vile vile na Tanzania Visiwani.

Kumekuwa na *argument* ya kwamba, Muswada huu ni wa Sheria wa Wizara ya Afya, kwa hiyo, Wizara ya Afya si chombo cha Muungano, lakini kuna mifano mingine tele; labda nitoe mfano wa Wizara ya Mawasiliano ambayo si ya Muungano lakini kuna mambo ya *Air Traffic* mle, ambao sehemu zote mbili za Muungano zinahusika. Kwa hiyo, hapa tunaongelea mambo ya *DNA* ambayo kama Mheshimiwa Waziri alivyosema, inahusisha faida nyingi tu; kutambua wahanga wa majanga, kutambua wahamiaji haramu, kutambua wahalifu wa makosa ya jinai, ambao unahusu pande mbili za Muungano; kwa nini basi Muswada huu usihusishwe pande zote mbili za Muungano? Ahsante sana.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Jambo hili ni kweli lilijitokeza jana na nifafanue tu tulichokisema jana; ni kwamba, huu Muswada umeletwa hapa Bungeni na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, ambayo si Wizara ya Muungano. Mfano uliotoa wa *Air Traffic,* nina imani kwamba, Baraza la Wawakilishi liliridhia hiyo. Sisi tuna uhusiano wa karibu sana na Wizara ya Afya ya Zanzibar na masuala kama haya tunayajadili na hapo watakapoona kwamba ni muhimu na wao wawe na sheria kama hii, itapitishwa katika Baraza la Wawakilishi.

Sasa hivi tuna Maabara yetu ya Mkemia Mkuu, ambayo wanaitumia bila matatizo. Kwa hiyo, kwa shughuli zinazoendelea pale wataweza kutumia; hapa tunazungumzia

habari za *DNA* sio masuala ya uhalifu ambayo yapo chini ya Polisi. Ina maana kwamba, Polisi wanaweza wakatumia; wawe wa upande huu au wa upande wa pili wa Muungano.

**MWENYEKITI:** Nadhani Mheshimiwa Mbunge, alitaka maelezo tu akitaka mabadiliko utaratibu ni mrefu, sio tu wa hiki lakini sheria zile zinazogusa pande zote mbili sharti Mabaraza haya mawili yakae pamoja na hili halikutokea; kwa hiyo nadhani maelezo ndiyo hayo.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

**MHE. DKT. ALI TARAB ALI:** Ya 3 naona …

Ibara ya 4

**MHE. DKT. ALI TARAB ALI:** Tumetoka ya 2 tumekwenda ya 4?

**MWENYEKITI:** Nimerudi nyuma kwa ajili yako.

**MHE. DKT. ALI TARAB ALI:** Tulikuwa tunaongea ya 2.

**MWENYEKITI:** Tulirudi nyuma kwa sababu ya kukusikiliza.

**MHE. DKT. ALI TARAB ALI:** Kwa hiyo, sasa tupo ibara ya 3.
**MWENYEKITI:** Ibara ya 4

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 5

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu kutazama ibara hii ya 5 pamoja na yale marekebisho kwenye lile jedwali lakini kuna vitu viwili ambavyo nilikuwa ninataka tuelewane na Mheshimiwa Waziri.

Katika ibara hiyo ya 5 yale mambo yaliyoorodheshwa pale (a) mpaka (k), nadhani yanakosa neno moja pale la kuunganishwa, kwa sababu zile zote ni *noun.* Kwa hiyo, ukisema *the regulator shall perform the following functions: (a) maintain the register*. Nadhani ni *to maintain otherwise* tungetumia "*noun*" pale ya kusema *maintenance* au *maintained and so on.*

Halafu katika kifungu hicho hicho nilitaka tu hili hasa kwa Waandishi wa Sheria, nimepitia huu Muswada wote kwa makini sana, nimeona pale mbele hili neno "*functions*" kuna mstari pale mdogo. Kwa mujibu wa utungaji wa sheria na Kiingereza kinavyokuja, pale panatakiwa pawe *colon* na *colon* maana yake ni *punctuation* ambayo

inawekwa kuashiria kwamba kuna orodha.  Kwa hiyo, ningeomba hapo napo pafanyiwe marekebisho.

Kuna vifungu vingi ambavyo vimewekwa hako ka-mstari ambapo kwa mujibu wa lugha ya Kiingereza, sikukaona tafsiri yake mahali popote isipokuwa hako kanaweza kuwekwa kuunganisha maneno mawili.

Ningeomba hili lizingatiwe, kuna vifungu karibu vingi tu ambavyo nitampa yule Mwandishi wa Sheria ili aweze wakati wanaikamilisha aweke hizo *colon* badala ya kale ka-mstari ambako hakaendani na hali halisi ya kuandika hii Muswada.  Ahsante sana.

**MWENYEKITI:**  Naweka mbele ya Meza ya Spika, sio kwa Mwanasheria. Yuko wapi?

Anachokisema Mheshimiwa hapa; *the function*s pale haikuwekewa kale ka-dash, sio maana yake ni *semi* colon.  Halfu *from* (a) mpaka (k) lazima *to maintain, to make, to conduct, to monitor, to coordinate, to provide, to initiate, to foster, to advise and to carry*. Kwa hiyo kifungu hiki kinaafikiwa?

(*Ibara Iliyotajawa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 6

(*Ibara Iliyotajawa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 7

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 8
Ibara ya 9

*(Ibara zilizotajawa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 10

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 11

**MHE. DKT. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Hapa kwenye ibara ya 11 kuna *appointment* ya *inspectors from amongst officers from the Government Chemist Laboratory Agency* kwa mujibu wa marekebisho kutoka kwenye Taasisi za Umma, lakini hapakuandikwa *qualification* ya hawa *inspectors* wenyewe. Je, haiwezekani ikaja baadae tukaletewa *Officers* kutoka Masjala au mtu yeyote?

Lazima pawe na *qualification* za *inspectors* ambao wanatakiwa kufanya kazi hizi.

**MWENYEKITI:** Una maana *qualification* hizi ziwepo hapa?

**MHE. DKT. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sifa zao kitaaluma ziandikwe.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Mbunge apendekeze ni *qualifications* gani angependa tuwape hawa *inspectors*. Sisi tulidhani kwamba, ikiwa wazi namna hii kuna maeneo mengi tu hata *regulator* hatukuandika awe mtu wa namna gani, hapa tungeacha tu hekima itumike kwamba, tutenge watu ambao wana uwezo wa kufanya hiyo kazi na sioni kama ni lazima iwekwe kwenye sheria.

**MWENYEKITI:** Mimi nilifikiri utaliweka kwenye Kanuni?

**MHE. DKT. ALI TARAB ALI:** Ndiyo.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Umeliweka vizuri zaidi kuliko nilivyotaka kusema.

**MWENYEKITI:** Ndiyo, maana si hekima tu ikae kwenye Kanuni.

*(Ibara iliyotajawa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 12
Ibara ya 13

*(Ibara zilizotajawa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 14

*(Ibara iliyotajawa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 15

**MHE. DKT. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninataka ufafanuzi wa Mheshimiwa Waziri; hii *Human DNA Laboratory* itakuwa katika Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, lakini hakuna chombo au maafisa ambao wataangalia *quality standards* ya maabara hii.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili alilileta Mheshimiwa Dkt. Tarab jana, alikuwa anazungumzia habari za *checks and balances*. Nilivyojaribu kulijibu, nilisema hapa tungejiridhisha kwamba, kazi inakwenda vizuri kwa maana ya vifaa na uwezo wa wafanyakazi na kitu cha kuzungumzia ni *quality assurance, quality control* na *quality standard.*

Kwenye *schedule of amendment* yetu namba (M), ambayo inakuja kwenye *clause* namba 17 kama inavyosomwa kwenye marekebisho kipengele (c) anasema: "The laboratory has evidence that it is implementing quality assurance programmes." Nataka kuamini kwamba, hilo linajibu hoja yake.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 16

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 17

*(Ibara iliyotajawa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 18
Ibara ya 19
Ibara ya 20

*(Ibara zilizotajawa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 21

*(Ibara iliyotajawa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 22
Ibara ya 23

*(Ibara zilizotajawa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 24

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara ya 24; jana nilipokuwa nachangia niliomba maelezo kidogo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. Ibara ya 24 pale inaposema *samples for human DNA shall be collected by sampling officers;* nilikuwa nimesema kuhusiana na ku-*collect sample*, tukii-*limit* kwenye sheria kwamba ni kikundi hiki cha hawa watu tu ndiyo watakaoweza ku-*collect* hata *sample*; je, hatutakuwa tunaji-*narrow* kwa sababu nchi hii ni kubwa na watu ni wengi?

Mawazo yangu ni kwamba, *analysis* ingeweza kushughulikiwa na hawa maafisa lakini *collection* ya *samples* tusingeweza kuipanua kidogo?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *definition* ukurasa wa saba inasema; *sampling officer means an officer appointed and gazetted to collect sample for human DNA under section 14;* ikiwa na maana kwamba, tutaweka utaratibu ili kutoleta usumbufu kwa wananchi, lakini lazima tuwafahamu na tuwa-*gazette.*

*(Ibara zilizotajawa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 25

*(Ibara iliyotajawa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 26
Ibara ya 27

*(Ibara zilizotajawa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 28

**MHE. DKT. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka ufafanuzi na kujiridhisha kwenye kifungu kidogo cha 2(j) kwamba, badala ya neno *may* liwe neno *shall* kwa lugha ya kisheria.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanzoni mwa kifungu cha pili cha 28(2) kinasema *the rights and assurances of the sample source shall include the following information;* na ukija kwenye je, tumekibadilisha iko kwenye *schedule* yetu ya *amendment* inasomeka *genetic counseling services*. Kwa hiyo, suala la kusema *may be available* au *must be available* haliji, kwa sababu kifungu ambacho kinatawala hivi vyote hapo kinajitosheleza.

*(Ibara iliyotajawa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 29
Ibara ya 30

*(Ibara zilizotajawa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 31

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 32

*(Ibara iliyotajawa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 33

**MHE. DKT. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara hii inaongelea *transportation of samples*; lakini *transportation* hii ni ya ndani ya nchi tu, ambayo Muswada uko kimya kuhusu *transportation* ya *samples* nje ya nchi. Pawe na utaratibu au kifungu ambacho kinazungumzia kuhusu *material transfer agreement* na SOPs ambazo zina mwongozo ambazo zinaruhusu kusafirisha *DNA* kutoka nchini kwetu kwenda nchi nyingine.

**MWENYEKITI:** Wapi inakuonyesha ndani ya nchi tu?

**MHE. DKT. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki kinasema *the sampling officer shall cause the sample for human DNA to be transported to the laboratory through the means he may consider appropriate and safe;* hapa inakusudia *human DNA* ipo ndani ya maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba tufanye *amendment* iliyotokana na mazungumzo ya hapa jana. Tulitaka tuilete mbele ya Bunge Zima kwamba, kulikuwa na suala kwamba *transportation* inampa uamuzi yule *sampling officer how to transport.*

Sisi tulisema hapana, lazima kuwe na *appropriate and safe means* ambazo zitatambulika na zitawekwa kwenye Kanuni na tulitaka isomeke *the sampling officer shall cause the sample for human DNA to be transported to the laboratory through appropriate and safe means.*

Nikija kwenye suala la Mheshimiwa Tarab, hicho kipengele kipo lakini siwezi kukipata sasa hivi, kama tutaruhusiwa tunavyokwenda nikikipata nitaweza kukileta mbele. Lipo suala la kubadilishana hata *samples* na watu wa *Interpol* watataka *samples* za *DNA* kutoka kwetu. Utaratibu huu upo katika kifungu kimojawapo ambacho kwa haraka haraka siwezi kukiona.

**MWENYEKITI:** Uliomba isomeke vipi?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Tulikuwa tunaomba Bunge lisomeke *the sampling officer shall cause the sample for human DNA to be transported to the laboratory through appropriate and safe means.*

**MWENYEKITI:** Yale yote *he may consider appropriate and safe* tunayaondoa.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Yale yanaondoka.

**MWENYEKITI:** Unajua mimi nilipouliza kwani kifungu hiki kinasemaje kama kinazungumzia habari ya ndani. *The issue* hapa ni *appropriate and safe means.* Sasa ni ndani au nje; *this must be considered*. Kwa hiyo, iwe nje au ndani.

*(Ibara iliyotajawa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 34

*(Ibara iliyotajawa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 35
Ibara ya 36
Ibara ya 37

*(Ibara zilizotajawa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 38

**MHE. DKT. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara hii inasema kwamba, mtu yeyote ambaye anataka kwenda kufanya utafiti ambao una-*involve DNA* atafute kibali kutoka kwa *regulator*. Vilevile tunajua kwamba, kuna taasisi nyingine ambayo imeundwa kwa Sheria ya Bunge hili Tukufu ya *National Institute for Medical Research*, ambayo pia inahusika na *medical research*. Sasa hapa pawe na *fine cut line* ya kujua *research* zipi zipewe *authority* na *regulator* na zipi zipewe *authority* na *NIMR.*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uniruhusu nirudie niliyomjibu jana. Kwamba, kweli tuna *NIMR, Ifakara Centre* wote wanafanya *research.* Hapa tunazungumzia *DNA* na tukiacha kila mtu akajiamulia afanye nini, wapi na lini, itatupa shida; ndiyo maana tukasema *to centralize* kwa mtu ambaye anaweza aka-*coordinate* haya mambo na hata tukitaka kujua kama hili kweli liliruhusiwa tuwe na mahali pa kwenda; sio kila mahali panapofanyika *research* tuwaruhusu wafanye hivyo.

Kwa mfano, ukiwa unafanya *research* kwa binadamu kuna mambo ya *ethical clearance* na hii inaweza ikatolewa na mtu yeyote lakini tuliona afadhali *NIMR* wawe ndiyo *in-charge* ili kila mmoja asijifanyie uamuzi. Kwa hiyo, kitu kama hiki ambacho ni nyeti, tulidhani mahali ambapo ni *appropriate* ni kwa Mkemia Mkuu.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 39

*(Ibara iliyotajawa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 40

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 41

**MHE. DKT. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa *researcher* yeyote ambaye anataka ku-*collect sample* za *human* DNA ni lazima amtaarifu *District or Regional Administration.* Naona ingekuwa vyema hapa tukamhusisha DMO na RMO, kwa sababu wao ndiyo wataalam hasa ambao wana ujuzi wa kisayansi na *ethically* kuweza kujua hapa hayaendi sawa.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hao wote aliowataja wapo katika *District* na *Regional Administration.*

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, hao madaktari wapo kwenye *District and Regional Administration.* Halafu nzuri zaidi wanasema na *sample* ni ile iliyo-*contain* katika *permit* sio *any.*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 42
Ibara ya 43

Ibara ya 44

*(Ibara zilizotajawa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 45
Ibara ya 46

*(Ibara zilizotajawa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 47
Ibara ya 48

*(Ibara zilizotajawa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 49

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mazungumzo ya jana tulisema ibara ya 48(2) inazungumzia habari za watu ambao wataruhusiwa kuwepo wakati *sample* zinachukuliwa *from a competent person* na baada ya majadiliano tuliona *Community Officer* hapa anapwaya kidogo sio mahali pake, tulikuwa tunaomba kuanzia *or a Community Development Officer* ifutwe.

**MWENYEKITI:** Ifutwe *Community Development Officer* lakini yule *Social Welfare Officer* anabaki?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Ndiyo ibaki ni *relevant.*

*(Ibara zilizotajawa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 50
Ibara ya 51

*(Ibara zilizotajawa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 52

*(Ibara iliyotajawa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 53
Ibara ya 54

Ibara ya 55

*(Ibara zilizotajawa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 56

*(Ibara iliyotajawa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 57

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 58

*(Ibara iliyotajawa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 59

**MHE. DKT. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara ya 59 inaongezea kama Mheshimiwa alivyotuambia ni *database* ya taifa; ikiwa tumesema sample hizi zitachukuliwa kwa maana ya Tanzania Bara peke yake, nafikiri hii haitakuwa ni *database* ya taifa, itakuwa ni *database* ya Tanzania Bara.

*(Ibara iliyotajawa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hapa tunacheza na maneno tu; tuna Muhimbili National Hospital ambayo ina Wazanzibari wengi sana, hakuna aliyefukuzwa pale. Mimi naona ibaki kama *National Database*.

**MWENYEKITI:** Ndiyo maana sisi wenzako tukaona tuendelee, maana ndiyo hivyo; basi tunaendelea.

Ibara ya 60

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 61
Ibara ya 62

*(Ibara zilizotajawa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 63
Ibara ya 64

*(Ibara zilizotajawa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 65

*(Ibara iliyotajawa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 66

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 67

*(Ibara iliyotajawa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 68

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 69
Ibara ya 70
Ibara ya 71

*(Ibara zilizotajawa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 72
Ibara ya 73
Ibara ya 74

*(Ibara zilizotajawa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge*

*Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 75

*(Ibara iliyotajawa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Jedwali la 1

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Jedwali la 2

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia hoja hii, kwenye ibara ya 5 kulikuwa na ibara nyingine nyingi ambazo zilikuwa zinahusika na yale niliyoyasema kwenye ibara ya 5 na nadhani nimekuletea orodha. Kwa kuwa Kamati ya Bunge Zima ndiyo imemalizika, nilitaka nizitaje hizo ibara kwa sababu zilikuwa nyingi sana.

**MWENYEKITI:** Endelea.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nimetoa hoja kwamba, *colon* inahitajika pale kuonesha kwamba kuna orodha inayofuata. Kwa hiyo, nilisha-*move* marekebisho katika ibara ya 5. Sasa ningeomba ibara ya sita ziwekwe hizo *colon;* ibara ya 6(1), ibara ya 8(2), ibara ya 9(2), ibara ya 12(1), ibara ya 13(2), ibara ya 17(3), ibara ya 20, ibara ya 25(2), ibara ya 26(1), ibara ya 28(2), ibara ya 29(1), ibara ya 30(1), ibara ya 36, ibara ya 38(3), ibara ya 44(1), ibara ya 49(1), ibara ya 56(2), ibara ya 57, ibara ya 58(1), ibara ya 60, ibara ya 61, ibara ya 65, ibara ya 66, ibara ya 67(3), ibara ya 71(2) na *second schedule*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ume-*include* 65?

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Ameleta hayo mabadiliko kwa maandishi, pamoja na kwamba tulitaka yaingie kwenye Hansard kama yalivyo.

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Vinasaba vya Binadamu wa Mwaka 2009**
***(The Human DNA Regulation Act, 2009)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Bunge Zima imepitia Muswada wa Sheria uitwao *The Human DNA Regulation Act, 2008* pamoja na mabadiliko yake, kifungu kwa hadi kifungu na kuukubali. Hivyo basi, naomba kutoa hoja kwamba, Muswada huo sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa*
*Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunapenda kueleza kwamba, Muswada huu umepita ngazi zote zinazostahili na umeungwa mkono na sasa unabaki kupewa saini ya Mheshimiwa Rais ili iwe Sheria. Tunaendelea, Katibu shughuli inayofuata.

**Muswada wa Sheria ya Mbolea wa Mwaka 2008**
***(The Fertilizer Bill, 2008)***

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kutoa hoja kuhusu Muswada wa Sheria ya Mbolea wa Mwaka 2008, naomba kutumia fursa hii, kwa niaba ya Wananchi wa Bunda, kutoa salamu za pole na rambirambi kwa Wananchi wa Busanda, kufuatia kifo cha aliyekuwa Mbunge wa Busanda, Marehemu Faustine Rwilomba. Naomba Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi, amina.

Aidha, nampongeza Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa ruhusa yako, naomba kutoa hoja kwamba, Muswada wa Sheria ya Mbolea wa Mwaka 2008 *(The Fertilizer Bill, 2008)*, pamoja na Jedwali la Marekebisho *(Schedule of Amendment)*, usomwe kwa mwaka ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitumie fursa hiin kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Majin chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mbunge wa Ileje, kwa kuuchambua Muswada huu kwa kina na ushauri mzuri walioutoa.

Aidha, napenda kuwashukuru wadau wote, ambao kwa namna moja au nyingine, wameshiriki katika kuuboresha Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni ya Muswada huu ni kufuta Sheria ya Mbolea na Vyakula vya Mifugo ya Mwaka 1962 *(The Fertilizers and Animal Food Stuff Act, Cap 378)* na kutungwa Sheria mpya ya mbolea inayokidhi mabadiliko ya kijamii na kiuchumi, kulingana na soko huria katika sekta ndogo ya mbolea; na kuweka mazingira mazuri yanayoruhusu wadau wote katika Sekta kushiriki kikamilifu katika mfumo wa soko huria kama linavyohusiana na mbolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria inayopendekezwa itasaidia kusimamia na kuratibu matumizi ya uendeshaji wa biashara ya mbolea katika mazingira ya soko huria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unazingatia maeneo muhimu yafuatayo:-

(i) Kuanzisha kwa Mamlaka ya Taifa ya Usimamizi na Udhibiti wa Ubora wa Mbolea *(Tanzania Fertilizer Regulatory Authority).*

(ii) Kusimamia na kuratibu utengenezaji, uagizaji, uuzaji na matumizi ya mbolea.

(iii) Kuhakikisha kuwepo kwa matumizi endelevu ya mbolea nchini yenye kuendana na hifadhi ya mazingira.

(iv) Kuweka utaratibu wa ukaguzi na uchambuzi wa mbolea katika ngazi zote kuanzia bandarini, ghalani na kwenye maduka, kwa lengo la kuhakikisha kuwa mbolea yenye ubora unaokubalika ndiyo inayotumika nchini.

(v) Kuainisha mbolea zitakazotumika kulingana na aina ya udongo na kanda za uzalishaji wa mazao *(Agro Ecological Zones).*

(vi) Kuwepo kwa nguvu za kisheria zitakazohakikisha kupatikana kwa takwimu na taarifa muhimu za mbolea kutoka kwa wadau wa mbolea.

(vii) Kuzifanyia majaribio mbolea zote kabla ya kutumika na kuimarisha mamlaka za Serikali zinazohusika na utafiti wa mbolea ili zitoe ushauri unaostahili kwa wafanyabiashara wa mbolea na wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada wa Sheria ya Mbolea umegawanyika katika sehemu tisa kama ifuatavyo:-

Sehemu ya kwanza ya Muswada huu inaainisha vipengele vya awali ikiwa ni pamoja na jina la sheria, tarehe ya kuanza kutumika na tafsiri ya maneno yaliyotumika katika sheria hii.

Sehemu ya pili ya Muswada inaanzisha Mamlaka ya Taifa ya Usimamizi na Udhibiti wa Ubora wa Mbolea ambayo itahusika na uratibu, usimamizi wa biashara na matumizi ya mbolea nchini. Usimamizi wa Mamlaka hii utakuwa chini ya Bodi.

Sehemu ya tatu inahusika na usajili wa aina zote za mbolea zitakazotumika nchini. Usajili wa mbolea utasaidia uratibu na usimamizi wa ubora wa mbolea hizo kama ilivyo kwenye viuatilifu *(pestcides)* na mbegu za mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkurugenzi wa Mamlaka ya Mbolea amepewa mamlaka ya kufuta usajili wa mbolea ambazo hazikidhi masharti ya usajili. Sehemu hii pia inampa madaraka Mkurugenzi wa Mamlaka kutoa leseni kwa wafanyabiashara wa mbolea, kwa lengo la kuhakikisha kuwa kampuni au mtu yeyote anayejihusisha na biashara hii anazingatia sheria na ana uwezo stahili.

Sehemu ya nne ya Muswada inaweka masharti ya kuzingatia katika utengenezaji, uagizaji kutoka nje na uuzaji wa mbolea, ikiwa ni pamoja na uhifadhi wake. Sehemu hii inalenga kuhakikisha kuwa biashara na matumizi ya mbolea vinazingatia ubora na uhifadhi wa mazingira. Masharti yaliyomo katika sehemu hii ni pamoja na kuweka mkazo kwa wenye viwanda vya mbolea, kutumia malighafi toka hapa nchini.

Sehemu ya tano inahusu ukaguzi na uchambuzi wa mbolea, uteuzi wa wakaguzi na wachambuzi wa mbolea na madaraka yao. Ukaguzi utasaidia kuhakikisha mbolea inayomfikia mkulima ina ubora unaostahili.

Sehemu ya sita inahusu utaratibu wa kukata rufaa endapo mtu atakuwa hajaridhishwa na uamuzi wa Mkurugenzi wa Mamlaka ya Mbolea na Watendaji wengine katika Mamlaka hiyo.

Sehemu ya saba inaelezea juu ya masuala ya fedha za Mamlaka ya Mbolea, ikiwa ni pamoja na vyanzo vya mapato, utunzaji na ukaguzi wa hesabu.

Sehemu ya nane inahusu makosa na adhabu kwa wakiukaji wa sheria, ikiwa ni pamoja na utoaji wa fidia kwa mtu atakayeathirika kutokana na ukiukaji wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tisa inahusu masuala ya jumla. Sehemu hii inaainisha madaraka ya Waziri kutunga kanuni zitakazowezesha usimamizi mzuri wa sheria. Sehemu hii itaweka utaratibu wa mpito wa miezi kumi na miwili ya kuwawezesha wafanyabiashara wa mbolea kusajili mbolea ambazo zimekuwa zikitumika nchini kabla ya kuanza kwa sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unakusudia kutungwa kwa sheria ili kuleta matokeo yafuatayo:-

(i) Kufutwa kwa Sheria ya Mbolea na Chakula cha Mifugo ya Mwaka 1962 na kutungwa sheria mpya ya mbolea.

(ii) Kuimarishwa kwa ubora na usimamizi wa haki za wakulima zinazohusiana na teknolojia ya matumizi ya mbolea.

(iii) Kuwekwa kwa utaratibu mzuri utakaowezesha upatikanaji wa taarifa muhimu kuhusu viini lishe vya mimea mbalimbali.

(iv) Kuweka utaratibu wa kusimamia utekelezaji wa mikataba mbalimbali ya kimataifa inayohusu mbolea.

(v) Kuwa na utaratibu na usimamizi rasmi wa uagizaji wa mbolea kutoka nchi mbalimbali kwa manufaa ya maendeleo ya kilimo cha Tanzania.

(vi) Kuwa na mipango madhubuti ya kujenga uwezo na kuagiza, kuhifadhi, kusambaza na kutumia mbolea kwa kuzingatia ushauri wa kitaalam. Uzalishaji wa mazao utaongezeka kutokana na matumizi endelevu ya mbolea zenye ubora unaostahili.

(vii) Kuoanishwa kwa shughuli za hifadhi ya mazingira na zile za matumizi ya mbolea ya aina mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, kupitia kwako, naomba Waheshimiwa Wabunge, waujadili Muswada huu na hatimaye upitishwe na kuwa Sheria ya Mbolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana kwa kunisikiliza na naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. BENSON M. MPESYA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kutoa taarifa hii, Kamati inapenda kuungana na Watanzania wote, kutoa pole na rambirambi zetu kwa Wananchi wa Jimbo la Busanda – Geita, kwa kuondokewa na Mbunge wao mashuhuri, Marehemu Kabuzi Faustine Rwilomba. Mungu awape moyo wa subira katika kipindi hiki cha majonzi kwao. Tunaamini subira hiyo itawapatia Mbunge mpya wa kuwawakilisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tulimfahamu Mheshimiwa Rwilomba, Taifa limempoteza kiongozi imara, mcheshi, jasiri na mwalimu wa wengi; alikuwa kinara katika kutetea maslahi ya Taifa letu. Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Marehemu mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, kwa niaba ya Mwenyekiti, napenda kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, kuhusu Muswada wa Sheria ya Mbolea wa Mwaka 2008 *(The Fertilizers Act, 2008)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kutoa maoni ya Kamati, naomba kutumia nafasi hii kuwapongeza wakulima wote nchini, kwa kazi nzuri ya uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara hapa nchini. Tunatambua na kuthamini sana mchango wao wa kuboresha kilimo nchini, pamoja na changamoto nyingi zinazowakabili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama sote tunavyofahamu, mbolea ni kirutubisho muhimu kwa uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara. Mbolea ni kichocheo muhimu katika mchakato wa Mapinduzi ya Kilimo nchini. Mpaka sasa matumizi ya wakulima wetu ni kidogo sana. Kwa takwimu zilizopo, matumizi ya mbolea nchini ni wastani wa kilogramu 6 mpaka 9 kwa hekta, wakati nchi kama Afrika ya Kusini wanatumia wastani wa kilogramu 50 kwa hekta na Kenya kati ya 12 mpaka 14 kwa hekta. Katika mazingira ya sasa ya uchumi wa soko ni muhimu kuwa na mfumo mzuri wa usimamizi, uagizaji, utengenezaji (uzalishaji), uuzaji na utumiaji wa mbolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufanikisha mchakato wa Mapinduzi ya Kilimo na kuhakikisha wakulima wanapata mbolea kwa wakati na kwa bei nafuu, haja ipo ya kuwa na mfumo wa sheria utakaowezesha hayo kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Mheshimiwa Waziri mtoa hoja alivyoeleza hivi punde, Muswada huu unakusudia kufuta Sheria ya Mbolea na Chakula cha Mifugo ya Mwaka 1962. Sheria hiyo inayokusudiwa kufutwa haikuwa na mfumo thabiti wa kusimamia mwenendo wa biashara ya mbolea, yaani uagizaji, utengenezaji (uzalishaji), uuzaji, usambazaji na utumiaji wa mbolea. Muswada huu unakusudia kuziba upungufu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilifanya jumla ya Vikao vinne (4) Jijini Dar es Salaam kuujadili Muswada huu. Kikao cha kwanza kilifanyika tarehe 6 Aprili, ambacho kilihudhuriwa na Naibu Waziri ambaye aliambatana na Watumishi wengine akiwemo Naibu Katibu Mkuu. Katika kikao hicho, Naibu Waziri aliwasilisha Hati ya Maelezo na madhumuni ya Muswada kwa Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 8 Aprili, 2009, kilifanyika kikao cha pili na Kamati iliwakaribisha wadau ili waweze kuujadili Muswada husika. Ushiriki wa wadau ulikuwa wa kuridhisha kwani wadau muhimu wote walialikwa na kufika.

Baadhi ya wadau hao ni pamoja na Wawakilishi wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA), Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA), Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC), Taasisi ya Mbolea Tanzania, Baraza la Kilimo Tanzania na Taisisi ya Utafiti wa Kilimo ya MLINGANO. Wadau wote hawa walitoa maoni muhimu sana ambayo yamezingatiwa katika Jedwali la Marekebisho, kama ambavyo limewasilishwa na Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kikao cha tatu kilifanyika tarehe 9 Aprili, 2009 na kilihusisha Wizara na Kamati. Katika kikao hicho, Kamati ilipata fursa ya kutoa maoni na ushauri na kufanya marekebisho na mabadiliko katika Muswada kama inavyooneshwa kwenye jedwali la marekebisho lililokwishawasilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tarehe 14 Aprili, 2009, Kamati ilifanya kikao cha nne ambacho ni cha mwisho na Wizara. Kamati ilipitia Jedwali la Mabadiliko na iliridhishwa na mabadiliko yaliyofanyika, kwani yalizingatia maoni na ushauri wa wadau na Kamati. Kwa hiyo, Kamati inashauri Bunge lako Tukufu, liujadili Muswada huu na hatimaye kuupitisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaipongeza na kuishukuru Wizara, kwa kukubaliana na ushauri wa Kamati na wadau. Kamati imeridhishwa na Muswada huu, kwani unalenga kuleta tija katika kilimo na kwa kiasi kikubwa, kupunguza malalamiko na manung'uniko dhidi ya usambazaji na upatikanaji wa mbolea kwa bei nafuu kwa mkulima hapa nchini. Pamoja na kuridhishwa huko, Kamati inatoa maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

(a) Serikali iendelee kuhamasisha na kutoa elimu kwa wakulima kuhusu umuhimu wa kuongeza matumizi ya mbolea ili kuleta tija, kwani kati ya nchi zinazotumia mbolea kwa kiasi kidogo duniani Tanzania ni mojawapo. Aidha, kuwepo na Maafisa Ugani wa Kilimo ambao watatoa elimu kwa wakulima kuhusu matumizi sahihi ya mbolea.

(b) Serikali iandae mipango ya kutengeneza mbolea nchini kwa kutumia malighafi tulizonazo kama vile gesi, *phosphates* na madini mengine. Aidha, vikwazo vigumu vya uingizaji wa mbolea vitolewe ili kuhamasisha uingizaji na hatimaye kuongeza matumizi ya mbolea kwa wakulima bila kuathiri umuhimu wa ubora wa mbolea hizo.

(c) Serikali ijitahidi kupunguza utitiri wa vyombo ambavyo vinaweza kumwongezea mkulima gharama.

(d) Kutokana na wakulima kutofautiana kipato na ukubwa wa mashamba, Kamati inashauri vifungashio *(Packaging Materials)*, ziwe zinatofautiana kuanzia kilo moja hadi hamsini ili kuwezesha kila mkulima kutumia mbolea tofauti na ilivyo sasa ambapo mbolea inapatikana katika ujazo wa kuanzia kilo hamsini.

(e) Baada ya Muswada huu kupitishwa na kuwa sheria, Serikali ihakikishe inatengeneza Kanuni mapema iwezekanavyo ili kuondoa mianya ya kutowajibika na kuwezesha utekelezaji wa mzuri kwa mamlaka zote zinazohusika.

(f) Ili kuwezesha matumizi sahihi ya mbolea, Serikali ifanye uchambuzi wa udongo *(soil analysis)* ili kubaini mahitaji ya virutubisho ili kuepuka kupeleka mbolea zisizohitajika kwa baadhi ya maeneo katika nchi.

(g) Kutokana na kutokuwa na viwanda vya mbolea vya kutosha nchini, Kamati inashauri kuwepo na vivutio *(incentives)* kwa wawekezaji wa viwanda vya mbolea vitakavyoanzishwa hapa nchini.

(h) Serikali ifute kodi ya usafirishaji wa mbolea *(VAT)* ili kupunguza bei ambayo inakuwa mzigo kwa mkulima kwani ndiye mlaji wa mwisho.

(i) Mkulima alipwe fidia anapokuwa ameuziwa mbolea yenye virutubisho chini ya kiwango na kumsababishia hasara ya uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati, kwa ushirikiano wao katika kuuchambua Muswada huu. Naomba kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Gideon A. Cheyo - Mwenyekiti, Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Teddy L. Kasella-Bantu, Mheshimiwa Charles N. Keenja, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Castor R. Ligallama, Mheshimiwa Joyce N. Machimu, Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mheshimiwa Said J. Nkumba, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said, Mheshimiwa Abdulkarim E. Shah, Mheshimiwa Kaika S. Telele na Mheshimiwa Benson M. Mpesya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inawashukuru wadau wote waliojitokeza mbele ya Kamati na kushiriki kikamilifu katika kuwasilisha maoni na mapendekezo ambayo yamesaidia kuuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. David M. David, Naibu Katibu Mkuu, Bibi Sophia Kaduma, pamoja na Watendaji wote wa Wizara, kwa ushirikiano wao katika kipindi chote cha uchambuzi wa Muswada.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha maoni ya Kamati. Napenda pia kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas D. Kashililah, kwa kuiongoza Ofisi ya Bunge na kuiwezesha Kamati kukamilisha Taarifa hii. Aidha, napenda kuwashukuru Makatibu wa Kamati; Ndg. Frank K. Mbumi na Ndg. Pamela E. Pallangyo, kwa kuihudumia Kamati vizuri na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshukuru Mwenyekiti wangu wa Kamati, kwa kunipa fursa ya kusoma taarifa hii hapa; imekuwa ni heshima kwangu na kwa wapiga kura wangu wote wa Jimbo la Mbeya Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono Muswada. Ahsante! *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Wewe umeridhika kabisa. Sasa naomba nimwite Msemaji wa Kambi ya Upinzani, atoe maelezo kuhusu Muswada huu.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, ningependa kutumia fursa hii kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii niweze kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa

Sheria ya Mbolea ya Mwaka 2008 *(The Fertilizers Act, 2008),* kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 86(6), Toleo la 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa, naomba kutoa rambirambi zangu kwa ndugu na jamaa wa wahanga wa ajali ya boti iliyokuwa ikitokea Tanga kwenda Pemba hapo tarehe 14/4/2009, ambapo hadi sasa imeripotiwa kuwa maiti kumi na nne zimepatikana na kuzikwa mwambao wa Mombasa, Kenya. Naomba Mwenyezi Mungu, awape wafiwa roho ya subira na ustahimilivu na azilaze roho za Marehemu hao mahali pema peponi. Amina.

Vilevile nawapa pole wale wote waliopata majeraha, nawaombea wapate unafuu haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiongozi wa Upinzani Bungeni aliwataka Mheshimiwa Ali Khamis Seif na Mheshimiwa Ali Said Salim, washirikiane na wahusika katika ajali hiyo kule Tanga na baadae Pemba kwa niaba ya Wabunge wote. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kupitia mamlaka yake ya SUMATRA, kufanya ukaguzi makini kwa vyombo vinavyosafirisha abiria na mizigo na kuwa tayari kutoa msaada haraka mara ajali zinapotokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuanza kuangalia vifungu vya Muswada huu wa sheria, naomba kwanza tuangalie madhumuni yake. Jambo la kujiuliza ni je, kweli Tanzania inahitaji kuwa na sheria ya mbolea inayojitegemea; na, je sheria hii inakuwepo kwa manufaa ya nani hasa; mkulima, mfanyabiashara au Serikali? Je, Muswada huu umezingatia Sera ya Kilimo na Mifugo ya Mwaka 1997?

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo kuu la Sera ya Kilimo ni kuinua maisha ya watu wote ambao msingi wa shughuli zao na namna yao ya maisha unategemea kilimo na wengi wa watu hawa ni wakulima wadogo. Mwelekeo wa sera hii ni kuwawezesha kuzalisha kibiashara ili kuongeza kipato chao na cha taifa kwa ujumla. Japokuwa Sera ya Kilimo inasisitiza kukifanya kilimo kuwa cha kibiashara na chenye tija, lakini sera hii ipo kimya kuhusiana na mbolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la msingi la kujiuliza katika Muswada huu ni je, kwa vipi wadau hawa, yaani wakulima wamehusishwa; na je, Muswada huu una lengo linaloendana na kuwafanya wakulima kunufaika au ni aina nyingine ya jinamizi kwa wakulima kama ulivyo utaratibu wa mbolea ya ruzuku ambapo wanaonufaika zaidi ni wafanyabiashara?

Mheshimiwa Naibu Spika, japokuwa Muswada huu umeanzisha bodi ambayo imepewa madaraka na uwezo kuangalia taslia nzima ya mbolea *(fertilizer industry),* lakini kuna jambo ambalo ndilo limekuwa likisababisha ucheleweshaji wa mbolea kwa wakulima nalo ni taratibu za kikiritimba zilizopo kwenye bandari zetu, pale gharama za bandari za siku saba zinapomalizika *(7 days grace period),* kunakuwa na ushuru wa aina mbalimbali.

Yote haya ni masuala mtambuka na yapo nje ya uwezo wa bodi. Hiki kinaendelea kuwa kilio kikubwa sana kwa taslia ya mbolea kwa wakati huu ambao mbolea nyingi inaingizwa toka nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, inafaa pia tujiulize, je kwa kutunga Muswada huu ni kweli tunapeleka madaraka kwa wananchi toka Serikali Kuu *(decentralization by devolution - D by D)* au tunazidisha ukiritimba ambao hauleti tija kwa mkulima wa kawaida?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuangalia suala la ubora wa mbolea, tuna mamlaka tatu za Serikali ambazo zina maabara za kisasa; ambazo ni maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Maabara ya Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) na Maabara ya Shirika la Viwango la Taifa (TBS). Swali la kujiuliza ni kwa vipi taasisi zote hizi zitashindwa kuhakiki ubora wa mbolea?

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, Kambi ya Upinzani inadhani tatizo la msingi katika taslia nzima ya mbolea hapa nchini si ubora au uzalishaji bali ni akina nani wamehodhi soko hilo, kiasi kwamba hata Serikali imeshindwa kudhibiti mzunguko mzima wa soko la mbolea hapa nchini. Jambo hili limeleta ukiritimba mkubwa sana na kusababisha wakulima waonekane kuwa wanyonge katika nchi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaona kuwa Muswada huu ungeweka njia bora za kusimamia na kuhakikisha kuwa mbolea kama mojawapo ya pembejeo, inawafikia wakulima kwa wakati muafaka na kwa bei inayostahili ili lengo kuu la sera ya kilimo na lile la MKUKUTA liweze kufikiwa. Serikali iendelee kuyahamasisha makampuni makubwa duniani kuleta mbolea hizo kwa wingi ili kuleta unafuu wa bei.

Kwa kuanzia, Serikali imekubaliana na Kampuni ya Yara kufungua Ofisi yake hapa nchini na imefanya hivyo kwa jina la Chapa Meli, lakini bado wafanyabiashara binafsi wamehodhi soko la mbolea na wamekuwa na nguvu kuliko Serikali kwa kuuza mbolea kwa bei wanayotaka wao. Je, hili ni suala la kuunda Mamlaka mpya kukabiliana nalo au ni suala la kusimamia sheria zilizopo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la uzalishaji wa mbolea kwa yeyote anayetaka kufanya hivyo, Kambi ya Upinzani inaona hilo hata halihitaji uanzishwaji wa Mamlaka mpya ya kutoa vibali husika, kwani kanuni na taratibu zilizopo kuanzia Mamlaka ya Usimazi wa Mazingira (NEMC), jinsi ya kufanya tathmini ya athari ya mazingira (EIA) na kufuatiwa na taratibu za kawaida za uanzishwaji wa viwanda ambazo zipo zinatosheleza haja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani imetoa angalizo hilo, kwa kuangalia hali halisi ya uchumi; si Watanzani tu bali wa Dunia nzima ulivyo na haitakuwa busara kutunga sheria ambayo itashindwa kutumika kutokana na kutokuwepo kwa rasilimali na vitendea kazi ili kufanikisha malengo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la Tanzania si upungufu wa sheria lakini kinachokosekana ni usimamizi makini wa sheria zilizopo, ukosefu wa utashi, rasilimali na vitendea kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kifungu cha 21 cha Muswada kinachohusiana na taratibu za uingizaji wa mbolea toka nje ya nchi; Kambi ya Upinzani inaona pamoja na taratibu zote zilizowekwa katika kifungu hicho ni bora Muswada ungekuwa na kifungu kinachoelezea jinsi ya kuharakisha utoaji wa mbolea pale inapoingia nchini, kwa kuzingatia kuwa mbolea huingizwa kwa kiasi kikubwa. Ucheleweshaji mbali ya kuongeza gharama na bei ya mwisho kwa mkulima, vilevile husababisha kupoteza ubora wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha pili kinachohusu tafsiri ya maneno, neno *committee* limeendelea kutolewa tafsiri japokuwa vifungu ambavyo vilikuwa vinatolewa tafsiri ya neno hilo vimefutwa katika jedwali la marekebisho yaliyofanywa na Mheshimiwa Waziri. Hivyo, Kambi ya Upinzani inaona itakuwa vyema pia kuondoa neno hilo kwenye tafsiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 25(2) cha Muswada baada ya kufanyiwa marekebisho kwa kufuta neno *Board* na kuweka neno *Director*; Kambi ya Upinzani inaona neno *itself* lifutwe na badala yake neno *himself* liongezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 31(2) cha Muswada kinachosomeka nanukuu: *"Any person who applies fertilizer or fertilizer supplements shall ensure compliance with the standards prescribed in the regulations or guidelines";* Kambi ya Upinzani inaona neno *"any person"* maana yake hata mkulima mwenyewe anahusika. Hivyo basi, kama llitatumika kwa mazingira halisi ya wakulima wa Tanzania, maana yake ni kuwanyima haki ya kudai fidia pale mbolea wanayotumia itakapobainika kuwa haikutakiwa kutumika, japokuwa waliingia gharama ya kuinunua. Kifungu hiki kiangaliwe upya ili kisimuumize mkulima pale janga litakapotokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 34(1) cha Muswada kinahusu mamlaka ya Wakaguzi kuwa *"may at any reasonable time …"* Kifungu kidogo cha (a) *"enter upon and examine any place, premises…* "

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 34(7) kinasema *the Inspector shall, before inspection of the premises, take reasonable steps to ensure that the owner or his authorized representative is present while carrying out inspection under this Act.* Kambi ya Upinzani inaona vifungu hivyo viwili vinatakiwa kuoanishwa *(harmonized)*, ili kuondoa mkanganyiko wakati wa utekelezaji wa sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 44 cha Muswada kinahusu *"burden of proof"*, naomba kunukuu *"… and in the case of an order, direction or requirement not published in the Gazette, that he had no notice of the contents of the order, direction, as the case may be required, shall lie on the accused person."* Kambi ya Upinzani inaona kuwa kifungu hiki moja kwa moja kinamnyima haki ya msingi mtuhumiwa, kwani

kinaeleza bayana kuwa mtuhumiwa hana uelewa wa kile kilichomo kwenye taarifa hivyo ni kwa vipi atathibitisha kuwa hana hatia? Ili kuweka mtiririko mzuri wa kifungu hicho ni bora maneno niliyonukuu hapo juu yafutwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, Kambi ya Upinzani inaomba ufafanuzi kwa nini utaratibu wa kutoa mbolea ya ruzuku kwa njia ya *voucher* haukuwekwa kwenye sheria hii ya mbolea? Hii imetokana na malalamiko mengi sana kutoka kwa wananchi ambao wana haki ya kupata mbolea hiyo. Kwa kuwa hakuna chombo au utaratibu ulio wazi wa kisheria wa kuwawezesha kupata haki hiyo, imesababisha wao kukosa haki hiyo na Serikali kupoteza kiasi kikubwa cha fedha za walipa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo machache na kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, nawashukuruni sana Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Msemaji kutoka Kambi ya Upinzani.

Waheshimiwa Wabunge, ninao wachangiaji kama saba hivi, lakini Muswada unaendelea mpaka baadae mchana. Kwa hiyo, kwanza nitamwita Mheshimiwa Godfrey Zambi, atafuatiwa na Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Simbachawene, nafikiri na Mheshimiwa Dkt. Mzindakaya anaweza kufikiwa.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nashukuru kupata nafasi kuwa mchangiaji wa kwanza kwa Muswada huu wa Mbolea. Niseme kwamba, nilitarajia pengine ningechangia jioni, kwa hiyo, inawezekana maandalizi yangu hayakufikia mwisho, lakini kwa sababu ni Muswada ambao unagusia maslahi ya wakulima wa nchi hii na wananchi wa jimbo ninalowakilisha, Wanambozi wakiwa wahusika sana, basi nitajitahidi kuchangia yale ambayo Mwenyezi Mungu atanijalia niweze kuyasema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijasema pamoja na kwamba Mheshimiwa Spika alishasema na kanuni inasema hivyo, lakini wakati mwingine inakuwa ngumu kunyamaza wakati wenzako wanasema hasa pale ambapo tunafikwa na msiba ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii, kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Mbozi Mashariki, kutoa rambirambi zangu kwa Wananchi wa Jimbo la Busanda, kwa kupoteza Mbunge wao Ndugu yetu Faustine Kabuzi Rwilomba, Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Marehemu mahali pema peponi, Amin.

Kwanza, naomba niishukuru sana Wizara kwa kuleta Muswada huu ili uweze kupitishwa na Bunge lako. Nina hakika Muswada huu utasaidia sana, hasa Wakulima wetu kupata mbolea kwa utaratibu mzuri zaidi kuliko ilivyokuwa huko nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ninataka kujiuliza kwamba; kuwa na sheria lakini pia upatikanaji wa mbolea yenyewe ni mambo mawili tofauti; tunaweza tukawa na

sheria nzuri sana inayozungumzia suala la mbolea, utengenezaji, usambazaji, uandikishwaji na kadhalika lakini mbolea yenyewe isipatikane, huu ndiyo wasiwasi wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana kuna mchangiaji mmoja alisema kwamba, tuna sheria nyingi sana lakini pengine matumizi ya sheria haya yanaweza yakawa yanakwamishwa na mambo mbalimbali. Mimi nina hakika sheria hii haitakwamishwa na hayo mambo mengine ambayo yanaweza yakajitokeza. Naamini kwamba sheria itafanya kazi yake vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nizungumze kwamba, tunazungumzia usajili wa mbolea mbalimbali; hilo linazungumzwa sehemu ya tatu ya Muswada, usajili wa mbolea aina zote lakini pia na usimamizi wa ubora wa mbolea yenyewe. Hapa naomba nizungumze najua sheria imeliweka hilo, lakini kabla ya sheria hii kuja na kwa sababu bado haijaanza kutumika ni mpaka hapo tutakapoipitisha na Mheshimiwa Rais kuisaini, utaratibu wa sasa wa usimamizi wa mbolea ni mbaya sana.

Hili linajionesha katika maeneo ambayo yanatumia mbolea katika nchi hii. Nina hakika kwa sababu tunaleta sheria basi hili Wizara itahakikisha kwamba litasimamiwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kwa undani kidogo suala linalohusu usimamizi wa ubora wa mbolea, hili pia nililizungumza nilipoingia kwenye Kamati tarehe 6 pale Dar es Salaam; kwamba, hili naomba Waziri atufafanulie, pamoja na kwamba sheria haipo lakini bado tunasimamia mbolea ambazo zinaenda kwa wananchi hata leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu kule Mbozi na mahali pengi, tumepelekewa mbolea ya Minjingu ambayo imewaharibia uzalishaji sana Wananchi wa Wilaya ya Mbozi na inawezekana na mahali pengine. Wananchi wale wanasema mbolea hii kama haitarekebishwa, naomba niseme kwa niaba yao, nina hakika kwa sababu ni wengi wananiona na wananisikiliza wamesema; Serikali isituletee mbolea hiyo.

Nalisema hili kwa sababu ndiyo ujumbe wao, naweza nikawa nawakwaza wengine lakini naungana na Wananchi wa Wilaya ya Mbozi na mimi nimeona mashamba ya wananchi yameharibika sana kwa wale waliotumia mbolea ya Minjingu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliposoma sheria hii nikasema leo tunasema sheria itadhibiti usimamizi wa ubora wa mbolea, hivi huko nyuma tulikuwa hatuna usimamizi wa ubora wa mbolea ambayo tunawapelekea wananchi?

Mhehsimiwa Naibu Spika, mimi sina hakika kama mbolea ya Minjingu imefanyiwa utafiti wa kutosha; kule Mbozi walikuwepo Maprofesa wa SUA, alikuwepo Dokta Msola ambaye yupo Kilimo, nimezungumza naye mara nyingi nimemweleza mbolea hii haifai kwa Mbozi; na wakati mwingine hata yeye anakiri kwamba, kuna

baadhi ya maeneo kule Mbozi mbolea hii haifai, lakini wakati mwingine wanasema wananchi hawajui matumizi ya mbolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wananchi wa Mbozi wamekuwa wanalima miaka mingi. Baba yangu alikuwa mkulima na nimesoma kwa sababu ya baba kuwa mkulima na mimi mwenyewe nazijua mbolea vizuri. Leo huwezi kumdanganya Mwananchi wa Mbozi, nina hakika na wananchi wa mahali pengine wanaotumia mbolea, huu siyo ubora wa mbolea ya aina fulani. Kwa hiyo, kumwambia mwananchi hajui kutumia mbolea si kumtendea haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba sheria hii isimamiwe vizuri, lakini pia leo Serikali iwape ufumbuzi Wananchi wa Wilaya ya Mbozi juu ya mbolea ya Mijingu. Tunaomba kama haitakuwa na marekebisho, mbolea hii msiwaletee Wananchi wa Mbozi kwa sababu mwaka huu imetudidimiza sana.

Namwomba Mheshimiwa Waziri, achukue maneno yangu waende Mbozi na mahali pengine hasa Mbozi mahali ninapotoka na ninayaona mashamba ya wananchi, wakaangalie ni namna gani mahindi ya watu yameharibika kutokana na matumizi ya mbolea ya Minjingu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna masharti wanayotueleza kwamba, ukitaka uzalishe vizuri chukua mifuko miwili ya Minjingu na nusu mfuko wa Urea halafu upandie; hutapata matumizi mabaya. Sasa *complication* zote hizi ni za nini kwa mkulima wa kawaida? Kwa hiyo, naomba sana Waziri utupe ufafanuzi wa kutosha juu ya suala hili, lakini pia nimeshazungumza na wewe juu ya suala la Mbolea ya Minjingu. Nadhani mlikuwa mnasema inawezekana mbolea hii imekosa kiuatilifu cha aina fulani, sasa kama ndiyo hivyo basi muwaeleze Watanzania na wananchi hawa ili wajue kama wanaitumia waitumieje lakini baada ya kuboresha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba pia nizungumze kwamba, tunaanzisha bodi nyingi sana za mazao; tuna bodi hii ambayo itakuwa inasimamia utaratibu mzima wa suala la mbolea, tatizo tulilokuwa nalo Wizara ya Kilimo kwenye bodi hizi ni kutokuzipa fedha za kutosha kuweza kufanya kazi zake sawasawa; hili ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Waziri; nilikwenda Moshi pale TCB kwa ajili ya kufuatilia mnada wa zao la kahawa, moja ya mambo ambayo tuliyakuta pale ni bodi pia kutokufanya baadhi ya majukumu yake sawasawa kwa sababu ya upungufu na ukosefu wa pesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mathalani mnawapa shilingi bilioni moja, lakini shilingi bilioni moja zile ambazo zipo kwenye bajeti kwamba mtawapa mpaka mwaka unaisha, hawapati hata nusu ya pesa hizo. Tunategemea bodi hizi zifanye kazi namna gani kama kweli tunataka ziwasaidie wananchi? Tunatunga sheria nzuri lakini usimamizi wake hauwezi kuwa mzuri, kwa hiyo, nina wasiwasi hata sheria hii tunayoitunga kama zitatolewa pesa za kutosha kuiwezesha kufanya kazi zake sawasawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna watu ambao wanasema watakuwa wanasimamia ubora wa mbolea, kuna idara mbalimbali zitakazokuwepo kwenye bodi hii, lakini utendaji wao wa kazi utategemeana na kuwepo kwa pesa; sasa tusije tukapata tena visingizio kwamba watu walishindwa kwenda kuchunguza ardhi kule, kwa sababu pesa hazikuwepo. Itakuwa haina maana ya kuwa na sheria na tutakuwa hatuwezi kuwasaidia wananchi wa nchi hii, ambao nina hakika wana ari kabisa ya kulima lakini bado Serikali inashindwa kuzipatia bodi zinazoratibu shughuli hizi kadiri inavyotakiwa ili ziweze kufanya kazi zake sawa sawa. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali tujaribu kuliangalia hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nilizungumza hata nilipokwenda kwenye Kamati ile na Naibu Waziri ndiye aliyekuwepo; nilisema bodi hizi muhimu sana zinazogusa maslahi ya wananchi, basi tunaomba muwaweke na baadhi ya Wabunge ambao inawezekana nao wana uzoefu na maeneo hayo, inawezekana wasiwe wataalamu lakini wana uzoefu wa maeneo hayo. Mimi sijasoma masuala ya mbolea kwa maana kama sayansi inayohusu masuala ya mbolea, lakini nimetoka kwenye eneo linalolima na nimekuwa nikitumia mbolea tangu wakati wa wazazi wangu na babu zangu na ninazijua mbola hizi. Kwa hiyo, kama mkiweka watu kwenye bodi kama hizi, hawa wanaweza wakasaidia sana bodi hizi lakini pia wakaisaidia hata Wizara yenyewe, kuweza kujua maoni ya wananchi juu ya masuala haya kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa manufaa ya wananchi, nimeona *schedule of amendment* sijaona mtu wa aina yoyote ambaye anaweza pengine akaliwakilisha Bunge kwenye Bodi hii ya Mbolea. Naomba hili liendelee kuangaliwa na watu wengine wanafikiri mtu anapokwenda kwenye bodi anafuata pesa, hamna mtu anayekwenda kwenye bodi ambayo inakaa mara nne kwa mwaka akafuata pesa, tunaenda kwa sababu tunataka tuisaidie Serikali lakini pia tuwasaidie wananchi wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ambalo ningependa nizungumze ni makosa na adhabu itakayotokana na ukiukwaji wa sheria yenyewe. Tunasema kwamba, sehemu ya nne na ya nane; mwananchi akitumia mbolea halafu ikaleta madhara kwenye mazao yake au mimea yake, anapaswa kulipwa fidia. Sasa mimi naomba Waziri atusaidie, nimesema awali kwamba wananchi wengi wa Mbozi, kwa kipindi cha mwaka huu wamepata madhara sana kwa sababu mbolea ile imejeruhi mimea yao; wale wananchi watasaidiwa namna gani na Serikali kwa sababu hawakutaka wao mazao yao yaharibike; tuliwapa mbolea waweze kuzalisha hekari moja, hekari hiyo moja imeharibiwa na mbolea ambayo nina hakika ni makosa ya Serikali ambayo yamewasababishia wale wananchi wapate hasara.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi hawa watasaidiwa namna gani na watumie utaratibu gani, chini ya sheria iliyopo sasa kwa sababu najua hii sheria haitaanza kutumika mpaka hapo tutakapoipitisha na baada ya Mheshimiwa Rais kuisaini; leo wananchi wale watumie sheria gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri anawaambia nini Wananchi wa Mbozi ili waweze kumsikiliza lakini pia waweze kufarijika wakimsikia akiongea. Naomba nisisitize kwamba, pengine hili lisiwe na mjadala kwamba wananchi wale wanakosea

kama nilivyokwisha kusema awali, hawakujua kuitumia mbolea vizuri; hapana, wananchi wanajua kutumia mbolea lakini mbolea ile haiendani na ardhi ya maeneo mengi katika Wilaya ya Mbozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wananchi wa Mbozi watasaidiwaje kwani nina hakika wanaweza wakaingia kwenye tabu kubwa sana ya njaa katika kipindi hiki cha mwaka 2009/10?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kusema kwamba, Wananchi wa Mbozi ni wakulima wazuri sana, ninaiomba Serikali iwapatie mbolea na kwa bei wanazoziweza.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja na nina uhakika Waziri atatoa ufafanuzi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nichukue nafasi hii, kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Muswada huu. Kwanza, nitumie nafasi hii, kuipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuleta huu Muswada Bungeni. Niipongeze Serikali ya Awamu ya Nne, kwa kuona umuhimu wa kuendelea kuwajali wakulima; kila mara imekuwa ikihangaika kutafuta mbinu na namna mbalimbali ambazo zinaweza kusaidia kuboresha kilimo na kuwasaidia wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu haiko mbali na ulimwengu kama ulivyo sasa na ninaposema ninaipongeza Serikali kwa kuleta huu Muswada, ninafahamu kabisa kwamba, Muswada huu unaendana na mabadiliko ambayo yameendelea kutokea katika ulimwengu kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, idadi ya watu duniani sasa hivi kwa takriban miaka arobaini iliyopita, ongezeko la watu limeshafikia idadi ya watu bilioni tatu; miaka 40 iliyopita sasa hivi tunakaribia bilioni saba. Ongezeko hili ukilitazama kwa picha ya kiulimwengu, unaona kabisa kwamba, nchi za Asia karibu ongezeko hili la watu linachukua asilimia 60 ya watu wote katika ulimwengu. Tanzania pia ni miongoni mwa nchi ambazo zinasababisha ongezeko hilo la watu katika ulimwengu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ongezeko hili sasa ndiyo linaleta changamoto mbalimbali ambazo tunatakiwa kukabiliana nazo. Kumekuwa na mawazo ya kuhama sasa hivi kutoka katika kilimo cha kugeuza mazao ya chakula kuwa mazao ya kutengeneza mafuta ili kuweza kukabiliana na changamoto za kidunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapoingia katika picha hiyo ya kiulimwengu, ninasema ni lazima sasa tuiangalie nchi yetu ya Tanzania; na hivyo Muswada huu wa Mbolea utakuja pia kutusaidia kupambana na kile ambacho kimeanza kutokea katika dunia kwa ujumla wake. Muswada wa Mbolea utatoa majibu ya kero nyingi za wakulima wetu.

Nianze kuipongeza Serikali kwa mfumo wa vocha na Jimbo langu la Peramiho mwaka huu limekuwa miongoni mwa Majimbo ama Wilaya ambazo zimeshughulikiwa katika mfumo wa vocha kwenye suala la pembejeo hasa mbolea na mbegu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu leo unatusaidia kujibu maswali ya usambazaji, uzalishaji, matumizi na usimamizi kwa ujumla wake. Haya ndiyo mambo muhimu sana kwa wakulima wetu. Wakulima wengi wa nchi ya Tanzania wakiwemo wa Jimbo la Peramiho ni wakulima wadogowadogo; na haya yanayojitokeza kwenye Muswada ndiyo hasa mahitaji ambayo wanataka wayapate katika mfumo mzima wa pembejeo na mfumo mzima wa mbolea kwenye nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninafurahi sana kuona Muswada huu unazingatia suala kubwa la uzalishaji wa mbolea katika nchi yetu ya Tanzania. Kwa muda mrefu, kero ya upatikanaji wa mbolea imesababisha nchi hii kukosa kujitegemea kwa chakula na kukosa kutumia mazao ya chakula na mazao mengine kama mhimili wa Pato la Taifa. Sasa leo tunapopitisha Muswada huu, wakulima wetu wanasubiri kuona utekelezaji wa usimamizi wa uzalishaji wa pembejeo ya mbolea utakidhi vipi haja ya kuwa na viwanda ambavyo vitazalisha mbolea na kuondoa uhaba wa mbolea ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunaelekea huko, tukumbuke kwamba kwa sababu sheria itawalinda na kuwasimamia waagizaji wa ndani na nje, lakini pia na wazalishaji. Nadhani ni wakati muafaka wa kuangalia ni namna gani soko hili sasa linapanuka ili kutosheleza mahitaji ya mbolea katika nchi yetu ya Tanzania na tukifanya hivyo tutawasaidia wakulima wetu kupata mbolea kwa bei ambazo zinalingana na kipato chao. Suala la msingi si tu kuwepo kwa mbolea, lakini suala la bei ni kitu kingine ambacho kinatakiwa kizingatiwe ili kuongeza tija na kuongeza uzalishaji wa mazao yanayotumia mbolea katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na wachangiaji waliopita kwamba, nchi yetu ni kati ya nchi nyingi ulimwenguni ambazo zinatumia mbolea kwa kiasi kidogo sana. Ardhi yetu ni kubwa, wakulima wapo lakini mahitaji yanayohitajika na kiasi cha mbolea ambacho wakulima wanakipata havilingani na hivyo inasababisha wakulima wetu kuendelea kuwa duni na kuwa katika kilimo ambacho hakina tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kusisitiza kwamba, Muswada unazungumzia sana usimamizi wa ubora na sheria mbalimbali zitakazotumika kuhakikisha mbolea inayosambazwa kwa wakulima iwe na ubora wa viwango vinavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mkurugenzi wa Pembejeo, mwaka huu tulipata shida kweli ya mfumo wa vocha kwenye Jimbo langu la Peramiho. Mwezi wa pili, nilimpigia simu Waziri kumweleza Serikali ilichelewa kutoa fedha, wakala wakawa wanahangaika, ndiyo msimu hasa wa kuweka mbolea kwenye mashamba lakini mbolea haipatikani. Naomba niseme, nampongeza Mkurugenzi wa Pembejeo, alikuja kwenye Jimbo langu na kufanya ziara pale ili kutatua matatizo hayo ya wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo, ninaomba sana kwa sababu Muswada huu unazungumzia pia usambazaji, ratiba ya usambazaji na ubora wa mbolea iwe ni kitu cha msingi.  Mkoa wa Ruvuma tuna Agizo la Mlale linaloelezea ni lini mbolea ya kupandia iwe imefika kwenye Mkoa wa Ruvuma, kama mbolea hiyo haitafika katika muda huo, huu Muswada kwa Mkoa wa Ruvuma utakuwa hauna maana hasa Jimbo la Peramiho.  Kwa mfano, mwaka huu mbolea ya kupandia tumeipata mwezi wa kwanza na mwezi wa kumi na mbili, muda ambao tayari tulishapanda.  Kwa hiyo, kipengele cha usambazaji kwenye Muswada kama hakitasimamiwa vizuri, hata lengo jema la kuwasaidia wakulima halitakuwa na maana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipeleka maombi yangu kwa Mheshimiwa Waziri na kumwomba kwa sababu misimu ya kilimo inatofautiana ndani ya nchi yetu ya Tanzania, hebu wajaribu kuwa na sera itakayoongoza ni namna gani wazalishaji wa chakula waweze kusambaziwa mbolea kwa msimu unaotakiwa na wazalishaji wa mazao mengine ya biashara na kadhalika. Kwa hiyo, hilo ni suala lingine muhimu na kwa kuwa Muswada unatoa maelekezo halisi, Kamati za Halmashauri zimepewa madaraka hayo na sisi kupitia Kamati hizo tutaendelea kuishauri Serikali yetu.  Kwa kuwa sasa itakuwa ni Sheria, hapo itakuwa kazi kweli kweli kama Serikali itachelewa kusambaza Mbolea kwa wakati unaotakiwa.  Mheshimiwa Waziri, nadhani kuna shughuli kubwa inakuja mbele yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbolea ikichelewa itatusababishia kufeli katika uzalishaji, tuta-*appeal* kwenye Kamati na bodi zako na hivyo wakulima sasa watakuwa na mahali pa kusemea na kulalamikia.  Hiyo ni katika maeneo yote; eneo la ubora na eneo la muda wa kusambaza na kuhakikisha kwamba mbolea inawafikia wakulima kwa wakati unaotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli wakati mwingine mbolea hizi ambazo tumekuwa tukiziagiza nje, zimekuwa na upungufu wa namna moja ama nyingine; mimi nafikiri Muswada huu kwa sababu pia unasimamia ubora na ukiangalia bodi ilivyoundwa, kila mdau anayehusika na sekta muhimu, yupo katika bodi hiyo. Suala kubwa nadhani tutawaomba wenzetu wazingatie sana ubora.  Wale wakulima ukikutana nao wanahamasishwa kweli, wanapewa maelekezo ya matumizi ya mbolea lakini mbolea zinazoletwa kila muingizaji anaagiza kutoka katika nchi anayoifahamu yeye kulingana na utaratibu uliowekwa na Serikali.  Mbolea zile zina ubora tofauti na tatizo kubwa zinapoingia inakuwa ni msimu wa kilimo, hakuna tena muda wa kufanya majaribio ya ardhi kulingana na aina ya mbolea iliyofika.  Matokeo yake ni kama aliyoyasema Mheshimiwa Zambi, wakulima wataitumia ile mbolea, muda wa kutosha wa wataalamu wetu kufanya utafiti wa ardhi na aina ile ya mbolea kulingana na hali halisi haupo; hivyo, kinachokuja kuendelea ni kuanguka kwa uzalishaji na kuwaingizia wakulima wetu hasara.  Malalamiko haya pia nimeyakuta Jimboni kwangu katika vijiji nilivyovitembelea huko Igagula, Wino, Lusonga na maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana sheria hii tutakapoitunga, Mkurugenzi wetu azipitie hizo bodi ambazo zimeainishwa katika sheria yetu waweze kufanya kazi vizuri, kuhakikisha kwamba wakulima wa Tanzania sasa wanaweza kujikomboa kutokana na Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nafikiri upo umuhimu pia wa sheria nyingine nazo zikaangaliwa, ambazo zinaweza zikatoa msukumo wa ushirikishwaji katika hii sheria mpya tunayoiweka. Lengo la kusimamia suala zima la kuongeza matumizi ya mbolea katika nchi yetu ni kuongeza uzalishaji, lakini uzalishaji huu hauangaliwi kwenye *angle* hiyo ya mbolea tu, liko suala la zana bora za kilimo. Nadhani Sheria ya Mfuko wa Pembejeo tunatakiwa pia tuiangalie, kwa sababu wakulima watapatiwa mbolea ya kutosha kama zana za uzalishaji zitaendelea kuwa duni, matumizi hayo ya mbolea pia hayatawasaidia kujiongezea kipato, kwa sababu watashindwa kuhama katika ukulima ule mdogo mdogo na kuinuka na kuwa wakulima wakubwa, kwa kutumia vyombo na zana bora za kisasa zinazoweza kuzalisha na kuongeza uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuongeza uzalishaji wa chakula na mazao mengine ya kilimo ni kuongeza uchumi na pato la taifa letu la Tanzania. Sasa hivi tuna kazi kubwa sana ya mtikisiko wa fedha katika ulimwengu, sisi Watanzania kitu tunachoweza kusimamia sasa hivi ni kuhakikisha kwamba, uzalishaji wetu wa mazao ya chakula na mazao ya biashara ni wa kujitosheleza ndani ya nchi yetu. Mbolea itatusaidia, lakini kilimo bora na cha kisasa, nadhani ni kitu ambacho kinatakiwa kiangaliwe pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sheria nyingine zilizoko chini ya Wizara hii, ambazo zitatoa msukumo wa kusaidiana na sheria hii, nadhani ni wakati muafaka ziangaliwe zote kwa pamoja, ziweze kuboresha suala zima la uzalishaji wa mazao katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa kuboresha kilimo na umuhimu wa matumizi ya mbolea, wala si ajenda mpya; hii ni ajenda ya muda mrefu na ilishazungumzwa katika Serikali yetu. Ninadhani huu ni wakati muafaka sasa wa kuifanya ajenda hiyo iwe ya kutendewa kazi kwa nguvu na kusimamiwa kwa kiasi cha kutosha sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia themanini ya Wananchi wa Tanzania ni wakulima na wengi wao wapo vijijini na wanategemea mbolea ili kuhakikisha kwamba wanamudu kujikimu katika maisha yao ya kila siku na kupambana na umaskini ambao wamekuwa nao. Kwa hiyo, Serikali inapokuja na sheria hii, tunaona ni ukombozi mkubwa sana.

Ukisoma taarifa mbalimbali za kiulimwengu, unaona kabisa kwamba, karibu asilimia hamsini ya mbolea yote katika ulimwengu mzima, inatumika kuzalisha mazao ya chakula, mahindi, mpunga na ngano kwa kiasi kidogo, lakini asilimia hamsini iliyobakia ndiyo inaingia kwenye mazao mengine yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada ni muhimu, nauunga mkono. Ninaomba usimamizi makini katika utekelezaji. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia suala la kilimo hususan katika sekta hii ya mbolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeulizwa sasa hivi kwamba ili tuweze kufanya mapinduzi ya kilimo katika nchi yetu tufanye nini; jibu langu lingekuwa rahisi tu kwamba; ni kufanya fujo na fujo yenyewe ni kutafuta *shortcuts* na siyo njia ndefu. Kwa mfano, hatuwezi tukafikiri kwamba, tunaweza tukafikisha mbolea kwa mkulima na ambalo ndilo tatizo la msingi kama tutaendelea kurefusha utaratibu mzima wa suala la mbolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningesema tu kwamba, Halmashauri zote ziwe na magodauni yenye mbolea zinazotakiwa katika Wilaya na maeneo hayo. Hizi programu za kilimo; *ASDP*, *DADPS* na nyingine, zingetazama maeneo ambako wananchi wanahitaji moja kwa moja kuwa na mahusiano na Serikali yao kwa kuwasaidia kutoka kwenye tatizo la kilimo, nadhani kwa sasa tatizo lisingekuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo kama ningeulizwa ningesema ni kwamba, kama kweli Serikali inataka kufikisha mbolea kwa wakulima ni ama kuchagua kupata faida inayotokana na kodi ya mbolea au kutokupata faida hiyo na kupata faida itakayotokana na mazao ya kilimo. Ukitaka vyote hivi viwili uvifanye kwa wakati mmoja; ni dhahiri kwamba hutafanikiwa chochote kile na hasa kwenye kilimo.

Tatizo la wakulima wetu ni kwamba, mbolea inayofika bei yake ni kubwa mno. Utashangaa mimi ninatoka Mkoa wa Dodoma, lakini ninazungumzia suala la mbolea! Mimi nina vijiji takriban saba ambavyo vina mbolea, havina uzalishaji katika kilimo. Nina vijiji vya Lumuma, Kitati, Idaho, Rufusi, Idodoma, Malolo, Kinusi; bila mbolea hawajazalisha na hivyo mbolea ndiyo pembejeo muhimu kwao kuliko kitu kingine chochote. Mara zote wamekuwa maskini na wameshindwa kutoka katika dimwi la umaskini na kuajiriwa kuwa vibarua kwenye maeneo ya mashamba yao na wenye fedha, kwa sababu tu ya bei ya mbolea. Mbolea itatoka Dar es Salaam shilingi 20,000 lakini mpaka ifike Rufuzi, Lumuma, Kitati au Malolo, inafika shilingi 50,000; ni mkulima gani wa kawaida anayeweza kuinunua?

Ninahisi lipo tatizo la msingi na ni vizuri pamoja na kwamba sheria hii inakuja, kuzingatia madhumuni ya Muswada wa Sheria hii ni kuzingatia ujio wa masuala haya ya mbolea; yanayozingatia hali ya uchumi wa sasa na hali ya soko huria; na kwamba tunahitaji kuzalisha mbolea hapa nchini na pia kuingiza mbolea kutoka nje. Kwa hiyo, sheria hii inakuja kuzingatia hali hiyo.

Mwisho wa siku tujiulize; mkulima huyu ataipata hiyo mbolea kwa malengo haya tunayoyazungumza au pamoja na kupanua na kuweka hilo soko huria na mambo kadha wa kadha tunayotaka kuyaweka katika sheria hii bado mkulima wetu atakuwa pale pale? Wasiwasi wangu bado upo pale pale na ninahitaji nifafanuliwe masuala kadhaa yaliyopo katika Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, wachangiaji wengi mchango wao hautakuwa mzuri katika Muswada huu, kwa sababu *schedule of amendment* ambayo ni ndefu sana imeletwa tukiwa humu ndani. Sasa unazingatiaje *schedule of amendment* na kile ulichokisoma na kujiandaa? Hili linakuwa ni tatizo kubwa sana.

Niipongeze Wizara kwa kukubali kuondoa ile *National Fertilizer Advisory Committee*, ambayo ilikuwa katika *section* ya tatu na ninaunga mkono. Vilevile wamekwenda kuondoa tena *section* namba sita, *District Fertilizer Committee*, ambayo sasa ndiyo kilikuwa kiungo cha mkulima kule chini kabisa. Kwa hiyo, mambo yote hapa yamebakizwa kwenye *Tanzania Fertilizer Regulator Authority, section seven*, ambayo ipo juu sana; unazungumzia *Ministerial level*. Sasa nadhani hapa bado tunamwacha mkulima pekee yake kule chini.

Ningeshauri chonde chonde, turudishe hii ya *District* kwani ni muhimu sana. Kwa muundo wowote ambao ungekubalika na Halmashauri husika au na Wilaya husika, hizi ndiyo zinge-*link* sasa na hii *Regulatory Authority* na Wizara. Tukiondoa hii *link* kutoka chini, hatuna chombo kitakachompelekea mkulima mbolea kule chini. Mimi nataka niseme, tatizo linabakia pale pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina hakika ni kwa sababu zipi wametoa hii, lakini ni miongoni mwa vitu vilivyonifurahisha sana, kwa sababu hata nilipokuwa nazungumzia matatizo ya Wakulima na Waziri anafahamu; nikitoka kwa mkulima nilikuwa nakosa mtu wa kuongea naye pale Wilayani anayehusika na suala la mbolea. Sana sana nilikuwa naongea na *DC*, naye ana majukumu mengi. Kwa hiyo, *committee* hii nilikuwa nadhani ilikuwa na umuhimu mkubwa sana. Hebu tufikiri mara mbili na tuone pengine kama kuna umuhimu, lakini nadhani umuhimu upo tena mkubwa wa kuweka hiki chombo pale chini ili kiweze ku-*link* Wizara na wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kodi. Tutasema hapa yote haya, lakini kama bado mbolea itapigwa kodi kubwa, bado kodi ya *VAT* itapigwa kwenye mbolea na bado tutaamini hawa mawakala, watu binafsi kwamba, ndiyo watakaofikisha mbolea kwa wakulima. Mimi nasema tutakuwa bado hatujatatua tatizo. Ni vyema tukafikiri njia mbadala ya kutumia njia za kiutawala za *system* ya Serikali kwa ku-*link* na *government* tukamfikia mkulima kumpatia mbolea.

Si kama ambavyo tumeondoa hii *section number 6*, ambayo inaondoa kabisa ule muunganiko kati ya mkulima wa chini na Wizara katika suala hili la mbolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala zima la bodi; sina hakika kama sote kwa pamoja tunatambua umuhimu wa mtandao wa wakulima wadogo. Wakulima wadogo nchini wameweka mtandao, mimi nimeupenda sana na sijui kwa nini tunapata kigugumizi au kwa sababu pengine ni *Non Government Organization* na imeweza kufanya kazi nzuri na kuwaunganisha wakulima wote nchini? Haionekani mahali ambapo inaweza ikashirikishwa kwa ufasaha na pengine katika sheria hii, nilitegemea katika ile *district level* hawa wakulima wadogo wadogo ndipo wangeweza kushirikishwa kuweza kusema matatizo yao kama wakulima wadogo wadogo.

Tunawajua, tunaona kazi wanayofanya, lakini hatutaki ku- *appreciate* kazi wanayoifanya. Tunakwenda kwenye maeneo yao, lakini hatutaki kuridhika na kile wanachokifanya. Mimi ningedhani kwenye *District level*, kwa sheria hii na katika suala la mbolea ambayo ni pembejeo muhimu sana kwa mkulima, wangepata na wao *forum* yao, waweke mawazo yao na hivyo wangeweza kutoa msaada mkubwa katika suala zima la uwezeshaji wa mbolea kumfikia mkulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, maandalizi yangu yameharibiwa na *schedule of amendment* ndefu, ambayo hata nilipokaa hapa sikuweza kuimaliza, kwa sababu nimeiona muda huu, Nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na huo ndiyo ulikuwa mchango wangu. Ahsante sana, napenda kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru. Ungesoma zaidi ingekuwa tatizo, maana na muda umemaliza.

**MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kama mwenzangu alivyosema, pengine nikiri kwamba, nimekuwa *pre-empted* na *schedule of amendments.* Kwa niaba ya Wananchi wangu wa Jimbo la Kasulu Magharibi, naomba na nitoe salamu za rambirambi kwa Wananchi wa Busanda, kufuatia kifo cha aliyekuwa Mbunge wao mpendwa, Mheshimiwa Kabuzi, kilichotokea hivi karibuni. Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sasa niende kwenye hoja. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, kwa kuja na sheria hii. Mimi nilifanya utafiti na wataalamu fulani kutoka *university* moja Marekani, tukazunguka nchi nzima tukiangalia utaratibu mzima wa matumizi ya mbolea na uhaba wake katika mikoa mbalimbali ya nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, mbolea ilikuwa inaingia kiholela tofauti na ile iliyokuwa inaingia chini ya utaratibu wa kiserikali; iliyokuwa inatolewa na Serikali kwenda mikoa mbalimbali, ilionekana kwamba elimu haikuwa inatosheleza katika mikoa mbalimbali ambako watu walipokea mbolea hiyo. Tulipofika Mikoa ya Rukwa, Mbeya, Iringa na Ruvuma, tulikuta udongo mwingi sana umeharibiwa kwa sababu ya matumizi mabaya ya mbolea. Hii ina maana kwamba, kulikuwa na *intensive use of ammonia,* ambayo ilikuwa inaharibu *natural facility* ya udongo katika sehemu hizi, matokeo yake *yield per* eka katika sehemu hizi ilikuwa inaenda chini na ilikuwa inapungua mwaka hadi mwaka. Tulipoendelea, tukafika mikoa mingine, hasa ya pembezoni, tukakuta kwamba mbolea nyingi iliyokuwa inakwenda huko ilikuwa haiwafikii wakulima, hata pale kiasi kidogo kilipopelekwa huko.

Nitatoa mfano na Mkoa wa Kigoma; mbolea nyingi ilikuwa inapita pale mpakani lakini tulikuwa tunashangaa kwa sababu *agent* wetu wa mkoa alikuwa hana mbolea. Tunaiona mbolea inapita mpakani, wananchi wanalalamika hasa wa Vijiji vya Kalizi, Manyovu, Muigwe na Muyama. Wanaiona mbolea inapita katika tarafa hiyo, wao wenyewe wanaweza kutumia kwenye kilimo chao, ikawa inasikitisha sana maana

hatukujua ile mbolea ilikuwa inatoka wapi. Kwa hiyo, utaratibu mzima wa *distribution* ya *fertilizer* ndani ya nchi ulikuwa si mzuri. Watu walikuwa wanasafirisha mbolea wanavyotaka na wakati fulani watu wa Kasulu walikuwa wananunua mbolea hii inayotolewa na Serikali kutoka Kahama. Bei ya Kahama inapishana kidogo na ile ya kawaida. Hata unajiuliza kwamba hii mbolea inatolewa bila mpango; hakuna ufuatiliaji. Kasulu tulikuwa tunauziwa mbolea iliyokwenda Kahama, sasa sijui Kahama nayo ilikuwa *stocking point;* watu wanaileta pale kwa sababu bei ni kubwa watu wanainunua inasafiri tu popote pale.

Kwa hiyo, moja ya mambo ambayo ningependa kusisitiza sana katika hili ni lazima Serikali ijihusishe sana katika *distribution* ya *fertilizer*; pamoja na kwamba watajihusisha sana nimeona mahali panasema kwamba, Mheshimiwa Waziri atachagua *inspectors. Inspectors* ni watu wa kufanya *sampling* na ku-*analyze* mbolea itakayokuwa inaletwa nchini na inazalishwa nchini ili kuangalia ubora wake isije ikaharibu mazao kama wasemaji wengine walivyosema humu ndani. Jambo hili ni la msingi sana, kwa sababu ni lazima ufanye utafiti juu ya kila aina ya mbolea inayoingia ili uwasaidie wananchi kulingana na udongo wao. Inawezekana udongo wa Mbozi sio sawa na udongo wa Kigoma au Tunduma, lakini *distribution* ya mbolea *is almost uniform, we can afford this.* Mheshimiwa Waziri, ninakuomba sana utafiti utiliwe mkazo wa kuichambua hii mbolea na kujua inafaa vipi kama tulivyoangalia suala zima la *DNA. (Makofi)*

Mbolea inayokwenda Rukwa itakuwa tofauti na mbolea inayokwenda Mwanza au Tanga na lazima tuangalie pale ambapo inakwenda ku-*improve productivity*. Unaambiwa sehemu nyingine hivi sasa bila mbolea *it is impossible* kuzalisha. Sisi tulishuhudia *where intensive use of ammonia* imetumika bila mbolea, utajisumbua kupanda mbegu utaharibu. Najua zipo sehemu nyingi katika nchi hii na wakulima wa taifa hili wanafahamu kwamba, ipo mikoa michache hivi sasa iliyobaki. Mkoa wa Kigoma pamoja na kwamba tumekuwa tunatumia mbolea, lakini mbolea inayotumika ni kidogo sana kuliko inayotumia kwa nchi nzima. Kwa hiyo, bado watu wanaweza kupata kiasi kidogo kwa ekari ambayo analima mtu akasema si haba, lakini akitumia *fertilizer* atapata zaidi na *yield* itakwenda juu zaidi. Kwa hiyo, kama utafiti utafanywa ni dhahiri kwamba, wakulima wetu watazalisha vizuri zaidi na nchi itapata chakula cha kutosha.

Sasa nisemee juu ya uongozi; ni kweli kabisa tunampongeza Mheshimiwa Waziri juu ya utaratibu mzima ambao umefanywa, kupelekwa vyombo vya kufanya kazi kuanzia Taifa, Mkoani mpaka Wilayani. Naomba Wilayani msifute, jaribuni kubuni kitu kitakachosaidia ku-*improve monitoring* kwenye ngazi ya Wilaya. Kabla ya sheria hii, mambo haya ya *fertilizer* wakulima walipokuwa wananung’unika, wewe Mbunge unajaribu kulifuatilia hilo jambo hata kupiga simu kwa *DC* au kwa mtu mwingine naye anakuta sheria haipo mkononi mwake na hajui cha kufanya. Kwa hiyo, naomba kwenye ngazi ya Wilaya kuwepo na *monitoring unit,* itakayosaidia sana kuangalia matumizi ya mbolea hii na inatoka wapi ili *network* nzima ya *distribution* iweze kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Lingine ninalotaka kulisemea ni mahusiano ya hiki chombo kinachoundwa na vyombo vilivyopo hivi sasa, ikiwa ni pamoja na *Tanganyika Fertilizers Association*

*(TFA),* wamekuwa wanajitahidi sana kufanya kazi ya *distribution* ya mbolea nchi nzima na ndiyo walikuwa wanatumia *voucher*. Hizi *voucher* ambazo tunazizungumzia, *technically,* kwa kumpa mkulima anayetoka Mbozi au Songea kule Mbinga anakwenda Arusha kununua *fertilizer,* inamsumbua kweli kweli maana atafanya safari mara mbili au tatu. *It is unworkable;* hizo *voucher* zingeangaliwa sana na zifanyiwe uchambuzi mzuri kwani zimemfanya mkulima awe *inefficiency* hasa pale anaponunua *fertilizer* kutoka Makao Makuu ya TFA.

Pili, *role* ya *TFA* iwe *defined* katika mambo haya yote. Naomba Mheshimiwa Waziri, atufafanulie kwa sababu nilifikiri hilo ningeliangalia baadaye, maana nilidhani nitazungumza mchana sikujua kama nitazungumza asubuhi. Naomba Mheshimiwa Waziri anisaidie kulifafanua hilo. *Role* ya vyombo vilivyopo katika *distribution network* nzima ya *fertilizer* itakuwa nini?

*TFA* wamekuwa wanafanya hii kazi kwa muda mrefu sana, hatuwezi kusema kesho hawana kazi. Ninaamini Mheshimiwa Waziri ata-*define* hata vyombo vingine vile ambavyo vilikuwa vinafanya hii *distribution network* na wanayo maofisi mikoani. Nilikwenda Ruvuma nikakuta ofisi mbalimbali zinafanya *distribution*.

La tatu, ninaomba pia Mheshimiwa Waziri atusaidie *equal distribution* ya *chemicals* inayofanywa na mashirika mbalimbali, mengine yanatoka Kenya, ninaomba nayo yaangaliwe maana tunaweza kuzungumzia mbolea kwamba hii inaharibu udongo kumbe inaletwa ambayo si sahihi.

Wananchi wanaambiwa kwamba hii ni mbolea kadhaa, lakini wanakwenda kuitumia wanaona haitoi uzalishaji unaotakiwa na haikidhi matakwa ya mkulima. Tafadhali naomba hili nalo liangaliwe na Waziri atuambie hivi vyombo *role* yake itakuwaje, kama kutakuwa na udhibiti maalum wa *distribution* zinazotoka kama Kenya na sehemu nyingine maana zimekuwa zinaingia tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, ninaomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Wataalam wa Wizara hii, kwa kuja na hoja ya kuanzisha Muswada huu. Ninawapongeza sana kwa kazi hiyo na nyingine ambayo wanaifanya kwa niaba ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili kuweza kuchangia machache hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Tunazo dakika 10 tu za kuchangia na hakuna hata mtu mmoja anayetaka kujitolea kuzitumia dakika hizo. Kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja jioni.

*(Saa 6.50 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kufuatana na ratiba ya kazi zetu hoja hii inakwisha kesho. Kwa hiyo, haijawazuia wengine kama wanapenda kuomba kuzungumza. Kwa kuanzia nitamwita Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Malangalila na Mheshimiwa Profesa Mwalyosi. Nakwenda hivyo kwa sababu wengine sijawaona kufuatana na listi.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia na ninaomba pia niungane na Kamati kuonyesha masikitiko yetu kwa kifo cha Mheshimiwa Mbunge mwenzetu kilichotokea juzi juzi. Mungu aiweke roho yake mahali pema Peponi. Pili, nataka kumshukuru Mheshimiwa Stephen Wasira na wenzake kwa kuleta Muswada huu ambao kwa kweli tunaona ni Muswada muhimu sana na kwa hiyo tunaipongeza sana Wizara na Serikali kwa jumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na Muswada kwanza. Kifungu cha 38(i) kuanzia (a) mpaka ile (i) inataja kazi za Mainspekta watakaokagua maeneo au mahali ambapo bidhaa za aina hii ya mbolea zinaweza kuhifadhiwa na wamepewa madaraka ambayo sina tatizo nayo. Lakini hoja yangu ni kwamba tunataka tuelezwe pia ni watu wa aina gani hawa? Wana utaalamu gani ambao wanaweza kuaminiwa kusimamia? Kwa sababu jambo hili ni kubwa na ni *sensitive*, ni vizuri tujue kama ujuzi tunao na kama hatunao ni aina gani ya wataalamu ambao wataaminiwa kuweza kupewa jukumu hili la ukaguzi. Hilo ndio la kwanza kuhusu Muswada.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mambo mengine ya msingi ambayo nilikuwa nataka kushauri, naomba pia sheria hii iweke msingi ambao utasaidia biashara ya mbolea isiwe ni biashara ya kutajirisha watu. Kwa sababu mbolea ikitumika vizuri na ikiwa inapatikana kwa bei nafuu, kwa kuongeza chakula nchi itapata faida. Inafaa mbolea isije ikatazamwa kama vile watu wanavyouza chumvi au sukari.

Kwa maana hii nilikuwa nataka kusema kwamba kazi ya chombo hiki itakuwa na mafanikio makubwa zaidi kama watu wote wanao-*import* mbolea watahakikishwa kwamba hawaweki bei wanavyotaka wenyewe ili mbolea hii iweze kuwa na nafuu.

Pia ninashauri vilevile Serikali tuimarishe *TFC*. Hiki ni chombo cha nchi na kimesaidia sana kwa upande wa Mkoa wa Rukwa, watu walipata mbolea nyingi na kwa bei nafuu. Juzi juzi wakati naondoka Sumbawanga walikuwa wameshusha bei ya mbolea ya *CAN* mpaka Sh. 36,000/=, lakini wafanyabiashara binafsi hakuna aliyeshusha bei kwa sababu kila wakati wao wanatanguliza faida tu.

Mheshimiwa Nnaibu Spika, nchi yetu ni tajiri sana kwa rasilimali. Sisi tunashauri kwamba juhudi kubwa iwekwe katika kutumia gesi asilia kwa ajili ya kutengeneza

mbolea badala ya kutumia kwa ajili ya umeme. Tujitahidi umeme tutumie mkaa wa mawe ambao upo umeenea Tanzania, kule Mchuchuma, Kitawaka sasa kule Ruvuma, Mbeya, Mkoa wa Rukwa ili hii rasiliamali itumike kwa ajili ya kupata umeme na gesi itumike kutengeneza mbolea ambayo inaweza kutuwezesha sisi kuanza kujitegemea na kuuza nchi za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningependa niliseme ni kuhusu mbolea na ardhi. Kwanza kilimo ni sayansi na ardhi ya nchi ya Tanzania hata ukifika mahali unaweza ukakuta eneo labda la kilometa 10 au 20 kuna utofauti wa ardhi. Kwa hiyo, bado nilikuwa nataka kusisitiza kwamba kwa sababu nchi yetu inategemea kilimo, ingefaa tukubali kufanya gharama ya kujua ardhi ya nchi yetu na tujue ni aina gani ya mbolea inatakiwa kutumika kila mahali. Kwa sababu kuna mahali ambapo mbolea inatumika ambapo isingetumika mahali pale, inatumika mahala hapo. Kwa mfano, mimi mahali ninapolima sikujua kama mbolea ya kukuzia ni *CAN*, nilidhani mbolea ya kukuzia ni *UREA* tu. Lakini wenyeji wa pale ambao sio Mabwana Shamba wakasema ukiweka hapa *UREA* mahindi hutapata, weka *CAN*. Kwa hiyo, nataka kushauri kwamba tujue ardhi ya nchi yetu vizuri ili tushauri matumizi mazuri ya mbolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikwenda Australia. Australia wamepitisha sheria ya kuzuwia matumizi ya mbolea ya chumvi chumvi na badala yake kwa kuwa wako katikati ya *ocean* wanakwenda baharini wanaokoteza kwembelela zile ndizo wanatengeneza wanasaga mbolea. Sasa nataka kushauri hapa kwamba sisi wenye bahati ya kuwa na minjingu, tujitahidi tutumie minjingu iwe ndio mkombozi wa mbolea katika nchi yetu, kwa sababu ile haiharibu ardhi. Mimi nimetumia na mwaka huu wametoa aina mbili, walitoa ile ya unga pamoja na ile ya chumvi chumvi. Mwanzo ukiweka huwezi kuona mazao yako yakiota yanakwenda *speed* kama vile ungekuwa labda umetumia *DAP*, inachelewa kidogo. Lakini wale waliotumia ile ya chumvi chumvi ilionesha kutoa matokeo mara moja. *I mean* haichelewi sana. Kwa hiyo, nashauri suala la minjingu tusije tukarudi nyuma, tusonge mbele kwa matumizi ya minjingu kwa sababu haina uharibifu wa ardhi. Ukiweka sasa utaanza kuona matokeo mwaka kesho.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile najua ukizungumza mbolea unazungumza kilimo kikubwa sana, lakini mambo ya kitaalamu kwa wakulima wadogo wa heka tano au kumi tuwatie moyo watu kutumia samadi. Kuna Mikoa mingine ambayo watu wana ng’ombe wengi na wanatoa samadi lakini wanaichoma, hawaitumii kulimia. Kwa sababu maelezo yetu yote yametanguliza sana habari ya kutumia mbolea ya chumvi, mimi nadhani tusipuuze mbolea ya samadi. Zamani sisi tulipokuwa Darasa la Nne tulijifunza namna ya kutengeneza mbolea inaitwa *manure*. Kwa hiyo, mimi natoa wito kwa Serikali na sisi viongozi wote tuwatie moyo wananchi kutumia mbolea ambayo haina gharama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi mara nyingi huwa ninapotaka kusema kitu ninakisema halafu natoa na mfano. Mwaka jana mke wangu alilima hekta 10 akatumia samadi, amepata gunia 36 kwa hekta aliyotumia samadi. Kwa hiyo, mapato yamekuwa ni makubwa kwa kweli kuliko hata kama angetumia mbolea ya chumvi. Mwaka huu

nilivyokwenda kukagua na kuangalia shamba atafika gunia 42 kwa hekta. Baada ya mchango huo naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuchukua nafasi hii kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia katika Muswada wa Mbolea ambao ni Muswada muhimu sana. Binafsi sikuwa nimepanga kuchangia Muswada huu, lakini nilipokwenda kupata chakula cha mchana nimepigiwa simu zaidi ya tatu ambazo zimenilazimisha kuja kuchangia Muswada huu. Kwa ufupi napenda kuunga mkono Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda ningependa nianze na historia fupi ya matumizi ya mbolea katika nchi yetu. Ni kweli kwamba kabla ya mwaka 1960, nchi yetu ilikuwa haitumii mbolea za chumvi chumvi, ilikuwa inatumia samadi ambayo inatokana na kinyesi cha mifugo. Lakini katikati ya miaka ya 1960 ndipo mbolea ya chumvi chumvi ilipopendekezwa kutumiwa katika nchi yetu kwa lengo la kuongeza mazao ya chakula, hususan katika ile Mikoa mnne inayoitwa *big four*.

Nakumbuka siku zile za mwanzo mbolea hii ilikuwa inatolewa bure na kwa sababu ilikuwa ni mbolea ngeni, wengine walidhani ni chokaa na wakawa wanapakia kuta za nyumba zao. Lakini Baba wa Taifa alikemea tabia hii na hapo ndipo watu walipozinduka na kuanza kutumia mbolea ya chumvi chumvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba mara tu baada ya kuanza kutumika kwa mbolea hii ndipo ilipoibuika Mikoa minne ambayo inaitwa *big four* kwa maana ya Mkoa wa Iringa, Mbeya, Ruvuma na Rukwa. Kwa kweli Mikoa hii ilikuwa inazalisha mahindi mengi sana na maharage mengi sana. Nakumbuka katika kipindi hicho mbolea zilizokuwa zinatumika zilikuwa ni *TSP, NPK* na *CAN* na zilikuwa zinazalisha mahindi na maharage mengi sana.

Nakumbuka wakati huo Wakuu wa Mikoa minne walikutana, nadhani Mbeya, kujadiliana ni namna gani ya kutumia mahindi kwa sababu mahindi yalikuwa ni mengi sana, wakaamua mahindi yale wayatumie kuzalishia chakula cha mifugo. Miaka hiyo Tanzania tulifikia uamuzi wa kutumia mahindi kulishia mifugo. Kwa lugha rahisi ni kwamba Taifa hili lilishapiga hatua kubwa sana katika kujitegemea kwa chakula. Sasa ni kwanini tulirudi nyuma?

Mheshimiwa Naibu Spika, tulirudi nyuma kwa sababu ya shinikizo la mashirika ya kimataifa. Shirika la Fedha la Dunia na Benki ya Dunia, wakasema kwamba hatutakiwi kuweka ruzuku katika mbolea na katika pembejeo za wakulima, hilo ndilo kosa kubwa ambalo Serikali ya nchi hii ilifanya. Kutokea hapo, sasa ndio tukaanza kupata njaa, ile mikoa iliyokuwa inaitwa *big four* nayo ikaanza kupata njaa. Mimi niliwahi kuzungumza ndani ya Bunge hili kwamba tunajenga barabara nyingi sana kwenda huko vijijini, hasa kwenye ile Mikoa minne, hizi barabara zinakwenda kufanya nini huko wakati hakuna mazao ya kuchukua? Nikasema hakika hizi barabara badala ya kwenda kuchukua chakula zitakuwa zinakwenda kupeleka misaada ya chakula. Hili ni kosa kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali, miaka michache iliyopita imelitambua hili na imeanza kuweka ruzuku katika pembejeo, hususan mbolea. Naishukuru sana Serikali kuanzia mwaka 2008 wananchi wameanza kuishukuru kwamba angalau sasa mbolea inapatikana kwa wingi. Sasa ni kwanini tulifika huko? Ni kwa sababu wataalamu walikuwa wanafika vijijini na wataalamu walitufundisha kupanda mahindi kwa mstari na pia walitufundisha kupanda mahindi kwa nafasi. Lakini leo ukienda Iringa, Mbeya, Rukwa na Ruvuma, ni mkulima gani anayepanda mahindi kwa mstari na kwa nafasi? Nadhani ni wachache sana. Kwa hiyo, nadhani tuna tatizo la wataalamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika kipindi hicho bei ya mbolea na mbegu ilikuwa chini. Sasa hivi ukienda Mbeya, bei ya mbegu ya mahindi kwa kweli inatisha. Tunasema wakulima wetu ni masikini, ni dhahiri kwamba hawawezi kununua mbegu, hawawezi kununua mbolea wakapata faida. Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, alisema kwamba ile Mikoa minne iliyokuwa inaitwa *big four* sasa inaitwa *big fools*, yaani wajinga wanne. Kwa kweli maneno haya alipoyasema mimi binafsi nilijisikia vibaya sana kwa sababu mimi mwenyewe wakati huo nilikuwa nalima mahindi mengi sana, lakini nilikuwa napata shida sana ya soko. Maana mtu anakuja umuuzie gunia moja la mahindi, hilo gunia anajaza, ukienda kupima lile gunia la kilo 100 unaweza ukakuta hata kilo 150 na yeye anasema ni gunia moja. Kwa hiyo, kimsingi wakulima wetu katika nchi hii wananyonywa sana na wafanyabiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mbolea, Mheshimiwa Mzindakaya ameisifia sana minjingu, lakini amesema hii minjingu inaanza kutoa mazao mengi mwaka wa pili. Yaani ukitumia minjingu mwaka huu hupati mazao mazuri na mwaka wa pili ndipo unapoanza kupata mazao mazuri. Lakini nimshukuru sana Mheshimiwa Mzindakaya kwamba samadi ni mbolea ambayo ni nzuri sana kwa sababu inaweza hata kuzalisha gunia 36 kwa hekari. Kwa hiyo, kwa ufupi mimi ningependa kuwataka Watanzania watumie mbolea ya samadi na mboji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tazama hizi mbolea za chumvi chumvi, hapo mwanzo nilisema kwamba baba wa Taifa alitutaka tutumie mbolea shambani na wala tusitumie mbolea kupaka kwenye ukuta kama chokaa, alifanya jambo zuri. Lakini kwa kadiri miaka ilivyokuwa inakwenda hili shamba linalotumia mbolea ya kisasa ni dhahiri kwamba hatungetumia mbolea, lakini mazao yake yanazidi kupungua mwaka hadi mwaka kwa sababu ubora wa ardhi unapungua. Lakini ukitumia samadi, ukitumia mboji, shamba linaendelea kuwa bora mwaka hadi mwaka. Kwa hiyo, Watanzania na Waafrika kwa ujumla tutumie samadi. Hizi mbolea za chumvi chumvi tulidanganywa! Baada ya kudanganywa wakatupunguzia bei, hatuwezi kuzinunua, hatuwezi kuzimudu. Kwa hiyo, kama hatutumii samadi na mboji tutakufa, hakuna namna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli ningependa kutoa wito kwa dhati kabisa kwamba ni lazima tutumie mboji na samadi. Hii minjingu bwana watu wengine wanasema ni mawe tu yamesagwasagwa mengine mazito mazito mengine laini laini wanasema mbolea, wengine wanasema *Organic Matter (OM), it is not a chemical!* Kwa

hiyo, kimsingi minjingu sio mbolea ambayo inaweza kutusaidia katika kufufua kilimo cha Watanzania, mimi mwenyewe nina shamba langu mwaka huu nimelima hekari nne na nimetumia minjingu, nilipokwenda nilitaka kutoa machozi. Maana nimeona vihindi vimekuwa vyekundu, vidogo, havina afya, nikasema ni mbolea gani hii? Wananchi wangu kule Mufindi wanasema Serikali ifute leseni ya Kampuni inayozalisha minjingu hapa kwetu. Serikali iweke ruzuku katika *DAP*, mbolea ambayo Watanzania wameizowea halafu isimamie wataalamu wa kilimo wafike na isimamie wakulima watumie samadi, isimamie wataalamu tutengeneze mboji ili tuweze kuzalisha chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unajua wakati mwingine huwa ni aibu kila siku ukisoma gazeti, njaa! Wilaya fulani, njaa! Wilaya fulani njaa! Bunda nako nasikia iko njaa, sijui ni kweli! Sijui Mbunge wa Bunda ni nani? Sitaki kusema. *(Kicheko)*

Mheshimiwa naibu Spika, kwa dhati kabisa....

**NAIBU SPIKA:** Jamani, hutaki kusema kwani hajulikani? *(Kicheko)*

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula, ahakikishe kabisa anatoa waraka kwa Maafisa Kilimo wa Wilaya na Maafisa Kilimo wa Kata, kama wako Maafisa Kilimo wa Kijiji wawasimamie wananchi wazalishe mboji, watumie samadi katika kilimo.

Nina hakika tukifika hapo kama Baba wa Taifa alivyoelekeza, tutafika mahali nchi hii suala la njaa njaa kila kukicha litakuwa halipo kabisa na tutakuwa na uhuru. Maana nchi ambayo ina njaa ina uhuru gani jamani? Kila siku unakwenda kuomba Marekani, Wamarekani wenyewe wanasema hawana nafaka za kutosha, Taifa kubwa hawana nafaka za kutosha. Australia wenyewe walishafutilia mbali, hakuna ruhusa kutumia mbolea ya chumvi chumvi. Kwa nini? Sasa ni kwanini sisi tuendelee kuzungumzia mambo ya mbolea ya chumvi chumvi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia nataka kusema kwa dhati kabisa kwamba nchi hii ni lazima tuweke mkakati kabisa wa kuhakikisha kwamba tunakuwa na wataalamu vijijini wanaosimamia mboji. Mbona ni nyasi tu! Unachukua mbolea kidogo ya ng’ombe au hata ya sungura au hata ya kuku, unaweka juu unamwagilia miezi kadhaa na baadaye unakuja kuifumua pale, mbolea safi kabisa, unatoa mahindi safi kabisa, unatoa ngano safi kabisa. Hivi Mungu atupe nini jamani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani sikuwa nimemtakia mema ndugu yetu Faustin Kabuzi Rwilomba, kwa kifo chake. Basi naomba Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema Peponi. Amen.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE:** Kuhusu utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Kuhusu utaratibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 63(2). Sikupenda kumwingilia Mheshimiwa Mbunge ili mtiririko wa hotuba yake usighafilike. Alisema kwamba wakulima tunaowaheshimu sana kutoka Mikoa ile mashuhuri minne kwamba sasa ni *Big Fools,* sio *Big Four.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli lugha hii sio lugha nzuri. Sio kuwatendea haki wakulima hawa mashuhuri wanaoilisha nchi hii. Ningemwomba sana Mheshimiwa Malangalila, ni rafiki yangu sana na ninamheshimu sana, bila shaka tutaungana naye katika kuwapa haki na kuwaheshimu wakulima wa Mikoa ya *Big Four* na angeondoa hilo neno *Big Fools* katika *Hansard* yetu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, hata mimi natoka katika Mikoa hiyo. Nilivyomwelewa Mheshimiwa ni kwamba wakati zao la mahindi lilivyoshamiri, watu wanalima wanauza vizuri kabisa na walitajirika kweli! Walikuwa wanaitwa *Big Four.* Baada ya hali ya mabadiliko kutokea na soko huru kuwepo, mbolea kutopatikana, sisi hatuwezi kulima bila mbolea, kabisa hatuwezi! Ndio sababu ya maneno haya. Sio kwamba ameyasema haya ila yanazungumzwa hata huko. *(Makofi)*

Tunaendelea, Mheshimiwa Profesa Mwalyosi, atafuatiwa na Mheshimiwa Tatu Ntimizi.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa fursa hii. Kwanza napenda kuunga mkono hoja. Ninalazimika kuunga mkono hoja kwa sababu mimi natoka Mkoa wa Iringa, ni kati ya Mikoa hiyo inayozungumzwa na ndugu yangu hapa na Wilaya yangu tunalima sana mahindi na tunatumia mbolea ya chumvi chumvi. Kwa hiyo, sina budi kwa sababu hatuna ujanja, ni lazima tutumie mbolea hiyo kwa sababu ardhi ya Mkoa wa Iringa na hususan ya Wilaya ya Ludewa kwa sehemu kubwa imeharibika. Tumeiharibu sisi katika utaratibu ambao Naibu Spika alikuwa anauzungumzia kwa sababu ya matumizi ya mbolea ya chumvi chumvi. Wananchi wale wa Ludewa waliitikia wito wa matumizi ya mbolea na wakaharaibu ardhi ile na leo hawana namna ya kulima na kuzalisha mahindi bila ya kutumia mbolea hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaunga mkono kwa sababu ni kitu tunachohitaji kuendelea kukitumia mpaka tutakapopata mbadala wake. Lakini naunga mkono kwa masikitiko kwa sababu najua matumizi ya mbolea hizi pamoja na Muswada huu ni sehemu ya mkakati wa kilimo cha kijani, nadhani inaitwa *Green Revolution. Green Revolution* inahusu utumiaji wa mbolea za chumvi chumvi ambazo wote naamini tunajua kama nilivyosema, zinaharibu ardhi na ukishaharibu ardhi huna ujanja unabakia wewe ni mtumwa wa kutumia mbolea hizo kama walivyo wakulima wa Mikoa ya Nyanda za Juu, ni watumwa wa kutumia mbolea hizo mpaka mbadala wake upatikane.

Mheshimiwa naibu Spika, hata hivyo, nilipenda nichangie kwenye vipengele vikubwa viwili kwenye *part four* ambayo inazungumzia kuhusu kutengeneza uzalishaji, uagizaji, biashara ya matumizi ya mbolea, lakini *part five* vilevile ambayo inazungumzia kuhusu masuala ya *fertiliser inspection, sampling* na *analysis,* nilitaka nijikite kwenye maeneo hayo mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kusema kwamba uzoefu nilioupata hasa safari hii na mwaka jana katika matumizi ya mbolea kwenye Wilaya yangu, kwenye Kata zote nilizopitia, katika ziara zangu Kata za Mlangali Mawengi, Ludewa, Amani, Mundindi, Lugalawa na kadhalika kati ya kilio kikubwa ilikuwa ni kuchanganyikiwa wakulima kwa sababu: moja, kulikuwa na mbolea mbalimbali zililetwa, watu wameagiza mbolea, kuna *TFC* walileta mbolea, lakini watu wengine wameleta vilevile mbolea zao, yaelekea hakukuwa na usimamizi wa kutosha kuhusu uagizaji na mbolea zipi zipelekwe kwenye maeneo yapi. Tumeambiwa na wenzetu hapa kwamba maeneo hayafanani, kuna maeneo hata katika kilomita moja kutakuwa na mabadiliko makubwa sana ya hali ya udongo, kila eneo litahitaji mbolea kwa viwango vyake na mbolea aina na aina.

Inapotokea kwamba watu wanajiagizia mbolea, kila mtu analeta na kuuza, hii inakuwa ni ya biashara ya ovyo ni biashara ya fujo na kwa kweli matumizi ya mbolea katika Wilaya yangu, naamini sehemu nyingi za Mkoa wa Iringa imekuwa ni biashara na ni matumizi ya ovyo, haina utaratibu unaoeleweka na matokeo yake yamekuwa ni mengi ambayo ni pamoja na wananchi kutumia pengine mbolea ambazo hawatakiwi kuzitumia. Wanatumia kwenye maeneo ambayo hayahitaji mbolea hizo kama alivyokuwa anasema mzungumzaji aliyepita. Unaweza kweli ukatumia mbolea kwa mahali isipohitajika hiyo lakini tatizo kubwa ni kupunguza uzalishaji. Wananchi wanategemea wakitumia mbolea watazalisha zaidi, matokeo hawazalishi. Lakini kibaya zaidi unawaondolea matumaini, unawaongezea umaskini ambao wanaendelea kuupata badala ya kutegemea maisha bora wanaendelea kupata maisha duni. Hii ni bahati mbaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naamini Muswada huu umekuja kwa wakati wake na wakati tunaendelea kutumia mbolea hizi, basi tuwe na utaratibu unaoeleweka kwamba watu wanaogiza mbolea wanaeleweka wanao-*deal* na mbolea na kutuletea kwenye maeneo yetu wanaeleweka na wanatambulika na wana vyeti. Kwa kweli tunaweza tukawapeleka hata Mahakamani wakati ambapo hawatutendei haki. Kwa hiyo, namna moja au nyingine, nakubaliana na Muswada huu kwa sababu ni lazima tutumie mbolea hizi na kwa vile Muswada huu utatuletea utaratibu mzuri zaidi wa uagizaji, utaratibu mzuri zaidi wa matumizi na kusambaza mbolea katika maeneo yetu, natarajia utaratibu utakuwa bora kuliko ulivyokuwa mwaka huu pengine na miaka iliyopita.

Pili nizungumzie habari ya kutengeneza mbolea ya kwetu. Watu wamezungumzia habari ya mijingu, lakini nilitaka nizungumze uzoefu wetu wa kutengeneza tulioupata Tanga, *is a good lesson*. Juzi nilikuwa Tanga na nilidhania tatizo la kiwanda kile yalikwisha, lakini nilipouliza hali ikoje kuhusiana na maeneo ambayo kulikuwa kiwanda hicho kuna nini sasa hivi, maana yake tuliambiwa madawa yaliteketezwa, *chemicals* zile ziliteketezwa na naambiwa bado zipo ma-*chemical* yale yamewekwa kwenye visima, yamehifadhiwa, *is still time bomb may be* bado hatujajua tuyafanyaje, kwa hiyo, bado

tuko katika mazingira ya kukaa na kitu ambacho ni hali ya hatari kwa maisha yetu wananchi.

Sasa yawezekana tulipoleta viwanda vile na najua hapakuwa na *environmental assessment* kwenye kiwanda kile, matokeo yake tukakiweka kiwanda mahali ambapo hakitakiwi kiwepo. Hatukuwa na uhakika na utaratibu wa kupata *materials*, hatukuwa na uhakika wa *storage*, hatukuwa na uhakika wa usafirishaji, matokeo yake ni kufungwa kwa kiwanda na kutuleta matatizo namna ya kushughulikia *chemical* ambazo bado ziko kwenye *site* pale Tanga. Nadhani viwanda tutakavyovianzisha havitaingia kwenye mkumbo huo tena, naamini tutajitahidi kufanya *environmental assessment* na kuhakikisha kwamba tunajenga viwanda kwa utaratibu unaoeleweka na unaokuwa endelevu.

Lakini vilevile mimi nimefanya utafiti kwenye kilimo cha vinyungu kule Iringa, nikasikitika sana kuona jinsi wakulima wanaozalisha nyanya, vituguu na kadhalika. Kule Iringa kwenye vinyungu wanamwagilia wakitumia maji wanayoyachota kwenye vijito ambavyo vinapokea maji yanayotoka kwenye mashamba, kwa hiyo, wanachota huku chini wanamwagilia kwenye mimea kule juu yanapita kwenye udongo, yanarudi kwenye kijito kile wanachota tena wanayarudisha kule kule, matokeo ni kwamba wana *concentrate chemicals* hizi kwenye mimea hiyo wanaendelea kuharibu udongo kwenye mashamba yao kwa sababu wanaendelea kuongeza chumvi chumvi zaidi na zaidi katika maeneo ya mimea, matokeo yake, nyanya zile mara nyingi zinakataliwa.

Watu wa Zambia walitaka nyanya kutoka Ilula, walikuja wakapima wakasema hizi hatuwezi kununua kwa sababu ni sumu, lakini kwa sababu hakuna mtu anayeangalia matumizi ya mbolea hizi athari ya mbolea hizo kwenye udongo ili tuweze kurekebisha aina ya mbolea ya kutumia baada ya udongo kuharibika, tutumie mbolea ipi kwa viwango vipi, hakuna uperembaji wa athari ya mbolea hizi kwenye udongo, tunaendelea ku-*pump* tu mbolea kwenye udongo huu na kuharibu. Nadhani ni *very unfair* kwa wakulima wanaotumia mbolea hizi kana kwamba hatuna watu wanaoweza kusaidia, hakuna mabwana shamba wataalam wa kilimo, wataalam wanaosimamia mbolea kuhakikisha kwamba tunajua udongo umeharibika kiasi gani tu-*apply* mbolea aina gani kwa viwango gani ili kuwasaidia wakulima hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nategemea Muswada huu, kutakuwa na ufuatiliaji upembeleji wa matumizi ya mbolea mbalimbali kujua athari kwenye udongo katika maeneo mbalimbali *overtime* ili kujua mabadiliko gani yametokea kwenye udongo ili tujue ni mbolea za aina gani mpya au zile zile au kwa viwango gani tuendelee kutumia mbolea hizi kama hatuwezi kutumia mbolea ambazo ni *organic*. Lakini nafarijika kuona kwamba: Je, kutakuwa na sheria kali, tutaweza kuwashitaki, mamlaka hii itakayopewa majukumu haya tutaweza kuwashitaki endapo mbolea hizi zitakazoletwa zitaleta madhara kwenye maeneo na zitawaletea madhara wananchi wetu badala ya kuwapa nafuu. Kwa hiyo, tunapitisha huku tukijua ni hatari, kwa mamlaka hiyo inajipalia mkaa. Nataka niseme, kwa niaba ya wananchi wa Ludewa hatutawaonea mamlaka hayo watakaokuwa wanatuletea vitu ambavyo vinatuuwa. Kwa hiyo, naunga mkono hoja lakini nikiwa na matarajio hayo kwamba sasa kutakuwa na mabadiliko katika kilimo cha utumiaji wa mbolea hizi, kutakuwa na uperembaji wa kujua athari za matumizi ya mbolea hizi

kwenye udongo wa aina mbalimbali na ushauri utolewe kwa wakulima kila wakati namna ya kubadilisha mbolea katika maeneo yao ili yaweze kuleta tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja tena. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Wakati tunaanza kikao mchana huu nilisema huu Muswada unaendelea mpaka kesho. Kwa hiyo, nilisema nitamwita Mheshimiwa Tatu Ntimizi na Mheshimiwa Getrude Mongella ajiandae na atafuatiwa na Mheshimiwa Mwananzila.

**MHE. TATU M. NTIMIZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia Muswada huu. Kabla ya kuanza nitoe rambirambi kwa kaka yetu mpendwa aliyetutoka, Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema Peponi na awape faraja familia yake na wapiga kura wake wa jimbo alikokuwa ametoka. Amen.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono hoja hii ili Muswada huu upite. Lakini nina machache ya kuweza kutoa dukuduku langu nililonalo. Kwanza, kuleta Muswada huu wa kudhibiti na usimamizi na ubora wa mbolea kutakuwa kwa manufaa ya wachache. Katika jimbo langu la uchaguzi Igalula, mbolea hii zaidi inawasaidia wakulima wa Tumbaku, lakini wakulima wa vyakula vingine inakuwa ni ndoto kupata mbolea hii.

Nchi yetu hasa Mkoa wa Tabora karibu nusu imekuwa kame, haina rutuba, kwa hiyo, kuwekwa kwa mbolea kwa kweli kungesaidia sana wakulima wa mazao mengine. Lakini kwa kweli mbolea hii haifiki, imekataliwa kununuliwa na watu ambao sio wakulima wa Tumbaku. Lakini sasa baada ya zao la tumbaku kuanza kupungua, wakulima wengi walipoona soko limeanza kuwa chini wakachagua kulima mazao ya kawaida. Walikuwa wanahitaji sana mbolea hii, lakini wakashindwa kuwa wanapata kutokana na umbali ulivyo. Mkulima wa kawaida alishindwa kabisa na walipotaka kununua na kupelekewa maeneo wanakolima ilishindikana kutokana na umbali katika mji wa Tabora mpaka kufika kwenye jimbo letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jimbo langu ni la wakulima. Wanakijiji, hawana watu wenye biashara kubwa ya kusema waweze kununua mbolea halafu wawauzie katika maeneo yao, kwa hiyo tegemeo ni sehemu moja tu ya Tabora. Utoke Tabora mpaka mwisho wa jimbo langu ni karibu kilomita 200 na kitu na hasa wakati wa mvua mbolea hii haipelekwi kwa jinsi umbali wake ulivyo. Kwa hiyo, naona sijui wanaitazamaje katika majimbo ya vijiji ambako usafiri ni wa taabu halafu wananchi sio wenye pesa za kutosha kuweza kumudu gharama ya mfuko mmoja ambao kipindi kilichopita ilifika mpaka uliuzwa mpaka Sh. 60,000/= au Sh. 70,000/=. Sasa huyu mtu asafiri, ni juu yake na anakokwenda ni mbali na pesa ni nyingi, atafanikishaje ukulima bora unaotakiwa na kwa mazao aweze kujikimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutumia malighafi kutoka hapa nchini nafikiri ndiyo maana wakulima wengi wanaiponda mbolea ya mijingu, huenda malighafi za hapa nchini

sio bora japo na hakuna utafiti wa kutosha kupata hiyo malighafi mpaka kuwezesha minjingu ikatoa mbolea iliyo safi inayotakiwa katika mazao yetu. Nimekuwa na wasiwasi nayo, kwanza wengi wanaotumia minjingu wanasema haifai. Sasa huu utaalam tukipitia hii sheria, kweli watatembea kutafuta au kuonyesha sehemu ambayo malighafi ya kutengenezea mbolea hii iweze kuwa nzuri na watu wakaipenda badala ya kununua mbolea kutoka nje au kuboresha soko la kutoka nje ambako inakuwa ni gharama sana katika ununuzi wa mbolea hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, ukaguzi wa mbolea kufanyika na wakaguzi watakaohakiki ubora wa mbolea, sidhani kama itakuwa rahisi sana kufanya ukaguzi huu. Kuna mambo mengi wataalam ambayo hawayafanyi. Muswada huu utakuwa na changamoto gani kuwafanya hawa wakaguzi kweli wawe wanakagua mbolea, wasije wakawa wanakagua mbolea wakifika pale wakakuta wale waliohodhi mbolea au walioleta mbolea kutoka nje wakazungumza nao kwa sababu imekuwa ndiyo namna ya kuishi, bwana we pitisha hii mbolea yangu ni safi mambo yatajipa, matokeo yake anayeumia ni huyu mpokeaji ambaye ni mkulima ambaye tunamtegemea apate mazao mazuri lakini ukaguzi nao kuna wasiwasi kama kweli utafanyika kwa dhati kulingana na hii sheria ili kweli waweze kupata mbolea ya kutosha na ya kufaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu katika *clause* ya nane, *sub section* moja wanasema wataalam watashirikiana na wananchi kufanya kampeni ya elimu juu ya matumizi ya mbolea hii. Hili sidhani kama litafanyika, ikiwa sasa hivi tuna wataalam wa kilimo mpaka kijijini lakini kazi zao hazina ufanisi unaweza ukakuta katika vijiji miaka mitatu minne hakuna afisa wa kilimo aliyetembelea kuwashauri au kuwaelekeza namna ya ukulima bora au kutumia mbegu bora. Sasa hawa wataalam kweli, hizi kampeni, au tunataka kuongezea waende wakapate posho labda au waende katika semina hizo ambazo Mheshimiwa Waziri Mkuu kasema tusizifanye sana, una hakika kwamba hizi kweli zitatoa matunda? Mimi nina wasiwasi kabisa!

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya hawa wataalam kwenda kwenye kampeni, kwanza tusisitize kwamba hawa wataalam wa kilimo waliopo katika maeneo ya Kata, maeneo ya vijiji tufanye tathimini kuona kwamba kweli kazi yao wanaifanya kwa ufanisi, wananchi wanahangaikia mbegu, wao wenyewe ndio wanakuwa wataalam, wao wenyewe ndiyo wanakuwa wakulima, lakini sijapata kuona katika jimbo langu wataalam wakaenda kijiji kwa kijiji nikapata taarifa kama Mbunge kwamba kijiji hiki wamepita wataalam, wametushauri hivi, wameelekeza hivi! Sioni zaidi ya kuwa katika maofisi yao!

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri jambo la muhimu hapa, wangefanya tathimini kwanza kabla ya kampeni hii ambayo tunataka kuifanya, tufanye tathmini ya hawa Maafisa Kilimo walioko katika maeneo yetu waliokaa kwa muda mrefu. Niliwahi kuzungumza katika kipindi kilichopita kwamba wanaokaa miaka 10 na 15 katika kijiji, anakuwa *part and parcel* ya kijiji kile, hakuna jambo analolifanya zaidi ya kuzoeana tu na watu, lakini kusema kwamba afanye kazi hasa ya Afisa Kilimo, hakuna! Nafikiri wangejidhatiti sana katika kuwahamasisha na kuwakagua hawa Maafisa wa Kilimo katika kijiji kuona kama kweli kuna mfano wa kijiji katika maeneo yao wamefuata

ukulima bora kupata mbegu nzuri, wamepata pembejeo, wamepata mbolea ya kutosha, ili angalau ikawe mfano kwamba kweli hawa watu wanafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumezungumza mara nyingi humu, utaona kwamba akitaka kuhamishwa huyu Afisa Kilimo atakaa miaka mitano, miaka sita, katika kijiwe. Yeye ana kijiwe chake. Katika Mtaa, yeye pengine kaoa au kaolewa pale. Sasa kweli ufanisi wa kazi ya ukulima utaonekana? Hii kampeni sidhani kama itafanikiwa ikiwa kampeni ya kazi haifanyiki. Kampeni ya maneno ndiyo itafanikisha kuleta mazao yaliyo bora ili wakulima hawa wajikomboe katika chakula! Njaa katika jimbo langu la uchaguzi ipo. Robo tu ya jimbo labda watapata chakula, lakini sehemu nyingine zote hata waliojidhatiti kutafuta mbolea, mvua nyingi iliponyesha mbolea yote ikaenda na maji, matokeo yake ikabaki mimea imesimama haina mbegu, haina chochote mpaka sasa, lakini sikuona wataalam wakifika kutoa ushauri wowote, hata hawakufika na kama wamefika labda kijiji kimoja, lakini katika vijiji tulivyonavyo vingi sidhani kama mtendaji wa kijiji au wa kata kuhusu kilimo amefika kutoa ushauri mwingine. Sasa nasema pamoja na kuiweka hii kampeni katika sheria hii, lakini kwanza utekelezaji wa wale ambao mmefanya tathimini Wizara ina habari, Halmashauri ina habari, au Serikali yote ina habari kwamba hawa utendaji wao wa kazi hauna ufanisi zaidi!

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba tuwatazame sana hawa wataalam na kama hawako ma kampens kwa ajili ya kutumia mbolea, basi hawa watendaji wa vijiji waondoke kwa sababu hatujaona manufaa zaidi ya wao kuwepo katika ofisi. Kwa hiyo, nasema kwamba tukifanikisha ofisi za watendaji hawa wa kilimo katika vijiji na katika kata wakafanya kazi zao zilivyoainishwa katika ratiba zao mimi nafikiri hata hii kampeni inaweza ikafanikiwa. Lakini tusifanye kampeni ya zimamoto watu kwenda kutembea katika maeneo lakini pasiwe na matunda kwa wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ushauri nilioutoa uzingatiwe kabla hatujaanza kufanyia kazi sheria hii. Baada ya hayo, naunga mkono hoja hii na kama mlivyosema nashukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MHE. BALOZI DR. GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie hoja hii iliyo mbele yetu inayohusiana na mbolea. Kabla sijaendelea, napenda niungane na wale wote ambao wametoa rambirambi kwa familia na wananchi wa jimbo la Busanda kwa kumpoteza ndugu yetu Mheshimiwa Kabuzi. Sisi tunaotoka Mkoa wa Mwanza tumepata pigo kubwa kwa sababu alikuwa miongoni mwetu mtu hodari sana katika kujenga hoja, alikuwa mkweli, muwazi, mwenye upendo wa hali ya juu kwa kila mtu. Kwa hiyo, tunajisikia wapweke kabisa kumkosa mwenzetu miongoni mwetu. Mungu atampa pumziko la milele. Amen.

Ndugu zangu, baada ya kusema hayo nina haya yafuatayo kuchangia, kwanza kabisa nataka nitumie nafasi hii kusema kwamba Wilaya ya Ukerewe tuna njaa kwa mara ya kwanza tangu dunia iumbwe. Hii imetokana na ugonjwa wa mihogo ambayo imeathiri zao hili la muhogo ambalo ndiyo zao muhimu. Natumai Mheshimiwa Waziri anayo taarifa kwamba kuna wakati tulikuwa tunahangaika hata tupate mbegu mbadala kwa ajili ya kunusuru maisha ya wananchi hao. Natumaini ninapounga mkono hoja hii na yeye

atafikiri sana kuhakikisha ya kwamba Wilaya hii ambayo hata siku moja hatujawahi kuwa na njaa wananchi wake wanapewa nafasi ya kupewa chakula kama inavyostahili. Hicho kilicholetwa cha kugawiwa kila mtu kibakuli kimoja kinatuletea tu ugomvi wa viongozi na wale wanaogawa hicho chakula.

Kwa hiyo, hilo nalitoa ni ombi rasmi kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Ukerewe ambao ni wakulima hodari sana na ninataka nianze kutoa mfano wa wakulima wa Wilaya ya Ukerewe hasa kisiwa cha Ukara; ukitazama katika *journals* za ulimwengu kisiwa hiki cha Ukara kimeandikwa sana na kuwekwa katika majarida ya kisayansi katika matumizi ya mbolea ya samadi na mboji na wale wote wanaosoma kwenye vyuo vikuu sio hapa nchini, unapzungumzia matumizi ya mbolea ambayo ni ya siri Ukara ambayo ni moja ya Kisiwa cha Ukerewe inachukua nafasi ya kwanza.

Napendekeza kwa Mheshimiwa Waziri kwamba basi aliweke maanani sana suala la matumizi ya mbolea na hasa mbolea asili kwa sababu inaleta urutubishaji wa ardhi ambao hauchujuki na nadhani Ukara haijatangazwa sana kwa sababu kila siku lile ambalo ni letu wenyewe tunalipuuza, tunachukua yale ambayo yanatoka nje kwa kasi zaidi. Hizi mbolea za *chemically*, zimetoka nje ya nchi, kwa hiyo, ni rahisi kuzielewa kuliko zile ambazo ni zetu. Nataka nitoe mfano mwingine. Katika Mkoa wa Ruvuma wakati ule waliendelea wakawa *the big one!* Naomba niwapongeze. *(Makofi)*

Pamoja na kutumia mbolea za *chemically,* wakulima wa Ruvuma walianza kutumia mimea ambayo inarutubisha ardhi marejea na ilikuwa mbolea ambayo inasaidia sana katika kukuza mimea.

Naomba nikumbushie kwamba tunapoileta hii sheria, tuweke na kipengele cha kutambua aina nyingine za mbolea ambazo zinaweza kutumika na zenyewe ziwekewe mikakati, kwa sababu unapotumia mimea kwa mimea mingine, ni vizuri pia *research* kuona kama kuna athari zinazotokea kulingana na uchafuzi wa mazingira, lakina marejea yamejaribiwa katika Mkoa wa Ruvuma na yakafanya kazi na nadhani aina hiyo ya mbolea inaweza kutolewa. Wengine hapa wamezungumzia mifano mingine mingi tu ambayo ipo, ukienda kisiwa cha Ukara zamani, ukaenda choo kwenye shamba la mtu mwingine ambako huli, watakwambia kale huko huko ulikopelekea mbolea. Lakini nataka niendelee kusisitiza kwamba kama tungetilia mkazo suala hili la mbolea ya asili lingekuwa na umuhimu wake wa pekee. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa niliweke suala la mbolea katika mantiki ya uchumi wa dunia uliovurugika. Nasikitika kuona kwamba sisi Waheshimiwa Wabunge hatujalizungumza suala hili, huenda likawekwa kwenye agenda wakati muafaka ili tuangalie jinsi uchumi wa dunia ulivyovurugika. Ulivurugika kwa sababu ya watu wachache wenye tamaa hasa nchi zilizoendelea kama Marekani na nchi za Ulaya. Walicheza mchezo wa mabenki na wamefika mahali wakaingia hasara kubwa ambayo sasa na sisi inaanza kutuletea madhara.

Tunazungumza juu ya mbolea wakati uchumi umevurugika kwa kipindi kikubwa na mengine mengi nitayaweka tutakapopata nafasi labda kujadili suala hili peke yake kwa

undani kuona madhara yatakayotufikia.  Katika Mikoa mingine tumeshaanza kuona athari. Kwa mfano, katika Mkoa wa Mwanza tunakolima pamba, pamba inaanza kukosa soko na haya masuala ni ya muhimu kuyazungumza. Mbolea tutapata, lakini kama hatutauza pamba, mkulima hawezi hata kurudisha zile pesa za kununulia mbolea.

Lakini kubwa sasa katika kuweka mikakati na hasa sisi nchi tunazoendelea, la muhimu sasa hivi ni kuhangaika na chakula, tuhangaike na uzalishaji wa chakula ili angalau tuweze kula hata kama hatutaweza kuuza na haya mambo yanaendelea, sisi tunaotoka sehemu za madini kuna hata sehemu nyingine za machimbo zimeanza kusimama kazi.  Haya yote ni madhara ambayo hatujayaangalia na tungekwenda kwa undani tungeona zaidi.  Kwa hiyo, kilichobaki, matumaini yetu katika Muswada huu ni kuangalia ni jinsi gani na mbolea zipi zitakazotumika katika kuzalisha chakula kuliko tupate yote mawili uchumi uvurugike, mauzo nje ya nchi yasiwepo na watu wawe na njaa na tusiwe na uzalishaji imara kuhusu chakula.

Nimesema hasa uzalishaji wa chakula kwa sababu unapokuja kwenye mbolea za *chemically*, imeshatambulika kisayansi ya kwamba mazao yana tabia ya kunyonya *chemically* zilizoko kwenye mbolea na kuzihifadhi aidha katika matawi, katika majani na katika mizizi na binadamu anapokula mazao ya aina hiyo anaweza akadhurika. Hizi *research* zimekamilika.

Kwa hiyo, kwa sheria hii, matumaini yangu ni kwamba kazi kubwa itakayofanyika ni ya kudhibiti mbolea zitakazoletwa wakati tunahangaika kulinusuru taifa hili na chakula zisiwe ni zile mbolea za *chemically* ambazo zitamdhuru binadamu. *(Makofi)*

Kwa mfano, ukitumia mbolea yenye *chemically* yenye *red* ndani yake na mama akaila ile ina tabia ya *red* ile kuingia katika kizazi cha mwanamke na watoto wanaobeba ile *red* katika miili ni watoto wa kiume na huu ni utafiti umefanyika. Kwa hiyo, kuna tafiti nyingi tu zimeonyesha matumizi ya mbolea yanavyoweza kuwa na faida na yanavyokuwa na hasara.

Kwa hiyo, kile kipengele cha kudhibiti matumizi ya mbolea hasa katika uzalishaji wa chakula, mboga, matunda na vitu vingine ni lazima uzingatiwe na ndiyo maana duniani sasa hivi kuna kampeni ya kuhakikisha ya kwamba chakula ambacho hakikuzalishwa kwa mbolea kinauzwa kwa bei kubwa kuliko chakula ambacho kimezalishwa kwa mbolea ya *chemically*. Hilo nalo lazima tuliweke mbele ili tusije tukafika mahali tukakosa mahali pa kuuza chakula chetu kwa sababu tumetumia mbolea za *chemically* katika kuzalisha chakula ambacho sasa hivi tungeweza kukifanya zao la biashara na pia tukatumia kama chakula kwa matumizi yetu. Kwa hiyo, nashukuru kwamba sheria hii imeletwa ili  iweze kutekeleza hayo yote ya kulinda chakula chetu, kuhakikisha kemikali zinazoletwa haziwezi kudhuru miili ya binadamu.

Ningependa pia niongeze kwamba katika mbolea hizi suala kubwa la kuzingatia ni suala la uchafuzi wa mazingira, iwe ni sehemu kubwa sana ya kuzingatia kwa wale watakaokuwa wanasimamia matumizi ya mbolea na wanasayansi wetu wapate nafasi

kubwa zaidi ya kupima matokeo yake, isiwe ikishapitishwa mara moja, basi inatosha kusema hii inatosha. Tuchukue mfano wa Malaria. Malaria sasa hivi tumekuwa tukibadilisha dawa hii na ile kwa sababu kuna utafiti ambao unaendelea wakati wote, kwa hiyo, kuwepo na utafiti wa kuhakikisha ya kwamba zile mbolea zinazoingia nchini, aina zote ziwe ni mbolea ambazo zimefuatiliwa kwa wakati wote baada ya kuwa imekubalika kutumika katika nchi.

Lingine ambalo ni uchafuzi wa mazingira, kwa mfano katika upande wa ukanda ule wa ziwa, inapokuwa mbolea nyingine zimetumika katika ardhi ya pamba, mbolea hizo kemikali zake zinapelekwa mpaka ziwani na kwenye mito na hilo nalo ni lazima liwe na ufuatiliaji wa kudumu. Bodi inaweza ikasimia kwa wakati mmoja, lakini kama hakutakuwa na ufuatiliaji wa kisayansi wa kila wakati hatutajua ni kiasi gani cha kemikali zimeshaingia katika maji ya maziwa ama maji ya visima na maji ya mito na ndiyo maana dunia ya leo yanaibuka magonjwa ya kila aina kwa sababu mengine yanatokana na matumizi mabaya ya kemikali.

Nimetoa maangalizo haya sio kwa sababu nataka kupinga Muswada, isipokuwa kwa sababu nataka uwepo umakini katika sheria hii kuonyesha kwamba hizi mbolea ambazo siyo za asili zinaleta madhara gani na namna gani ya kujikinga na haya madhara. Lakini pia, ningependa kiongezwe kipengele cha kulinda matumizi ya mbolea kama mboji na samadi na mfano mzuri ni katika kisiwa cha Ukara Wilaya ya Ukerewe na Waziri anakaribishwa sana na watalaamu wake kuja kupata mafunzo kutoka katika kisiwa hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nichukue nafasi ya kipekee kushukuru sana kupata nafasi hii ya kuchangia huu Muswada wa mbolea. Ilikuwa nisichangie kutokana na hali ilivyo, lakini suala la mbolea katika jimbo langu katika Wilaya ya Njombe katika Mkoa wa Iringa ni kitu cha muhimu sana, nisipochangia nitaonekana ni mtu wa ajabu sana.

Kwa hiyo, Muswada huu kwanza umechelewa lakini hatusemi umechelewa sana ila wananchi toka muda mrefu sana wamenyonywa kwa kutokuwa na Mamlaka inayodhibiti suala la uagizaji, utengenezaji, usambazaji na utumiaji wa mbolea.

Lakini kabla sijatoa hoja zangu hasa, nami niungane na Watanzania wote kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Njombe Magharibi kutoa pole kwa ndugu zetu wa Jimbo la Busanda kule Geita kutokana na kifo cha ndugu yetu Mheshimiwa Kabuzi Faustine Rwilomba kufariki dunia. Kwa kweli imetusikitisha sana na tunaomba tuwape pole sana.

Labda niendelee na hizi hoja zangu za uchangiaji kwenye upande wa hii Mamlaka ya udhibiti wa mbolea. Labda nizungumzie kuhusu hili suala la vocha. Sasa hivi kuna hii elimu ya vocha kwamba kuna mbolea ya ruzuku, wananchi kule kwangu, ile mbolea imekuwa ni tatizo sana kwamba imefika kwa kiasi kidogo sana. Sasa najaribu kuangalia

hii sheria kama inaweza ikatusaidia wale wananchi wasiteseke kwa mbolea kutokufika kwa wakati unaotakiwa na inakuwa ni kidogo, nafikiri hili ni suala la msingi sana kuangalia kwamba hii Mamlaka isiwe ipo kama pambo, iwe na nguvu, uwezo wa kudhibiti kwa kweli taratibu zote za uagizaji, usambazaji na utumiaji wa mbolea.

Lingine ambalo ningependa kutoa ushauri kwa hii Mamlaka au kwa Mheshimiwa Waziri anayehusika kwamba hii vocha ni mtindo mzuri sana lakini bahati mbaya ni kwamba elimu haikufika ya kutosha, kwa hiyo ningeshauri kitu kama vocha ilikuwa ni kizuri sana na ni mkombozi mkubwa. Kwa hiyo, ni vizuri sana suala la vocha litiliwe maanani na elimu iwe ya kutosha.

Lakini kwa haraka niende kwenye upande wa bei za mbolea. Pale Makambako mbolea zimelundikana, zipo tani karibu 14,728 lakini ukiuliza zile mbolea zimejazana pale wananchi wanashindwa kuzinunua ziko za aina mbalimbali iko *Can, Urea, DAP, SA* na minjingu. Mbolea zile zimekosa soko, bei imekuwa ni kubwa na sasa nilikuwa nataka nitoe ushauri tu kwamba tunapoagiza mbolea ni vizuri tungeweka hata badala ya kilo 50 tuweke vipaketi vidogo vidogo hata vya kilo 20 au 10 ili wananchi ambao wana uwezo mdogo wawe wanaweza kununua hata ya kilo 10 kuliko ilivyo sasa hivi ni kilo 50. Sasa kilo 50 kwa mfano mfuko wa *DAP* ni kati ya Sh. 95,000/= mpaka Sh.100,000/=. Sasa Sh.100,000/= kwa mwananchi wa kawaida huyu anayetumia jembe la mkono maana yake umemuumiza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, data ninazo. Hapa nchini wakulima wetu ni 70% wanatumia jembe la mkono, 20% wanatumia wanyamakazi na 10% tu wanatumia matrekta. Sasa huyu mkulima anayetumia jembe la mkono unasema anunue mfuko mmoja wa Sh.100,000/= kwa kweli unamtwisha mzigo mzito sana. Lakini angalau tungeweka kiasi kidogo kidogo watu wangeweza ku-*afford*. Kwa hiyo, ninashauri pamoja na kung’ang’ania kwamba tuweke kilo 50 ni vizuri tuweke hata kilo 10 au kilo 20 ili wananchi wa kawaida hawa 70% waweze kununua hii mbolea.

Lingine, wenzangu walikuwa wanailalamikia hii mbolea ya minjingu na mimi kule kwangu tuna kilio hicho hicho kuhusiana na hii mbolea ya Minjingu, hawaihitaji kabisa! Siyo nzuri, kwa hiyo, haijawasaidia wakulima. Kwa hiyo, nilichokuwa nafikiria ni kwamba pamoja na kwamba Serikali inahangaika kuhusu suala la Minjingu, tuangalie njia mbadala. Njia mbadala niliyokuwa nashauri ni kutumia mbolea hizi za mboji, yaani *organic fertilizers*.

Mheshimiwa Waziri siku moja alisema *organic fertilizers* hapa nchini haipo, lakini mimi nina makaratasi hapa, mbolea hii mimi nimeiona, iko pale Chang’ombe, ni nyingi tu matani kwa matani. Tatizo ni kwamba Wizara inatakiwa isaidiane na yule *supplier* ambaye anaitwa *Tigi International Limited* isaidie kusambaza ile mbolea na kuiuza, kwa sababu bei yake ni nafuu, halafu ni rafiki wa mazingira, haiharibu ardhi kama hii mbolea ya chumvi chumvi. Wasije wakanielewa vibaya hawa wanaoagiza mbolea ya chumvi chumvi, lakini hii mbolea kwa kweli nayo ilitakiwa ipewe umuhimu wa kipekee na ikiwezekana ipewe hata ruzuku kama zilizopewa ruzuku mbolea nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninashauri kwamba *organic fertilizers* ambayo inatoka Marekani, Serikali ingetilia maanani kuona kwamba ina umuhimu wa kipekee kama zilivyo muhimu hizi mbolea za chumvi chumvi ambazo ni *inorganic*, lakini hii ni nzuri zaidi kwa sababu haiharibu mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wazo lingine ambalo nilikuwa nashauri kwa wenzangu wa Wizara ni kwamba maadam mwekezaji ameshajitolea anataka kujenga kiwanda pale Njombe tena Jimboni kwangu pale katika kijiji cha Ikingula au Mung'elenge Wilaya ya Njombe, nilikuwa tushirikiane na tusaidiane kile kiwanda tukijenga na kile kiwanda kinakuwa ni kikubwa katika Afrika, ingeweza kusambaza katika nchi za jirani kama Malawi, Zambia hata *South Africa*, tungekuwa *supplier* wa mbolea kwa sababu fedha ni zake, mtu anataka kuwekeza na kiwanja tumeshatoa, sasa *problem* inaonekana anazungushwa yule mtu.

Kwa hiyo, nashauri kwamba pamoja na Mamlaka hii kuundwa, isaidiane na mimi kwani ninamfahamu vizuri yule mwekezaji Mmarekani, angeweza kutusaidia hili tatizo la mbolea na lingepungua sana. Kwa hiyo, nilitaka kushauri kwamba mbolea hii ingeweza ikawa mkombozi sana kuliko kuagiza mabilioni ya fedha, tunaagiza nje badala ya kusaidiana na huyu mwekezaji tungejenga kiwanda hapa hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nilitaka nizungumzie ni kuhusu suala la upungufu wa mbolea. Jimboni kwangu wakati natembelea hivi karibuni kuna kijiji kinaitwa Lyamluki kiko katika Tarafa ya Wanging'ombe – Njombe. Kijiji kile kina tatizo la njaa. Ni njaa kabisa, kwani mvua imenyesha kidogo na mbolea ilifika kwa taabu sana, kwa hiyo, nilikuwa nafikiria wahusika tunaomba mtusaidie, kile kijiji wananchi wangu pale wamelima kidogo, mvua haikunyesha kwa hiyo kuna njaa pale. Pamoja na kwamba kuna vijiji vingine katika Kata ya Saja, lakini tatizo kubwa liko pale katika kijiji hicho cha Lyamluki.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nizungumzie kuhusu suala lingine la mbolea. Sisi ambao tunatumia mbolea hasa upande wa viazi mviringo pamoja na kwamba mnasema mmeleta hii mbolea ya ruzuku kwa ajili ya viazi, tunaomba ije kwa wakati unaotakiwa kuanzia mwezi wa nane au wa tisa, ingetusaidia sana kulima viazi mviringo pamoja na mahindi kwa sababu sisi tunalima mara mbili. Kwa hiyo, wananchi wa vijiji kama vya Igosi wanavyonisikia hivi, vijiji vya Imalinyi na vijiji mbalimbali ambavyo ni vya Mdandu wangejisikia vizuri sana kama mbolea ingewahi sana pamoja na kwamba tunasema mbolea inatakiwa ije mwezi Desemba, lakini inachelewa, inakuja mpaka mwezi Januari au Februari. Sasa inapokuja inakuwa ni *useless*.

Kwa hiyo, tunaomba ile mbolea kwa sisi na sehemu nyingine ambao wanalima viazi katika Wilaya ya Njombe muwahishe mwezi wa Agosti na Septemba ili mbolea ifike kwa sababu sisi tunalima mara mbili; tunalima hivyo viazi mviringo na tunalima vilevile mahindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu nataka niache na wenzangu wachangie, nashukuru sana na kwamba naunga mkono hoja hii na ni hoja nzuri sana. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Muswada ambao uko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa salamu za pole kwa msiba uliotupata wa ndugu yetu Mheshimiwa Faustine Kabuzi Rwilomba na tunawapa pole familia yote pamoja na ndugu, jamaa na wananchi wote wa jimbo la Busanda. Mwenyezi Mungu awape moyo wa uvumilivu na ustahimilivu. Amen.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Watendaji wake wote kwa kuandaa Muswada huu na kuuleta hapa Bungeni ambao ni matumaini yetu kama utasimamiwa kikamilifu, pengine utajibu maswali ya wakulima wa Tanzania ambao wamekuwa wanauliza kwa muda mrefu bila kupata majibu ya kueleweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania zaidi ya 80% ambao wanategemea kilimo kwa muda mrefu wamekuwa wanalima bila tija kwa sababu Serikali imeshindwa kuweka mipango mizuri ya upatikanaji wa mbolea kwa wakati na kwa muda unaotakiwa na kwa bei inayoweza kununulika. Serikali pia imekuwa inatoa ruzuku kwa muda mrefu na ruzuku hiyo imekuwa inatolewa na Serikali kwa utaratibu ambao haumnufaishi mkulima. Kwa hiyo, mbolea inayotolewa imekuwa haimnufaishi mkulima na matokeo yake wanaonufaika ni wafanyabiashara na wafanyabiashara wamekuwa wanatumia fursa hii kwa kujinufaisha na kujineemesha bila kuwa na huruma kwamba mkulima anahitaji alime ili aweze kujiinua kutokana na hali ya kipato cha chini na pia kuongeza uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na utaratibu mwingine ambao Serikali imeleta sasa hivi wa kutoa ruzuku kwa kutumia vocha, bado kumeonekana kuna matatizo. Kwa hiyo, inaonekana pia Serikali haijakaa chini na kuja na mipango na mikakati mizuri ambayo inaweza kutoa suluhisho la kudumu. Mpango wa kutumia vocha bado umekuwa ni tatizo kwa sababu wakulima wanapata ruzuku hii ya mbolea na mbegu kwa wakati ambao msimu umepita. Licha ya hivyo, jinsi ya kufuata hivyo ruzuku mpaka ukapata hiyo mbolea, ni mbali, wakulima kwa hali ya maisha duni waliyonayo hawawezi kumudu gharama za kufika huko, kwa hiyo, matokeo yake unakuta pamoja na utaratibu kubadilishwa bado mkulima hajaweza kunufaika vizuri na ruzuku hii inayotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninatumaini kabisa kwamba angalau kwa Muswada huu sasa Serikali iandae kanuni ambayo itatoa mwongozo kamili jinsi gani mbolea iende moja kwa moja kwa mhusika, jinsi gani mkulima anufaike na mbolea hii, vinginevyo, bado suala la kuboresha kilimo litakuwa ni tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukienda kwenye suala la ubora wa mbolea, ningependa kujua ni nani anayedhibiti ubora wa mbolea hapa nchini? Tuna *TBS*, Mamlaka ya Chakula, Kambi ya Upinzani wamesema kuna Mkemia Mkuu, ni nani anayedhibiti suala la mbolea? Ni kwa nini mbolea inakwenda mpaka kwa wakulima matokeo yake wakulima wanaunguziwa mahindi na nafaka zao zikiwa mashambani? Ni kwa nini mbolea inakwenda mashambani badala ya kurutubisha ardhi inaharibu ardhi na badala ya kumsaidia mkulima imekuwa ni kumletea hasara? Mbolea zinaharibu ardhi pamoja na mazao yanayotolimwa mashambani. Kwa hiyo, tungependa Serikali ituambie kwamba nani hasa anatakiwa kudhibiti kabla mbolea haijafika kwa mtumiaji, hapa katikati ni nani anayehakikisha kwamba mbolea hii iko kwenye viwango vinavyotakiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuendelea kuleta taratibu za jinsi ya kusambaza mbolea ambapo ndiyo hasa Muswada huu unalenga, ningependa pia kujua Serikali ina utaratibu wa kufanya uchunguzi? Tafiti mbalimbali zinafanyika kwa muda gani kuweza kujua kwamba mbolea hii inafaa maeneo gani na wakati gani? Kwa sababu siyo suala la kusambaza mbolea tu, wakati gani na mahali gani? Tuna vituo vingi sana ambavyo tunaweza kufanya *research* kama *Sokoine University* ambayo ina maabara nzuri sana ya udongo, wanaangalia na Serikali inapeleka udongo pale ili kuhakikisha kwamba mbolea hii inafaa kwa udongo huu Tuna wataalamu wa aina mbalimbali wa udongo, kilimo, na kadhalika tunawatumiaje watu hawa kuweza kusaidia kufanya utafiti wa uhakika kuona kwamba mbolea inamnufaisha mkulima?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu sana Serikali iangalie suala la utafiti kwa umakini mkubwa sana, kabla ya kutengeneza mbolea kwanza iwe na uhakika kwamba mbolea hii inayotengenezwa hapa inatumika wapi? Tunao wataalamu, vituo vyetu na hata *University* Serikali ivitumie kuhakikisha kwamba tunaweza kutoa mboleaili tuwasaidie Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye Mkoa wangu wa Tabora. Mkoa wa Tabora umekuwa na wakulima wazuri wa zao la Tumbaku. Zao hili la Tumbaku limekuwa linaiingizia Taifa hili fedha nzuri sana za kigeni na Serikali itakubaliana na mimi kuhusiana na hili. Ardhi ya mkoa wa Tabora imechoka kwa sababu imetumia mbolea kwa muda wote, kwa hiyo mkulima kama hajatumia mbolea hawezi kabisa kuvuna chochote, lakini jambo la ajabu ni kwamba, pamoja na wakulima hawa wa Mkoa wa Tabora kuendelea kuchangia pato kubwa kwa Taifa, Serikali haijaonyesha nia yoyote ya kuwasaidia katika upatikanaji wa mbolea. Ni jambo la kusikitisha sana.

Wakulima wanakopeshwa mbolea na wafanyabishara ambayo ni makampuni ya tumbaku. Makampuni haya yanakopesha mbolea kwa bei wanayotaka wao tena kwa bei ya dola. Mfuko mmoja wa kilo 50 wanakopesha kwa dola 60.2, ukipiga hesabu ni karibu Sh. 73,000/= au Sh. 75,000/= kwa mfuko mmoja.

Kwa hiyo, mkulima huyu anaendelea kuilimia kampuni. Serikali hii inajua, ni kwa nini kwa kutambua mchango wa tumbaku kwenye uchumi wa Taifa, Serikali imeshindwa kuwasaidia wakulima hao? Wakulima wa Tabora baada ya kuona kwamba zao la tumbau

haliwasaidii, wameamua kubadilisha sasa na kuingia kwenye mazao mengine, wanalima karanga, mahindi, ufuta na kadhalika lakini hakuna ruzuku ya mbolea inayotolewa pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sasa kwa Muswada huu itoe kipaumbele kwa wakulima wa Mkoa wa Tabora wanaingiza pato kubwa sana kwa Taifa, Serikali itambue mchango wa wakulima hawa na iwasaidie ili waweze kujinufaisha na waweze kuinua vipato vyao na waweze kuendelea kuchangia pato la Taifa kwa wingi zaidi. Hii tabia ya kuwaachia makampuni kufanya kama wanavyotaka imekuwa inawadidimiza wakulima wa Tabora na ni kilio kila siku. Hapa ninasema, lakini hakuna hatua zinazochukuliwa. Naomba sana, Muswada huu nina imani utatoa na majibu yatakayowasaidia wakulima wa Tabora na wakulima wa tumbaku waweze kunufaika vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumaini yetu sasa kwamba Muswada huu ambao ni muhimu sana utaweza kutoa majibu mazuri, kuweka taratibu nzuri ambazo wakulima wataweza kupata tija kwa kupata mbolea kwa bei inayotakiwa, yaani *standard price*, mbolea ya kiwango kinachotakiwa na kwa wakati unaotakiwa ili tuweze kulima kwa tija na hivyo kuweza kuwa na ile dhana ambayo tunasema kwamba tunaboresha kilimo kwa kutumia mbolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie katika Muswada huu. Naomba niungane na wenzangu kumwomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Marehemu Kabuzi Faustine Rwilomba mahali pema Peponi na aiimarishe familia yake waweze kustahimili msiba huu mgumu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo chetu ni kilimo ambacho kiko nyuma sana. Tija katika kilimo ni ndogo sana na kutokana hali hiyo wananchi wetu wengi, zaidi ya 70%, ambao wanaishi vijijini, wanakotegemea kilimo, hali zao sio nzuri, ni hali za umaskini.

Kwa hiyo, Muswada huu ni muhimu sana na ninaomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kuuleta hapa Bungeni kwa sababu ni Muswada unaoweka utaratibu wa kuingiza mbolea nchini, kuzisambaza, kuzihifadhi na kuhakikisha kwamba zinawafikia wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mjumbe wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji chini ya Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Gideon A. Cheyo. Tulipitia Muswada huu kwa umakini mkubwa sana tukaridhika kwamba Muswada huu katika hali yake inayoletwa Bungeni sasa uko katika hali ya kuweza kutekeleza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mbolea ni ya lazima katika maeneo yote ya nchi hii, Mikoa ya kusini, *the Big Four,* bila mbolea hawazalishi kabisa! Ukiotesha mahindi Iringa, Mbeya, Rukwa na Ruvuma kama hukutumia mbolea utavuna sifuri, hutavuna

chochote! Mbolea ni ya lazima na kazi ya mbolea ni kuweka katika udongo virutubisho ambavyo ama vimeondolewa na maji au mimea na kwa hiyo havipo tena katika ardhi. Kwa hiyo, mbolea ni ya lazima sana.

Huu Muswada ninapata taabu kidogo kuzungumza baada ya Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya, lakini nasema huu Muswada unaweka utaratibu wa kuingiza mbolea. Kwamba mbolea zikiingizwa humu nchini zitafanyiwa kwanza uchambuzi, zitajaribiwa mashambani kabla hazijaruhusiwa kwenda kwa mkulima. Kwa hiyo, kuna utaratibu umewekwa kabisa utakaohakikisha kwamba hakuna madhara yatakayotokea kwa mkulima kwa sababu ya mbolea hizo zitakazoingizwa kutoka nje. Kwa kweli ni Muswada mzuri, umeandaliwa kwa umakini na ninafikiri una manufaa makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikumbushe Bunge lako Tukufu kwamba Watanzania tunatumia kiasi kidogo sana cha mbolea. Inakisiwa kwamba tunatumia kiasi cha kilogram 6 – 7 kwa hekta. Ingekuwa ni chumvi umeweka kwenye chakula hutasikia hata harufu yake. Ni kiasi kidogo sana cha mbolea tunachotumia.

Kwa hiyo, kuna ulazima wa kuongeza matumizi haya ya mbolea kwa kiwango kikubwa sana. Wenzetu wa Malawi wanatumia kilogram 16, Kenya wanatumia, nafikiri 26 na ukienda katika baadhi ya nchi za Ulaya wanatumia zaidi ya kilograms 220 kwa hekta, lakini sisi tunatumia kilogram 6, kwa hiyo mnaweza kuona tofauti na hii mbolea inayotumika humu nchini sehemu kubwa inatumika katika mashamba makubwa na siyo katika mashamba yetu madogo madogo. Kwa hiyo, kwa kweli tunahitajika kuagiza mbolea kutoka nje kwa wingi, kuisambaza kwa umakini mkubwa ili imfikie mkulima na iweze kumwezesha mkulima kuongeza uzalishaji wa mazao yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hatukutumia mbolea kwa wingi, hakutakuwepo na *"green revolution"* na wala hatutaweza kupambana na huu umaskini na kuupunguza. Ni lazima tutumie mbolea kwa wingi ili kuongeza uzalishaji wa mazao mashambani. Mimi naamini kabisa kwamba kwa eneo tunalolima la hekta kama milioni 10, kama tungetumia mbolea na tukaitumia kwa usahihi lingeweza likazalisha zaidi ya mara tano ya kiasi ambacho tunazalisha sasa. Kwa hiyo, tungejitosheleza kwa chakula, tungezalisha ziada ya chakula ambacho tungeweza kuuza nje na mazao ya biashara nayo yangeongezeka kwa kiwango kikubwa sana. Kwa hiyo, tunahitaji kutumia mbolea kwa wingi na tunahitaji kuagiza mbolea hii kutoka nje lakini tunahitaji vilevile kutengeneza mbolea humu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo ambalo mara nyingi sana hatulitambui. Upatikanaji wa mbolea nje ni wa matatizo. Kuna miaka ambayo huwezi kupata mbolea kiasi unachohitaji, hasa wakiingia wanunuzi wakubwa kama Marekani na Wachina na nchi nyingine ambazo zina kilimo kikubwa.

Kwa hiyo, ni lazima Tanzania tujihakikishie upatikanaji wa mbolea kwa ajili ya kilimo chetu ambacho wote tunakubali kwamba ndicho msingi wa maisha na uchumi wa Tanzania. Ndiyo maana nakubaliana na wote wanaopendekeza kwamba mbolea izalishwe humu nchini na Sheria inatambua umuhimu huo na inaweka utaratibu wa kuwezesha

mbolea kuzalishwa humu nchini na kusimamia uzalishaji huo. Tuna raslimali za kutuwezesha kuzalisha mbolea humu nchini; tuna gesi katika maeneo matatu na ninaambiwa Mkuranga imepatikana gesi nyingine nyingi sana karibu na Dar es Salaam na karibu na njia kuu za usafiri. Tunaomba Serikali iweke mpango wa kutumia gesi hii kuzalisha mbolea za aina ya *nitrogen, ammonium* na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna *phosphate deposits* mahali pa tatu nchini, Minjingu, Mpanda na Mbeya, tutumie hizi *phosphate* kuzalisha mbolea za *phosphate* kwa ajili ya kutumia katika mashamba yetu, Sheria inaruhusu na inaweka utaratibu wa kusimamia utengenezaji wa mbolea hizo ili kuhakikisha kwamba zinatengenezwa kwa kiwango cha kuridhisha na bila kuathiri mazingira na kilimo kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Muswada huu inaanzishwa Bodi na Bodi itakuwa na Kamati ya Wataalamu na ukiangalia Wajumbe wa Kamati ile ya Watalaamu ni Wajumbe ambao wanatokana na vyombo vyote ikiwa ni pamoja na vyombo vya mazingira. Kwa hiyo, huu mfumo unaowekwa ni mfumo mzuri utakaohakikisha usimamizi wa makini wa matumizi ya mbolea katika nchi yetu na ni mfumo ambao kwa kweli unajitosheleza. Tunachoomba ni kwamba gharama za kuendesha vyombo hivi ziwe ni za Serikali na zisiongezwe kwenye mbolea kwa sababu mbolea, kama alivyoeleza ndugu yangu Mheshimiwa Yono Kevela, tayari ziko juu mno. Kwa hiyo, Serikali ibebe gharama za kuendesha Bodi hii ya Mbolea, ibebe gharama za kuendesha Kamati zake na shughuli zake nyingine kama inavyofanya kwa Bodi za Mazao. La sivyo mkulima atapata matatizo sana kununua mbolea hii ambayo bei zake ni kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo mengine mawili ambayo ningependa kuyagusia. La kwanza ni lile alilolizungumzia ndugu yangu Mheshimiwa Yono Kevela kwamba ni lazima mbolea ifungashwe katika viwango ambavyo mkulima anaweza akavitumia. Kwa mfano, mkulima mwenye shamba dogo anahitaji kilogramu chache tu za mbolea, lakini akienda dukani anakuta mfuko wa kilo 50. Sasa kilo 50 afanyie nini naye mahitaji yake ni kilo mbili au tatu? Hatujaweka utaratibu wa kuhakikisha kwamba mbolea inauzwa katika viwango ambavyo vinamwezesha kuvitumia.

Vilevile ni kwamba, mbolea sasa bei zake zipo juu sana na inatokana na kupanda sana kwa bei ya mafuta. Kwa hiyo, nategemea kushuka kwa bei ya mafuta kutasababisha kushuka vile vile kwa bei ya mbolea. Lakini tunahitaji mbolea ifungashwe katika viwango ambavyo mkulima ambaye analima bustani anaweza akanunua kilo zake tano, anahitaji kilo 10 anaweza akanunua kilo 10, anayehitaji kilo 50 akanunua kilo 50 na anayehitaji hata zaidi ya hapo akanunua zaidi ya hapo. Tunaomba hili lizingatiwe na kwa kweli litekelezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mkulima, wakati mwingine ninahitaji mbolea kidogo, nakwenda dukani wananiambia kuna mfuko wa kilo 50. Nikichukua mfuko wa kilo 50 nikatumia hapo kilo 5 zile kilo nyingine nisipozihifadhi vizuri hazitakuwepo kwa ajili ya matumizi ya msimu unaofuata inakuwa zimekwishaharibika. Kwa hiyo, tunaomba hili litazamwe.

La pili, suala la usambazaji litazamwe. Katika maeneo mengi utakwenda maili nyingi sana kabla hujafika mahali inapouzwa mbolea. Kwa mfano, ukichukua hata mfano wa Mkoa wa Ruvuma, ukitaka mbolea utaipata pengine Namtumbo ama Songea hutaipata karibu na maeneo wanapoishi wakulima. Ukienda Iringa tatizo ni hilo hilo, utaipata Makambako; ametueleza Mheshimiwa Yono Kevela pale, utaipata Iringa na utaipata pengine Njombe, lakini hutaipata kijijini. Kwa hiyo, tunaomba uwekwe utaratibu ambao utawezesha wafanyabiashara pamoja na Vyama vya Ushirika kuchukua mbolea hizo na kuzipeleka karibu na wakulima ili mkulima anapoihitaji aweze kutoka nyumbani kwake anunue na arudi shambani kwake. Sasa hivi mbolea ni kitu ambacho unakipata kwa taabu sana. Sisi wa Dar es Salaam hali ni mbaya hata zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina hakika watu wengi sana ukiwauliza utapata wapi mbolea Dar es Salaam wanaweza wasijue. Maana mbolea inapatikana Kariakoo na kama unaihitaji labda uende Kibaha. Tuna matatizo sana na mbolea. Kama ni kitu kweli ambacho kinahitajika kwa kilimo ili kumwezesha mkulima kuongeza uzalishaji wa mazao yake, ni lazima ipatikane kwa urahisi. Pale panapopatikana jembe, panga, papatikane pia na mbolea ili mkulima akienda pale ananunua mahitaji yake halafu aondoke kurudi kwenda shambani kwake.

La mwisho ni hili suala la bei na Serikali imejitahidi sana kutoa ruzuku ili kupunguza gharama za ununuzi wa mbolea, lakini bado bei za mbolea zipo juu sana. Mbolea aina ya *DAP*, sasa hivi mfuko mmoja wa kilo 50 ni zaidi ya Sh. 100,000/=. Tunaomba Serikali iliangalie suala hili na nini tufanye kuhakikisha kwamba mbolea inapatikana kwa wingi, kwa wakati na ipatikane karibu na mkulima na kwa bei ambayo mkulima anaimudu. Hii bei ya mfuko mmoja wa kilo 50 kwa Sh. 100,000/= au laki moja na zaidi wakulima wengi hawataimudu. Inabidi kwa kweli bei ya mbolea ishuke ili imwezeshe mkulima kuinunua kwa wingi na kuitumia kwa mazao yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi nichangie katika Muswada huu. Kwanza kabisa napenda nichukue nafasi hii kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya wapiga kura wa Jimbo la Kwimba kuwapa pole familia ya Marehemu Mheshimiwa Faustine Rwilomba pamoja na wapigakura wake. Kweli tumejisikia vibaya sana na tumeumia sana hasa sisi watu wa Mkoa wa Mwanza kama alivyosema Mwenyekiti wetu, ni jambo la kusikitisha sana. Alikuwa ni kiungo muhimu sana katika Wabunge wa Mkoa wa Mwanza. Kwa hiyo, tunamwomba Mwenyezi Mungu apumzishe roho ya Marehemu mahali pema Peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nimeshawishika kusimama kuchangia katika Muswada huu kwa sababu chache sana. Kwanza, napenda nichukua nafasi hii kuipongeza Serikali kuleta Muswada huu, ni Muswada mzuri sana na mimi moja kwa moja ninaunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mbunge wa Jimbo la Kwimba, kwa muda mrefu sana nimeshindwa kufanya kampeni ya matumizi ya mbolea katika Jimbo langu na

hasa mbolea ya chumvi chumvi. Mbolea ya chumvi chumvi ni kweli ina faida nyingi sana; ina faida ya kuongeza mazao katika mashambani yetu ambalo ni jambo jema, lakini watu wengi wanaangalia faida hiyo tu bila kuangalia athari zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbolea ya chumvi chumvi ina athari kubwa kwa udongo na hasa kama eneo hilo litakuwa limepungukiwa maji, mazao yanaweza kuwa kidogo zaidi kuliko ambavyo ungeweza kutegemea na Jimbo la Kwimba sio eneo ambalo tuna mvua nyingi sana. Kwa hiyo, nilikuwa na wasiwasi kwamba tukifanya kampeni ya matumizi ya mbolea ya chumvi chumvi inawezekana tukapata hasara kubwa zaidi kuliko kutokutumia mbolea hiyo. Lakini athari nyingine ya mbolea ya chumvi chumvi ni kwenye mimea. Ni kweli kama nilivyosema, mbolea ya chumvi chumvi inaongeza mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa kuangalia matokeo mazuri ya kupata mazao mengi zaidi peke yake haitoshi. Lazima tuangalie vilevile mazao hayo yana athari gani kwa binadamu. Kwa hiyo, ukiangalia vitu vyote hivyo lazima uwe na mashaka juu ya kufanya kampeni ya matumizi ya mbolea ya chumvi chumvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sheria hii sasa, nimeshawishika leo kuwaomba wapigakura wa Jimbo la Kwimba na wenyewe sasa waanze kufikiria kutumia mbolea ya chumvi chumvi na hasa sheria hii itakapoanza kufanya kazi na kwa makini zaidi. Kweli mbolea ya chumvi chumvi itasaidia kuongeza mazao, lakini bila kuwa waangalifu sana athari zake ni kama nilivyozisema.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naangalia hii sheria, hasa ile Kamati ya Wilaya, mimi ninaamini kama Kamati hii itafanya kazi vizuri sana, tutaweza kupata matokea mazuri sana. Mheshimiwa Waziri amepewa jukumu la kuteua Wajumbe wa Kamati hiyo na mimi ningemwomba Mheshimiwa Waziri awe makini sana katika uteuzi wa Kamati hiyo ili iweze kusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini hao watu ambao watateuliwa wengi watakuwa wanatoka katika mazingira hayo hayo, kama kweli watakuwa ni wataalam wa matumizi bora ya mbolea watatoa ushauri mzuri sana. Lakini kama hawatakuwa makini wanaweza kusababisha madhara makubwa sana katika maeneo yao. Kwa hiyo, hata wale watakaokuwa wanapendekeza yale majina, nawaomba sana wawe makini katika kupendekeza majina hayo kwa sababu wakipendekeza vibaya watakuwa hawamsaidii sana Mheshimiwa Waziri kuweza kuteua Wajumbe wazuri sana kwa Kamati hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipokuwa naipitia sheria hii, nimekuta kuna maeneo fulani ambayo nilikuwa nafikiri kwa sababu mimi siyo mtaalam sana wa Uandishi wa Sheria ningependa labda kusaidiwa. Ukurasa wa tisa chini ya Kamati ya Wilaya Na.2 nilikuwa nafikiri kuna neno ambalo limesahaulika. Wanasema kwamba: "*The Committee shall be composed of not less six and not more than nine…!*" Nilikuwa nafikiri kwamba kati ya neno *less* na *six,* neno *than* lingeweza kuwekwa pale.

**NAIBU SPIKA:** Kifungu gani Mheshimiwa Bujiku Sakila.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Kifungu cha pili, sehemu ya pili.

**NAIBU SPIKA:** Sehemu ya pili, ahaa kifungu cha sita.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Kifungu cha sita, namba mbili.

**NAIBU SPIKA:** *Okay*.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Kati ya neno *"less"* na *"six"* neno *"than"* lingeweza kuwekwa pale. Lakini vilevile katika sehemu hiyo hiyo Na.3 kwenye Kamati hiyo ya Wilaya, naongelea juu ya Kamati ya Wilaya itaishauri Kamati, nilikuwa nashindwa kuelewa hii ni Kamati ipi? Ni Kamati hiyo hiyo inajishauri?

Halafu Na. 3(e) nashindwa kuelewa nikisoma: *"participate in, or supervise the dissemination of educational campaigns and other and undertakings to provide the public with accurate information…!"* Nilikuwa nafikiria baada ya neno *undertakings* ile *"to"* imekuwa ni jukumu lingine tena badala ya kuunganishwa. Hayo ni masahihisho ambayo ningependa kufafanuliwa maana yake ni nini au kuwekewa masahihisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kifupi sheria hii ni nzuri na inahitaji umakini, lakini ninachotaka kumalizia nilipokuwa nawasikiliza wachangiaji wengine wamekuwa wakiongelea mbolea ya chumvi chumvi kutoka Minjingu kama nimewaelewa vizuri, wameongea kwamba mbolea hii ina kasoro. Kwa bahati nzuri mimi sijawahi kuiona. Lakini ninachotaka kutoa tahadhari, kiwanda hiki ni kipya na kwa sababu ni kipya unapoanzisha kiwanda ujue kwamba kutatokea kitu kingine kipya, unaingia kwenye mashindano. Kwa hiyo, unaingia kwenye vita.

Mimi nilichokuwa nashauri, uchunguzi wa makini ufanywe ili kweli kuthibitisha kama hiyo mbolea ina upungufu au ni kwa hujuma ambayo imefanywa katika kiwanda hicho, kwa sababu tunaweza kwenda haraka haraka kumbe tunasaidia watu wengine. Naomba sana uchunguzi ufanywe kwa makini nje na ndani ya kiwanda hicho, hicho ni kiwanda cha nchi yetu ambacho ndicho mkombozi wa wananchi hasa tunapoongelea juu ya upatikanaji wa mbolea. Lakini wapo watu ambao wananufaika na mbolea kwa utaratibu wa zamani. Kwa hiyo, unapotengeneza tena mbolea hapa hapa nchini, kuna uwezekano mkubwa sana wa upotoshaji kwa sababu utakuwa unawaharibika maslahi yao.

Kwa hiyo, mimi sisemi kwamba hiyo mbolea ni nzuri, lakini ninachoomba tu ni kwamba ufanyike utafiti wa makini na wa kizalendo kama hiyo mbolea kweli haina manufaa isiendelee, lakini kama hiyo mbolea inahitaji kufanyiwa marekebisho, hayo marekebisho yaweze kufanywa haraka ili wananchi wasiendelee kuumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Bujiku Sakila vile vifungu ulivyosema katika *Schedule of Amendments* vimefutwa, wame-*delete clause* 3, 4, 5 na 6. Kwa hiyo, nadhani kama walivyosema *Schedule of Amendments* ililetwa wakati wanaendelea na Muswada, wengi walishindwa kulinganisha. Tunaendelea. Mheshimiwa Said Arfi simwoni, namwita Mheshimiwa Lukas Siyame atafuatiwa na Mheshimiwa Fuya Kimbita na Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu ajiandae.

**MHE. DR. LUKA J. SIYAME:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ili nami nishirikiane na wenzangu katika kuchangia Muswada huu wa mbolea. Awali ya yote napenda kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Mbozi hususan wale wa Mbozi Magharibi niungane na wenzangu katika kutoa pole kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Kabuzi Faustine Rwilomba na wananchi wote wa Busanda kwa kumpoteza Mbunge makini, shujaa, kipenzi cha kila mtu na kwa kweli tumepoteza mtu makini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba nirudi kwenye Muswada huu. Kwa hakika kwa leo nilikuwa sina nia ya kuchangia hasa baada ya kuona wale walionitangulia wameongea kwa ufasaha na kwa hakika niseme kabisa nakubaliana na Muswada na nauunga mkono, ila basi kutokana na kwamba wakati nimeketi hapa nimepata simu hata nilipotoka nje nimekumbana na waraka kutoka kwa wananchi wa Jimbo langu wakiwa na malalamiko maalum ambayo nitayatoa katika kujadili huu Muswada.

Kwanza kabisa kama sheria ilivyokusudia, Muswada huu una nia ya kuweka mazingira mazuri yanayoruhusu wadau wote katika sekta ya mbolea kushiriki kikamilifu katika mfumo mzima wa soko huria la mbolea. Naamini hapa tulipo hakuna hata mmoja wetu ambaye anakubaliana mia kwa mia kwamba wadau wote wanashiriki kikamilifu kwa usawa katika sekta hii. Naweza kusema kwa hakika wanaofaidi ushiriki huu ni wafanyabiashara. Kwa ujumla mkulima hajapewa nafasi ya kuweza kuchangia kwa faida yake. Maana yeye wakati wote yuko kwenye *receiving end*, kwa hiyo, wakati wote anaumia. Iko haja ya kuhakikisha tunaweka mazingira ya mkulima katika hali ile ambayo yeye atajiona Muswada huu unamsaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la Kamati. Naafiki kabisa kuwepo kwa Kamati ya Taifa ya ushauri katika masuala ya mbolea na kuwepo Kamati katika Halmashauri za Wilaya katika haya masuala ya mbolea ni jambo sahihi kabisa. Lakini katika hili naamini watalaam wanahitaji kwa kweli kuainisha kila eneo kuwa na aina ya mbolea ya pekee maana yake ardhi ya nchi hii kama wenzangu walivyokwishazungumza inatofautiana kutoka eneo moja hadi lingine. Hivyo mbolea inayopelekwa kwa mfano katika jimbo langu la Mbozi Magharibi ambalo lina Kanda mbili, ukanda wa juu na ukanda wa bonde la ufa, wahakikishe mbolea inayopelekwa ukanda wa bonde la ufa ni tofauti kabisa na ile inayopelekwa ukanda wa uwanda wa juu kwa sababu ukanda wa bonde la ufa una *advantage* ya kwamba yanapokuja majira ya mvua ule udongo unaotoka kwenye ukanda wa juu ikiwa nipamoja na kutoka kwa Mheshimiwa Zambi Mbunge wa Mbozi Mashariki, nafikiri udongo wake pamoja na mbolea wanayotumia watu wake

inakuja kwangu kwenye bonde la ufa. Hivyo mbolea inayohitajika pale kwangu labda ni ya kukuzia maana ya kupandia tayari ninakuwa nimeshapata kutoka kwa mwenzangu.

Sasa katika hilo tunahitaji kuwa makini katika utawanyaji wa hii mbolea. Kuna suala la usimamizi wa usambazaji wa mbolea. Katika hili ndiyo naomba niseme kwamba nimepokea simu kutoka kule jimboni kwa wananchi wakidai ile mbolea ya ruzuku ambayo kwa uzuri kabisa Halmashauri ya Wilaya ilivyoketi katika ugawaji imefanya mgao mzuri kwa kila sehemu iliyokuwa inahitajika. Lakini katika usambazaji, mawakala na watendaji naambiwa na baadhi ya Madiwani katika jimbo wameamua kuuza mbolea na zile *voucher* sehemu nyingine. Hivyo sasa hivi wanasema kuna Watendaji wa Kata katika hayo maeneo yangu ambao wameshindwa hata kwenda kwenye Kata zao kwa sababu ile mbolea haijafika na hivyo wamesababisha upungufu mkubwa wa mbolea kwa wale walengwa, hawajafikiwa, badala yake wameuziwa watu wengine na wamesha-*sport* maeneo ambayo hiyo mbolea imeuzwa. Sasa katika hali hiyo, tungeomba utaratibu mzuri wa usambazaji wa hii mbolea katika ngazi zote.

Napenda niseme kwamba mbolea pamoja na uzuri wake, lakini hizi *inorganic fertilizers* ni sumu pia, si kwa binadamu tu hata kwa udongo kwa sababu baada ya muda udongo huu unakosa vile virutubisho vyake vya asili. Hivyo katika maeneo fulani iko haja ya kusisitiza kwamba tunachohitaji *ni organic fertilizers* ikiwa ni pamoja na samadi na mboji ambayo hata gharama yake kwa hakika si kubwa kama hizi mbolea za viwandani. Kule kwangu naweza kusema hatuna *experience* ya mbolea ya Minjingu kwa sababu kwa mara ya kwanza ndiyo imegawiwa mwaka huu na kwa bahati mbaya kama nilivyosema ndiyo hii ambayo imeuzwa njiani, kwa hiyo, hatuwezi kuongelea lolote juu ya Minjingu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ARCHT. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii jioni hii ya leo, nami niungane na wenzangu katika kuzungumzia huu Muswada ulioko mbele yetu ambao tunaamini ni Muswada muhimu sana ambao nadhani tulihitajika tuwe tumeupata siku nyingi. Lakini nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kuuleta.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kusema kwamba naunga mkono hoja hii kwa sababu asilimia kubwa ya wananchi wa Tanzania ni wakulima. Lakini pia, niungane na Waheshimiwa wengine hapa ambao wameendelea kutoa salaam za pole na kumwombea mwenzetu, jirani yetu Mheshimiwa Marehemu Faustine Rwilomba ambaye ametangulia mbele ya haki. Tuzidi kumwombea kwa Mwenyezi Mungu ili azidi kumrehemu huko aliko na kuiombea ile familia yake uvumilivu na matumaini makubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kikubwa ambacho nami ningeona nikizungumzie katika Muswada tulionao mbele yetu kwa siku hii ya leo ni elimu. Naamini elimu ni kitu muhimu sana kwamba tukawatumie wale watalaam wetu wa ugani hata kama hawapo wa kutosha, lakini naamini watapatikana kwa sababu bajeti iliyopita na hata siku zilizopita

Mheshimiwa Waziri ametuhakikishia kwamba anao mpango kabambe wa kutupatia watalaam wa kilimo katika kila kijiji na nia na madhumuni ni kuwajengea nyumba waishi katika hivyo vijiji ili waweze kutoa elimu kwa wananchi wetu. Kuna umuhimu mkubwa sana wa kutoa elimu juu ya matumizi ya mbolea kwa sababu kwingine tunalima kwa mazoea tu au kwa kusikia fulani amefanya hivi pasipo kuelekezwa na mtalaam wa kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata haya malalamiko mengine ambayo tunayasikia hapa na mengine haya yamekuwa ni makali sana kuhusu hii mbolea ya Minjingu, natumaini ni elimu tu kwa sababu hawa watu wa Minjingu pale Wilayani kwetu Hai wameshatutembelea wakatufundisha na kikubwa nadhani walichosema ukiweka mbolea ya Minjingu kwenye ardhi mwaka huu haitakuletea yale matunda unayotarajia kwa mwaka huu au kwa msimu huu uliopo utarajie matunda mazuri zaidi msimu utakaokuwa unafuata kwa sababu ndiyo itakuwa imeshaingia ardhini na utaweza kupata vile virutubisho ambavyo vilikuwa vinahitajika kwenye ardhi yako. Ndio maana nazidi kusisitiza kwamba elimu ni muhimu zaidi na niwaombe wale wenzangu ambao labda wamezungumzia hii mbolea ya Minjingu kwa ukali kidogo na wale wananchi kuichukia, natumaini elimu ingekuwa imetolewa ya kutosha wangekuwa wameelewa vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa hiyo, kwa ujumla elimu ni kitu muhimu kujua jinsi gani ya kutumia mbolea na mbolea gani itumike. Kwa hiyo, nazidi kusisitiza suala la elimu wakati gani itumike mbolea gani ya kuoteshea, mbolea gani ya kukuzia mimea yetu ili tuweze kuelewa vizuri matumizi bora ya mbolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe kwa zile mbolea ambazo zitaweza kutengenezwa hapa nchini kutokana na malighafi tulizonazo na Mungu amebariki tumeendelea kupata *gas* asilia ambayo ni muhimu pia katika uzalishaji wa mbolea na madini mengine tuliyonayo. Zile mbolea zote ambazo tunaweza tukazitengeneza hapa nchini kutokana na malighafi tuliyonayo hapa nchini, niombe sana kwamba tuzitengeneze hapa nchini. Tumemsikia Mheshimiwa Rais, akiwa na jitihada kubwa sana hata kutafuta watu wa kuweza kuwekeza katika viwanda vya mbolea hapa nchini, tuombe zile jitihada tuziharakishe ili tuweze kuzalisha mbolea ambayo natumaini pia itapunguka bei kwa maana itakuwa *affordable* zaidi na itaweza kupatikana kwa wingi kadri tutakavyotarajia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesikia hata Mheshimiwa Charles Keenja amesema kuna wakati mwingine duniani unaweza ukawa unahitaji mbolea hata kama fedha unazo lakini usipate kutokana na mahitaji makubwa katika nchi hizi nyingine ambazo ni kubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba *packaging* ni muhimu ili kuwe na uzito mbalimbali, naweza nikawa nahitaji kiasi cha kilo 75 lakini sasa nitalazimika nikanunue kilo 100, hizi nyingine zitakuwa ni *wastage*, kwa hiyo, niombe katika hivi viwanda vitakavyojengwa hapa nchini, umuhimu wa ku-*pack* mbolea katika uzito mbalimbali nao usisitizwe hata ile inayotoka nje wakati mwingine inakuja *in bulk* kwa

hiyo, wakati wa *packing* ni vizuri pia tukaweza kui-*pack* katika *size* mbalimbali ambako pia itamsaidia mkulima wetu yule mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba pia Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa anisaidie kunielimisha pamoja na watu wengine matumizi ya mchanganyiko wa kutumia mbolea ya samadi pamoja na hizi mbolea za viwandani: Je, kuna athari au itakuwa ndiyo bora zaidi? Kule Wilayani kwetu Hai kwa sababu na wafugaji tunao pia tumeanzisha utaratibu ambao tunatumia mbolea ya samadi ile ambayo ni kavu iko katika fomu kama mchanga mchanga, wakati mwingine tunanyunyizia kwenye mashamba yetu tunakuja kuvuruga mashamba yale kwa maana ya kulima na kupiga *harrow*. Lakini pia wakati wa kuoteshea tunalazimika pia kutumia hiyo mbolea ya kuoteshea na kukuzia. Je, kuna athari au ni kitu kizuri zaidi? Kwa hiyo, nitamwomba Mheshimiwa Waziri, kwa utaalam wao watusaidie tujue kwamba je, hiyo ni sahihi au siyo sahihi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maneno mengine nilikuwa naomba pia tuweke msisitizo, mbolea ya samadi ninavyoamini mimi kwa sababu sisi ni watoto wa wakulima na tumeiona ikitusaidia, Hai imetusaidia sana katika kilimo chetu cha migomba ambako inatusaidia tunapata ndizi laini vizuri zinazokua vizuri. Kwa hiyo, ningeomba pia tusisitize matumizi ya hii mbolea ya samadi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ambacho ningependa kusisitiza hapa ni *soil analysis*. Nafahamu *soil analysis* kwa maana ya kutafiti vilivyopungua katika ardhi yetu ili watalaam waweze kushauri kwamba tuweke mbolea kiasi gani au mbolea aina gani. Lakini ningeomba kwamba iwe inafanyika mara kwa mara kwa sababu udongo unachakaa, mabadiliko mengine yanatokea. Mheshimiwa Profesa Mwalyosi alizungumza kile kiasi cha mbolea inayoingia ardhini na kusafirishwa kwa hiyo, ni vizuri tukawa tunafanya hizi *soil analysis* mara kwa mara ili kufahamu vizuri kwamba ni mbolea ipi kwa wakati huo sasa itumike. Sio lazima ninavyoamini mimi mbolea iliyotumika miaka mitatu, minne iliyopita iwe ndiyo hiyo hiyo inayohitajika kutumika kwa kipindi kama hiki tulichonacho hivi sasa.

Kwa hiyo, ningeomba tuzingatie zaidi kwenye mambo ya *soil analysis* pamoja na muda sahihi wa kuitumia ile mbolea. Wenzangu wameshazungumzia tumeshuhudia katika baadhi ya maeneo msimu wa kutumia mbolea ya kuoteshea umeshapita ndiyo inafika kwenye kijiji au kwenye Wilaya. Sasa hapo inashindikana kueleweka hata wale wananchi wanajiuliza hawa wakulima sasa tunaletewa mbolea ya kuoteshea kipindi hiki, wakati tungehitaji ya kukuzia, tunaletewa ya kuoteshea ije itusaidie kitu gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ningemwomba Mheshimiwa Waziri anisaidie kwa sababu tunazungumzia mbolea, lakini: Je, katika yale mazao ya muda mfupi sana kama mboga mboga tuna kabeji, nyanya na vitu vingine, haya matumizi ya mbolea kwenye mazao ya muda kama kabeji, karoti, mchicha: Je, hayo matumizi yana athari kiafya katika kutumia mbolea?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna gharama kubwa sana katika upande wa usafirishaji wa mbolea. Nami niungane na wenzangu kusema tunaomba mbolea ziwe

zinafikishwa jirani na mkulima kadri inavyowezekana. Nichukulie mfano hai kule Wilayani kwangu Hai, watu wamelalamika sana, kwa sababu utaratibu tuliokuwa tumepanga katika ugawaji wa mbolea tulikuwa tumekusudia kwamba vyama vya msingi au vyama vya ushirika, ndivyo vigawiwe mbolea viweze kuwafikishia wananchi. Lakini ukaja utaratibu mwingine baadaye kwamba ni wale ambao wataweza kulipa. Sijui kulikuwa na fedha za kulipa kwenda kwenye semina fulani kiasi kama cha shilingi laki mbili na nusu au kiasi gani ambako vyama vingi vya msingi havikuweza kulipa! Kwa hiyo, matokeo yake ni wafanyabiashara binafsi wamekuja kupewa ile mbolea. Lakini imekuwa ni usumbufu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilayani Hai tuna jiografia tofauti, kuna maeneo ya tambarare na maeneo ya milimani. Unakuta mkulima ana shamba kule tambarare lakini wakati wa kutumia mbolea bado inamlazimu akanunue kule kwa mfanyabiashara wa tambarare aende nayo mlimani. Pia ikifika wakati wa kwenda kuitumia arudi nayo tena kule tambarare, ni gharama zinazidi kuongezeka. Kwa hiyo, ningeomba tuangalie sana na kuna maelekezo mengi mno yamekuja kutoka ngazi za juu kiasi kwamba ilileta vurugu kiasi fulani ambako imemwongezea mkulima gharama kubwa sana katika usafirishaji na anayefaidi zaidi pale ni yule wakala binafsi kwa sababu yeye hana hasara.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kingine ambacho ningeomba nikiongelee hapa naishukuru Serikali imetoa mbolea ya ruzuku kwa maana ya *voucher system*. Lakini ruzuku hii imekuwa ni kidogo, sijui kwenye Mikoa mingine lakini kule kwangu Hai kumekuwa na ugumu sana jinsi ya kugawa zile *voucher*, zimekuwa chache mno. Kwa mfano kuna kijiji unakuta kinagawiwa *voucher* 45 za aina fulani ya mbolea sasa utampa nani utamnyima nani? Ningeomba kwamba kama tunakusudia kutoa hizi *voucher* tutoe kwa wingi na labda tukichukuliwa kule Hai labda kilimo hakifanyiki sana, kweli tuna uhaba wa ardhi lakini tunafanya kilimo cha kisasa sana ambapo pia tunahitaji hii mbolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, imefikia mahali kwa mfano kwenye mikutano mingine kwa mfano kwenye kijiji cha Saawe na maeneo mengine wananchi walikuwa wakali kidogo wakasema mmetutangazia kuna mbolea ya ruzuku na mbegu, mbegu hatujapata! Lakini tunashukuru mbegu zimefika hivi karibuni siku za nyuma kidogo kabla hatujaanza Kamati za Bunge. Lakini wananchi walikuwa wanalalamika mnatutangazia kwamba itakuwepo mbolea ya ruzuku wakati tunapata wachache mno ndani ya kijiji, bora msitutangazie. Mzee mmoja akawa na hasira kiasi cha kusema hata sitaki kusikiliza tena redio kwa sababu mnatutangazia vitu ambavyo havitimiziki. Kwa hiyo, ningeomba tu ni kutokana na uwezo Serikali ingependelea sana itoe *voucher* za kutosheleza kila mmoja wetu lakini uwezo ndio unakuwa kidogo. Lakini ningeomba kwamba tufikiriwe na sisi kule Hai pamoja na maeneo madogo ya kulima kilimo tunakifanya cha kisasa hivyo tungehitaji mbolea zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe ombi langu kuwa tumepata shida kule kwetu kaskazini sasa hivi, uhaba wa mvua, ukame umekuwa mkali sana kabla hatujaanza Kamati zetu za Bunge tumeweza kuzunguka katika vijiji vingi sana inafikia mahali roho inaumia, unakuta mibuni imekauka kwa sababu ya ukame maji ni kidogo, ugomvi katika kugawana zamu za maji ya kumwagilia. Sasa kutokana na hii hali ya mvua ilivyokuwa

ngumu watu walilima wengine wakajaribu kuotesha mapema mbegu, zimeharibika, lakini mchana huu nimezungumza na wapigakura wangu kule jimboni namshukuru Mungu kwamba nasikia kuna mvua nyingi imenyesha pia mchana huu kuanzia milimani mpaka tambarare. Sasa nilikuwa nimwombe Mheshimiwa Waziri kama kuna uwezekano pamoja na hiyo hasara wananchi wameipata atufikirie katika kutuongeza mbolea ya kukuzia nayo iwe ya ruzuku angalau kumfidia yule mwananchi au kumpa pole kutokana na ule ukame ambao umetokea ili tuweze kumpunguzia mwananchi hasara ambayo ameshaipata kwa hivi sasa tunavyozungumza. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nikuombe sana na wale wananchi wanakufahamu vizuri sana kwamba utufikirie kwa huruma kabisa tuweze kupata mblea ya kukuzia kwa wale ambao wamekuwa wameshaotesha kwa hivi sasa tunavyozungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kikubwa, niombe na nisisitize kuwa tathmini ya njaa ilifanyika lakini kutokana na ukame ambao nauzungumzia kwa wakati ule ilionekana kama tungepata mvua za vuli nazungumzia hilo liko nje ya mbolea lakini liko Wizara hiyo hiyo ya Kilimo kwa sababu tulipata shida ya upungufu wa mvua za vuli kwa hiyo hatukuweza kupata hata yale mazao ya muda mfupi. Kwa hiyo, kuna upungufu wa chakula au uhaba wa chakula. Ningemwomba Mheshimiwa Waziri atume wataalamu wake kule waweze kutambua hayo maeneo tuweze kuwasaidia wale wananchi ambao watakuwa na uhaba wa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ni Muswada mzuri, tulikuwa tunaouhitaji siku nyingi, lakini naomba elimu itolewe kwa wingi zaidi pia kwa nafasi hii kwa sababu niko hapa Dodoma kuwawakilisha hao wananchi wa Hai lakini niwape pole wananchi wa jimbo langu la Hai kwa kufiwa na Katibu Kata wetu wa Kata ya Machame Magharibi, Ndugu Phares Kimaro naye namwombea Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema Peponi na kuwapa pole wale ndugu wote walioguswa na huu msiba. Amen

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme naunga mkono hoja Muswada huu, ni mzuri sana, nami niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu tuweze kuupitisha ukafanye kazi haraka inavyowezekana ili tuweze kuwa na Mapinduzi makubwa katika kilimo chetu. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Asubuhi Naibu Waziri wa Nishati alisema umeme unakatikakatika kwa hiyo, sio uzembe ila miundombinu mibovu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu katika orodha ya wasemaji ninaye jina lake hapa. Mheshimiwa itabidi uhame, naona ushuke.

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Awali ya yote, kwa niaba yangu mwenyewe na wananchi wa Jimbo la Bukene naomba kutoa rambirambi kwa jimbo la Busanda kwa ajili ya kifo cha Marehemu Rwilomba, roho ya Marehemu ipate rehema kwa Mungu ipumzike kwa amani. Amen

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mmoja wa Wajumbe wa Kamati ya Kilimo, Maji na Mifugo kwa hiyo, ni mmoja ya wale tuliopitia huu Muswada na tumekubaliana

yale tuliyokubaliana mpaka ulipofika. Ila nataka kuongeza kidogo katika kusisitiza yatusaidie zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaanza moja kwa moja katika kuzungumzia hasa mambo ya ku-*pack*, *pack materials*. Kwa sababu *packing* zake za mbolea zinakuwa katika mifuko mikubwa ambayo wakulima wa kawaida ambao wanatumia jembe la mkono na ndio wengi zaidi wanashindwa kutumia mbolea hii. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiria na kama tulivyoshauri katika Kamati na mimi naendelea kusisitiza tungeomba na tunaendelea kuomba kwamba *packing* zake ziwekwe vile vile katika *packing* ndogo ndogo kama zile za kilo 5, 10 na kadhalika ili ziweze kumsaidia hata mkulima wa kawaida ambaye anahitaji mbolea kidogo tu labda kwa shamba lake dogo au bustani yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nahangaika kidogo katika kuangalia kupitisha mbolea hizi za chumvi chumvi hasa nikiangalia wale wenzetu waliotumia mbolea ya chumvi chumvi katika Mikoa ile *"Big Four"* na ukiangalia vile vile ukienda nje ya nchi kama Ulaya kwa mfano wanataka chakula au mazao ambayo yametumika au yamelimwa bila kutia mbolea ya chumvi chumvi. Ukiangalia kwenye jimbo langu, sisi kwa kweli tunatumia mbolea za chumvi chumvi hasa hasa kwa wakulima wanaolima tumbaku na wakulima wanaolima pamba, lakini kwenye mambo ya mahindi ni kidogo sana. Kwa kweli ukiangalia ardhi katika Tanzania kuna sehemu ambayo ardhi bado iko nzuri ina rutuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nataka kushauri kwamba kwenye sehemu ambayo ina rutuba bado na kweli hatuhitaji kuweka mbolea ya chumvi chumvi naomba tuwashauri wakulima wasitumie mbolea za chumvi chumvi maana ujuzi tuliopata kutokana na Mikoa ile minne iliyokuwa inatoa mazao mengi lakini ardhi inaharibika. Sasa kwa kuwa bado hatujapata utaratibu wa kuonyesha kwamba ikifika mahali fulani labda unapotengeneza na kulima ardhi yako ikifika katika aina hii unatakiwa kuiacha au kuifanyaje ili uweze kutumia sehemu nyingine kama vile kwetu. Kilimo cha asilia unalima kuna mashamba yanaitwa matongo, unalima mwaka huu sehemu hii halafu mwaka kesho unaliacha lile shamba unalima shamba lile la pili hili linapumzika. Kwa hiyo, pale pale unapokwenda kulima tunazoea kutumia mbolea asilia ambayo sisi vile vile ni wafugaji. Kwa hiyo, tunatumia mbolea ya mavi ya ng'ombe ambayo ni samadi.

**NAIBU SPIKA:** Wanasema kinyesi, sema samadi sio hivyo ulivyosema.

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Eehhh!!!?

**NAIBU SPIKA:** Inaitwa samadi

**MHE. TEDDY KASELA-BANTU:** Haiitwi samaki?

**NAIBU SPIKA:** Samadi.

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Kwani nimesemaje? Mavi ya ng'ombe ambayo yanaitwa samadi. Nimekosa nini sasa hapo, si ni mavi ya ng'ombe kweli. Ila Kiswahili safi sasa ndio samadi lakini ni nini? Ni mavi ya ng'ombe. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nataka kusema, ile samadi tunaiweka ndani ya shamba mwaka mmoja baadaye tena unakuja kulima, lakini shamba lingine unaliacha kwa ajili ya mwaka kesho ni kama unalipumzisha. Vile vile tulishaonyeshwa hata shuleni tulivyokuwa tunasoma Darasa la IV nafikiri na mimi nakumbuka Darasa la IV au wapi, lakini nakumbuka Shule ya Msingi wakati huo zilikuwa zinaitwa *Native Authority (NA)* au *Local Authority (LA)* tulikuwa tunafundishwa jinsi ya kuweka takataka hizi unazichimbia kwenye shimo halafu baada ya muda unatoa unakwenda kupeleka shambani ambayo ni mboji, si ndio?

Kwa hiyo, mimi nafikiri tuwapeleke wakulima wetu watumie mboji na samadi kwa wale ambao ardhi yao bado haijaharibika. Kwa sababu tukienda sisi wote kwenye kutumia mbolea hii ya chumvi chumvi na tukihamasisha wote nchi nzima watumie mbolea ya chumvi chumvi na baada ya miaka mitano au kumi ardhi yote ikiharibika tuwe tunategemea kutumia mbolea ya chumvi chumvi tutakuwa hatujawasaidia wananchi na vile vile tutakuwa tunahangaika maana yake hao hao Wazungu ndio wanaotucheza wanatuletea mbolea ya chumvi chumvi wanatuacha tutumie mbolea ya kwamba tunapata magunia mengi, tunafanya nini, halafu hao hao wanatuambia tena aah sisi hatutaki kununua chakula au mazao yote yaliyotumia mbolea ya chumvi chumvi tunataka mazao yaliyolimwa na kutumia mbolea asilia au hawataki kemikali. Kwa hiyo, mimi nafikiri tuwe na sehemu ambayo tunaweza kutoa chakula chetu na chakula kingine cha kuuza nje chochote kinachoweza kuingia ndani ya tumbo tutumie mbolea ya samadi na tutumie mbolea ya mboji.

Mheshimiwa Naibu Spika, wale ambao tunawapeleka kwenye kutumia mbolea ya chumvi chumvi ambao kweli ardhi zao zimeshachoka au pengine ardhi sio kwamba imechoka kwa sababu ya kemikali lakini pengine ardhi yenyewe ndiyo ilivyo. Kwa hiyo, tuwategemee zaidi wataalamu walioko katika kilimo waende waliosomea udongo wafanye kazi karibu na wakulima washauri cha kufanya toka mwanzo wawe nao karibu. Kwa kifupi, nataka kusema Mabwana Kilimo na Mabibi Kilimo yaani Maafisa Kilimo wasikae mezani, wasiwe Mamangimeza waende mashambani kabisa kwenye Kata, kwenye vijiji kwenye Vitongoji waende wakawafundishe wakulima wetu jinsi ya kuchanganya hizo kemikali na jinsi ya kutumia vizuri ili tuweze kupata mazao ya kutosha, kwa ajili ya kuuza na mengine ya kutumia nyumbani. Lakini ningependa tufuate ile asilia kwa sababu ya kuzuia kemikali inayoingia ndani ya mwili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa na lingine nilikuwa nataka kuzungumza, samahani kidogo.

**NAIBU SPIKA:** Hamjui kama alihama makazi? *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nataka kuzungumzia kuhusu ruzuku ya mbolea. Kwa kweli kwa kawaida hii ruzuku

inatoka inakwenda hasa hasa kwa wafanyabiashara na ikifika kwa wafanyabiashara inamnufaisha hasa mfanyabiashara. Mpaka sasa hivi haijamnufaisha mkulima. Kwa hiyo, naomba Wizara itafute mbinu ya kuhakikisha kwamba hii ruzuku inamfikia mkulima wa kawaida isiishie pale kwa mfanyabiashara. Kwa kuwa Wizara hii ni ya Kilimo, Chakula na Ushirika basi Maafisa Ushirika wahamasishwe kwenda kule mpaka vijijini waweze kuangalia kama wanaweza kufanya *SACCOS* au ushirika wowote wa wakulima ili waweze kupata pembejeo na kuuziana wao kwa wao ili wanufaike kwa kupata faida ya ruzuku hivi sasa inavyokwenda inaishia kwa wafanyabiashara tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nataka tena vile vile kusisitiza kwamba wakati wa zile gharama za Bodi na Kamati maana yake kutakuwa na watu watakaochaguliwa kufanya kazi hiyo ninasisitiza tu kama Mjumbe wa Kamati kwamba zile gharama zichukuliwe na Serikali ili zisiwe mzigo tena kwa kuingia maana ukishaiweka iingie tena kwa wale wafanyabiashara, basi utaona inakwenda tena, mtu anayekuja kuumia zaidi ni yule mkulima pale dakika ya mwisho ambaye ndiyo anayenunua hiyo mbolea. Kwa hiyo, naomba gharama zake zichukuliwe na Serikali.

La mwisho, lakini sio la mwisho kwa umuhimu na mimi naomba kutoa taarifa kwamba katika jimbo langu patakuwa kidogo na njaa mwaka huu, kwa hiyo, natoa kama taarifa. Mvua imekuja nyingi tukalima mpunga na kwa mpunga hatuna wasiwasi, lakini kama unavyojua tunapenda kulima mpunga kwa ajili ya biashara, lakini sisi ni walaji wa ugali. Mahindi hakuna yameshindwa kuvumilia, mvua iko nyingi, yamekuwa mekundu na yameharibika. Kwa hiyo, tunaomba wakati mnapopanga mambo ya chakula cha njaa mfikirie vile vile kwenda Bukene na kuangalia hali halisi ilivyo. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:**Waheshimiwa Wabunge, niliokuwa nao kwenye orodha wamebaki watatu, lakini naambiwa kuna kikao mahali ambapo hawa wamepaswa kuwepo. Kwa hiyo, tutaendelea kesho asubuhi baada ya kipindi. Kesho si mnafahamu ni Alhamisi, kwa hiyo kuna kipindi cha Maswali kwa Waziri Mkuu! Kwa hiyo, tutaangalia kama hao watapewa nafasi au tutaingia moja kwa moja na Mheshimiwa Waziri kuanza kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge na kuingia kwenye Kamati ya Bunge Zima. Kwa hiyo, kwa sasa sina matangazo mengine, napenda kuahirisha kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.15 Usiku Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Alhamisi Tarehe 23 Aprili, 2009 Saa Tatu Asubuhi)*